

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Ishirini na Tano – Tarehe 8 Mei, 2020

(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA NISHATI:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

MHE. USSI SALUM PONDEZA AMJADI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI):

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati Fungu 58 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wa Wizara ya Nishati. Hayupo. Katibu.

NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI

MASWALI NA MAJIBU

(Maswali yafuatayo yameulizwa na kujibiwa kwa njia ya mtandao)

Na. 231

Uhaba wa Walimu – Mkoa wa Tanga

MHE. OMARI A. KIGODA aliuliza:-

Kutokana na uhaba wa walimu Mkoa wa Tanga umekuwa haufanyi vizuri katika matokeo ya ufaulu wa wanafunzi:-

Je, kuna mkakati wowote wa Serikali wa kutatua changamoto hiyo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MITAA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omari Abdallah Kigoda, Mbunge wa Handeni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuajiri Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari nchini ambapo kuanzia mwaka 2017 hadi 2019 jumla ya walimu 420 wameajiriwa na kupangwa katika Mkoa wa Tanga. Walimu 130 walikuwa wa Shule za Msingi na walimu 290 walikuwa wa Shule za Sekondari. Serikali itaendelea kuajiri Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari nchini kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

Na. 232

Kukamilisha Ujenzi Kituo cha Afya Mtii – Same

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya kinachojengwa Kata ya Mtii ambapo hakuna hata zahanati ya Serikali?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MITAA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Same Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kata ya Mtii kwa kushirikiana na Halmashauri na wadau wa maendeleo wamekamilisha ujenzi wa jengo moja lenye vyumba 14. Serikali inakamilisha taratibu za kuiombea zahanati hiyo ili ianze kutoa huduma. Serikali itaendelea kujenga vituo vya afya na zahanati kadri upatikanaji wa fedha utakavyoruhusu.

Na. 233

Kufufua Viwanda Vilivyoko Mkoani Tanga

MHE. SONIA J. MAGOGO aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua viwanda vilivyoko Mkoani Tanga ambavyo vilikuwa na tija kubwa sana kwa Taifa?

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Sonia Jumaa Magogo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Tanga ulikuwa na jumla ya viwanda 12 vilivyobinafishwa wakati wa zoezi la ubinafishaji vinavyojumuisha viwanda vya mbao, chai, sabuni na katani.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa jumla wa Serikali katika kushughulikia viwanda vilivyobinafishwa ni kufanya ufuutiliaji na tathmini, kushauri wawekezaji kuhusu maboresho yanayopaswa kufanywa, kurejesha viwanda na kutafutia wawekezaji wengine wenye uwezo wa kuwekeza na kutafuta wawekezaji wapya.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mkakati huo, Serikali ilifanya tathmini ya utendaji wa viwanda vilivyobinafishwa ikiwemo viwanda katika Mkoa wa Tanga na kubainisha kuwa kuna jumla ya viwanda 12. Kati ya hivyo, viwanda viwili vinafanya kazi kwa ufanisi; viwanda sita vimerejeshwa Serikalini na viwanda vinne vinafanya kazi kwa kusuasua.

Mheshimiwa Spika, katika viwanda sita vilivyorejeshwa Serikalini, Kiwanda cha Chai cha Mponde kuna mwekezaji aliyeonesha nia ya kukifufua.

Aidha, Serikali itaendelea kutafuta wawekezaji watakaoweza kuwekeza katika viwanda vingine vilivyorejeshwa Serikalini na kuhamasisha wawekezaji wengine wanaoendesha viwanda vinavyozalisha chini ya uwezo uliosimikwa waongeze uzalishaji.

Na. 234

Ujenzi wa Barabara ya Londo – Songea Km 113

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Londo - Songea ambayo inaunganisha Mkoa wa Morogoro na Ruvuma yenye urefu wa kilometra 113 ambayo imekuwa ikiongelewa kwa muda mrefu sana na madaraja yalishajengwa na kilichobaki ni kuunganisha barabara hii?

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Londo – Songea (Lumecha) yenyeye urefu wa kilometra 124 ni sehemu ya barabara Kuu ya Kidatu – Ifakara – Malinyi – Kilosa kwa Mpepo – Londo – Lumecha (km 512) inayounganisha Mkoa wa Ruvuma na Morogoro kuititia Wilaya za Kilombero, Ulanga, Malinyi na Namtumbo.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza azma ya kujenga barabara hili kwa kiwango cha lami, Serikali imefanya na kukamilisha kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara yote.

Mheshimiwa Spika, kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami imeendelea kutekelezwa kwa awamu ambapo ujenzi wa Daraja la Magufuli katika Mto Kilombero lenye urefu wa mita 384 na barabara unganishi zenyeye urefu wa kilometra 9.142 ulikamilika tarehe 30 Julai, 2017. Aidha, ujenzi wa barabara ya Kidatu – Ifakara (km 66.9) kwa kiwango cha lami unaendelea. Ujenzi wa sehemu iliyobaki ikiwemo Londo – Lumecha (km 124) kwa kiwango cha lami utaendelea kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa sehemu ya barabara kutoka Londo – Songea (km 124) kiuchumi na kijamii, Serikali kuititia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) Mkoa wa Ruvuma, inaendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali barabara hili kila mwaka ili iweze kuitikika majira yote ya mwaka. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, barabara hili imetengewa jumla ya Sh.1,068,795 kwa ajili ya matengenezo mbalimbali.

Na. 235

Tatizo la Ardhi Kati ya Hifadhi na Wananchi – Wilaya ya Wang'ombe

MHE. NEEMA W. MGAYA aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatatua tatizo la ardhi kati ya Hifadhi ya Mpanga – Kipengele na Vijiji vya Malangali, Wangomiko na Mpanga mpya katika Wilaya ya Wang'ing'ombe Mkoa wa Njombe?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uwepo wa vijiji vya Malangali, Wangomiko na Mpanga mpya ndani ya Pori la Akiba Mpanga -Kipengele kabla ya kuanzishwa kwake. Moja ya hatua iliyochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na changamoto hiyo ni uthamini wa mali za wananchi na ulipaji fidia kwa mujibu wa sheria ili wahame. Mfano, mwaka 2007 wananchi 325 wa vijiji vya Iocco, Usalimwani na Kigunga vya Wilaya ya Makete walilipwa jumla ya Sh.190,067,151. Mwaka 2012 wananchi 161 wa Kijiji cha Iocco waliolalamika kupunjwa walilipwa jumla ya Sh.829,841,000. Aidha, mwaka 2018, Serikali ililipa fidia jumla ya Sh.837,071,100 kwa wananchi 308 wa Kitongoji cha Machimbo katika Kijiji cha Madabada, Wilayani Mbarali.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa migogoro ya ardhi baina ya vijiji na hifadhi, likiwemo Pori la Akiba Mpanga-Kipengele, Serikali imekuwa ikiweka alama za kudumu (vivingi) zinazoonekana kuzunguka mipaka ya hifadhi. Aidha, jumla ya alama za kudumu (vivingi) 152 kati ya 494 zimekewka kuzunguka mpaka wa Pori la Akiba Mpanga-Kipengele kwa ushirikiano na Serikali za mikoa, wilaya na vijiji husika. Zoezi hili linaenda sambamba na utoaji wa elimu kwa

wananchi kuhusu sheria na kanuni zinazosimamia maeneo ya hifadhi na umuhimu wa utekelezaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi baina ya maeneo ya hifadhi na vijiji nchini, unafanyiwa kazi na Kamati ya Mawaziri wa Sekta nane ambazo ni wadau wa matumizi ya ardhi. Hivyo, Vijiji vya Malangali, Wangomiko na Mpanga mpya ni mionganoni mwa vijiji vinavyofanyiwa kazi na Kamati hiyo ambapo utekelezaji wa zoezi la utatuzi wa migogoro katika maeneo hayo utaendelea kufanya kwa kufuata uamuvi wa Baraza la Mawaziri. Utekelezaji huu ni shirikishi na utahusisha Serikali za mikoa na wilaya husika.

Mheshimiwa Spika, Wizara inawaomba wananchi kuzingatia na kufuata Sheria za Uhifadhi wa Wanyamapori pamoja na kuacha kuvamia maeneo mapya na kuwa wavumilivu wakati Serikali ikifanyia kazi migogoro hiyo. Vilevile, halmashauri za wilaya zinakumbushwa kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa vijiji vinavyopakana na maeneo ya hifadhi ili kupunguza migogoro kati ya wananchi na wahifadhi.

Na. 236

**Leseni Zilizotolewa na EWURA kwa Wazalisha Umeme
Wadogo**

MHE. JUMA OTHMAN HIJA aliuliza:-

Moja kati ya kazi za Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (*EWURA*) ni kutoa leseni za kufanya biashara ya umeme:-

Je, ni leseni ngapi zimetolewa kwa Wazalishaji Wadogo (*Small Power Producers*) katika kipindi cha mwaka 2017 – 2018?

WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Juma Othman Hija, Mbunge wa Tumbatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wazalishaji Wadogo wa Umeme (*Small Power Producers*) ni wazalishaji wa umeme kuanzia kilowati (kW) 100 hadi Megawati (MW) 10. Kwa mujibu wa Sheria ya Umeme ya mwaka 2008, Sura Na. 131, leseni zinazotolewa kwa wazalishaji wadogo huanzia Megawati 1 hadi 10. Hivyo, wazalishaji ambao uwezo wao ni chini ya Megawati 1 hawahitaji leseni. Wazalishaji wa aina hii husajiliwa na *EWURA*. Leseni au usajili wa wazalishaji umeme wadogo ni kwa ajili ya:-

- (i) Kuuza kwa *TANESCO*;
- (ii) Kuuza moja kwa moja kwa watumiaji; na
- (iii) Kwa matumizi binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017 hadi 2018, *EWURA* ilitoa jumla ya leseni sita (6) kwa wazalishaji wadogo ambapo leseni tano (5) ni za Muda wa Maandalizi (*Provisional Licence*) za uzalishaji umeme na leseni moja (1) ya kipindi cha miaka mitano ya uzalishaji umeme kwa matumizi binafsi.

Mheshimiwa Spika, leseni hizo tano (5) za muda wa maandalizi zilitolewa kwa: Kagera *Sugar Limited* (MW 6.2); Ludewa *Capacity Building* (MW 10); Mkonge *Energy Systems Co. Ltd*-Mandera Site (MW 9); Mkonge *Energy Systems Co. Ltd*-Ngombezi Site (MW 2); na *Ninety-Two Limited* (MW 1.9). Aidha, leseni moja (1) ya muda wa miaka mitano ilitolewa kwa Kampuni ya Shanta *Mine Co. Ltd* (MW 8.2).

Na. 237

Mpango wa Kuongeza Wakulima wa Pamba

MHE. ZAYNABU M. VULU aliuliza:-

Pamba ni zao la kibiashara na linaingizia mapato Taifa letu.

Je, nini mkakati wa Serikali wa kuongeza idadi ya wakulima wa zao hilo nchini kama ilivyofanya kwenye korosho?

WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vulu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali ya kuendeleza tasnia ya pamba kwa lengo la kuongeza idadi ya wakulima, tija na uzalishaji. Mikakati hiyo ni pamoja na kuongeza uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora za pamba aina ya UKM 08, kushirikisha wazalishaji wa viuatilifu kuwekeza nchini Tanzania ili kupunguza bei ya viuatilifu, kuhakikisha uwepo wa huduma za ugani fanisi na endelevu kwa kuanzisha mfumo wa wagani kazi na kuwajengea uwezo Maafisa Ugani katika maeneo yanayolimwa pamba.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuhamasisha kilimo cha pamba ambapo msimu wa 2018/2019 zao hilo limeanza kulimwa katika Wilaya za Bahi, Chamwino na Chemba Mkoani Dodoma na kuongezeka kwa maeneo katika Mkoa wa Kigoma na Katavi. Katika msimu wa 2018/2019, Bodi ya Pamba imesambaza jumla ya tani 109.28 za mbegu bora ya pamba katika Mkoa wa Dodoma, tani 463 katika Mkoa wa Katavi na tani 73 katika Wilaya ya Uvinza Mkoani Kigoma. Aidha, Katika msimu wa kilimo wa 2019/2020 Mkoa wa Dodoma umepokea mbegu tani 96, Katavi tani 297 na Kigoma tani 83.

Mheshimiwa Spika, jitihada hizo zimeongeza uzalishaji wa pamba katika Mkoa wa Katavi kutoka tani 519 mwaka 2018/2019 hadi tani 8,583 mwaka 2019/2020 ambapo Mkoa wa Dodoma uzalishaji umeongezeka kutoka tani 43 mwaka

2018/2019 hadi tani 344 mwaka 2019/2020. Aidha, kwa Mkoa wa Kigoma uzalishaji pia umeongezeka kutoka tani 316 mwaka 2018/2019 hadi tani 2,257 mwaka 2019/2020.

Na. 238

Mradi wa Umwagiliaji wa Titye/Alambe-Kasulu

MHE. AUGUSTINE V. HOLLE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa mradi wa umwagiliaji wa Titye/Lalambe uliopo katika Wilayani ya Kasulu?

WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Augustine Vuma Holle, Mbunge wa Jimbo la Kasulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Skimu ya Titye ipo katika kijiji cha Titye, Kata ya Titye, Tarafa ya Heru katika Wilaya ya Kasulu. Aidha, skimu hiyo inapata maji ya umwagiliaji kutoka Mto Ruchugi unaotiririsha maji yake kwa mwaka mzima na inajumla ya hekta 700 zilizopimwa na kusanifiwa ambapo kati ya hekta hizo, hekta 575 zimeendelezwa kwa kilimo cha zao la mpunga.

Mheshimiwa Spika, eneo lililoendelezwa lina miundombinu yote ya msingi ya kupeleka maji mashambani kama vile banio la kuchepusha maji kutoka mtoni, mfereji mkuu, mifereji ya kati iliyojengwa kwa mawe, mifereji ya mashambani, vigawa maji na barabara za shambani kwa ajili ya kurahisisha uingizaji na utoaji wa zana za kilimo pamoja na kusafirisha mazao yaliyovunwa.

Mheshimiwa Spika, tunawapongeza wakulima wa Skimu ya Titye amba walishiriki katika kusawazisha hekta 475 ambazo zinamwagiliwa na zinalimwa zao la mpunga. Eneo lililobakia la hekta 100 ambazo usawazishaji wake

haujakamilika kwa sasa wakulima wanalima zao la mahindi. Aidha, katika msimu wa 2020/2021, Tume ya Taifa ya Umwagililaji kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu pamoja na wakulima watahakikisha kwamba eneo lilitobaki linasawazishwa ili kuwezesha uzalishaji na umwagililaji wa eneo lote lilioendelezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Skimu ya Titye ina miundombinu ya kuingiza maji mashambani lakini haina mfumo wa uondoaji maji ya ziada mashambani, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Tume imepanga kuchimba mfereji mkubwa wenye urefu wa kilomita sita (6) ili uweze kusaidia kutoa maji ya ziada yatokayo mashambani ambapo ujenzi wa mfereji mkuu utagharimu shilingi 40,000,000 na utekelezaji wake utatumia utaratibu wa "*Force Account*".

Na. 239

Vitendo vya Ukatili wa Kijinsia kwa Watoto

MHE. CATHERINE N. RUGE aliuliza:-

Kumekua na ongezeko kubwa la vitendo vya ukatili wa kijinsia hususan ulawiti na ubakaji kwa wanafunzi vinavyofanywa baina ya wanafunzi wenyewe kwa wenyewe au watu wa karibu katika familia:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa dharura kudhibiti matendo hayo?

(b) Wakati MTAKUWWA ukielekea ukingoni; je, ni kiasi gani zimetumika tangu mpango huu uanze?

(b) Je, ni kiasi gani Serikali imerasimisha utekelezaji wa MTAKUWWA katika ngazi za shule na taasisi nyingine?

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO aliijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Catherine Nyakao Ruge, Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo la ukatili wa kijinsia kwa watoto bado ni kubwa ambapo takwimu za Jeshi la Polisi zinaonyesha kuongezeka kwa vitendo vya ukatili dhidi ya watoto ambapo mwaka 2017 matukio yalikuwa 13,457, mwaka 2018 matukio 14,419 na mwaka 2019 matukio 15,680. Aidha, kwa mwaka 2019 vitendo vya ukatili vilivyoongoza ni ubakaji (6,506), mimba za wanafunzi (2,830) na ulawiti (1,405).

(a) Mheshimiwa Spika, mikakati ya Serikali katika kukabiliana na ulawiti pamoja na ubakaji ni kutoa elimu kwa jamii kuititia watu mashuhuri, viongozi wa kisiasa, dini na mila ili kushiriki katika kubadilisha tabia na mienendo ya baadhi ya watu wanaoendelea tabia za aina hiyo katika jamii kwa kuchukua hatua kali za kisheria kuwafikisha Mahakamani wale wote wanaotenda makosa hayo ili haki itendeke kwa mujibu wa sheria. Pia kuna huduma za simu bila malipo kwa watoto ambayo inawezesha jamii kutoa taarifa za vitendo vya ukatili.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha miaka mitatu (2017/18 – 2019/20) jumla ya Tsh. 41,730,266,435.00 zimetumika katika kutekeleza afua mbalimbali za mpango ikiwemo Shilingi 31,683,755,896.00 zilizotolewa mikopo kwa wanawake wajasiri amali.

(c) MTAKUWWA unatekelezwa na Wizara za kisekta zikiwemo Afya, Elimu, Sheria, Mambo ya Ndani, Ardhi, Mifugo, Ujenzi, Uvuvi na Maji. Halmashauri zote 184 zinatetekeleza mpango huu. Aidha, katika shule za msingi na sekondari afua mbalimbali zinatetekelezwa ikiwa ni pamoja na kuanzisha klabu za watoto 2,475 ili kuwasaidia watoto kujua aina za ukatili na kutoa taarifa.

NAIBU SPIKA: Katibu!

NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 – Wizara ya Nishati

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Sasa nimuite Dkt. Merdad Kalemani, Waziri wa Nishati. (*Makofii*)

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nitumie nafasi ya leo kuwasilisha katika Bunge lako tukufu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijawasilisha naomba nipate nafasi kwa dakika moja ya kuungana na Waheshimiwa Wabunge, wewe mwenyewe pamoja na Mheshimiwa Spika kutoa pole kwa Viongozi, Waheshimiwa Wabunge wenzetu waliotutoka hivi karibuni; Mheshimiwa Lwakatare, Kiongozi wa Kiroho katika Kanisa la Mlima wa Moto, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Sumve na Mheshimiwa Augustine Mahiga, Waziri wa Sheria na Katiba. Mwenyezi Mungu apumzishe roho zao mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sasa, kufuatia Taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuwajaalia afya njema Viongozi wetu Wakuu wa Kitaifa, Waheshimiwa Mawaziri wenzangu, Waheshimiwa Wabunge na Viongozi wengine mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kipekee nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na kuniwezesha kuendelea kusimama na kusimamia sekta ya Nishati na leo kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niungane na Mawaziri wenzagu, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Jemedari na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo yake thabiti yanayonisaidia kusimamia vyema sekta ya Nishati. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kuwa Rais wetu amekuwa chachu katika kutekeleza mipango mikubwa na kuleta tija katika sekta ya Nishati hapa Nchini. Mipango hiyo ni pamoja na kuanza kutekeleza mradi mkubwa wa kielelezo wa Julius Nyerere wa kuzalisha umeme wa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Rufiji, *megawatts 2115* na mradi wa Treni ya kisasa ya mwendokasi itakayotumia umeme yaani *SGR*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwaahidi Watanzania kuwa Wizara yangu kwa kushirikiana na Bunge lako Tukufu na wananchi tutaendelea kuwa *engine* ya kujenga uchumi wa viwanda na kuinua maisha ya Watanzania kutoka katika maisha yao ya chini kuelekea maisha yao ya kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuwashukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mbunge), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo mbalimbali wanayonipatia katika kusimamia sekta hii muhimu ya Nishati. Nakiri kuwa, maelekezo na miongozo yao kwa kweli sisi ni msingi wa kusimamia sekta hii. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ally Mohamed Shein, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

kwa kuendelea kusimamia kwa ufanisi utekeleza wa maendeleo katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kuwapongeza Mawaziri walioteuliwa hivi karibuni na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nampongeza Mheshimiwa George Boiniface Simbachawene, Mbunge aliyeleteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu aliyeleteuliwa kuwa Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia masuala ya Mazingira pamoja na masuala ya Mungano na hatimaye Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba kuwa Waziri wa Sheria na Katiba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukupongeza wewe mwenyewe, wenyeviti wa Bunge, wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Bunge pamoja na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge lako Tukufu katika kutekeleza kwa umahiri sana kazi zenu za Kibunge. Kwa namna ya kipekee natoa shukurani zangu za dhati kabisa kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula (Mbunge), Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri (Mbunge) na Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa ushirikiano na maelekezo wanayotupatia. Nakiri kuwa Kamati hii imefanyakazi kubwa kuishauri Wizara katika masuala mbalimbali na hasa katika kuitisha Bajeti ya Mwaka 2020/2021. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, naomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Mapato, Matumizi na Utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Nishati kwa Mwaka 2019/2020 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti iliyopitishwa kwa ajili ya Wizara ya Nishati pamoja na Taasisi zake Mwaka 2019/2020 ni jumla ya shilingi trilioni 2.142 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, Bajeti ya miradi ya maendeleo ilikuwa shilingi trilioni 2.116 sawa na asilimia 98.8 ya Bajeti yote ya Wizara na Bajeti ya Matumizi

ya kawaida shilingi bilioni 26.3 sawa na asilimia 1.2 ya Bajeti yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Nishati katika Mwaka 2019/2020 ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 421.36. Hadi kufikia tarehe 15, Mei Wizara kuititia *TPDC* pamoja na Mashirika yake, imekusanya jumla ya shilingi bilioni 375.7 makusanyo hayo ni sawa na asilimia 89.8 ya lengo. Matumizi ya gesi asilia yameongeza mapato hayo kwa takribani bilioni 32.2 na kufikia bilioni 59.2. hii ni sawa na asilimia 84.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2019/2020; maeneo ya kipaumbele ya Wizara ya Nishati kwa mwaka 2019/2020 yalikuwa ni pamoja na kuongeza uzalishaji wa umeme kwa kutekeleza miradi mikubwa ikiwemo mradi wa kuzalisha umeme wa Julius Nyerere katika Mto Rufiji, megawatts 2115, mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilimia yaani *Kinyerezi One Extension, megawatts* 185 na kuendelea na ujenzi wa kuzalisha umeme wa maji wa Rusumo katika Mto Kagera, *megawatts* 80, kuimarisha mifumo ya kusafirishe umeme nchini, kuendele ana utekelezaji wa Awamu ya tatu yaani mradi kabambe wa kusambaza umeme Vijiji (REA III), kuendelea na utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta kutoka Uganda hadi Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mingine ni ujenzi wa umeme kuunganisha Treni ya mwendokasi kutoak Dar es Salaam hadi Morogoro umbali wa kilometra 160, kuimarisha shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia hapa Nchini. Kazi nyingine ni kuhakikisha upatikanaji wa mafuta ya kutosha, kuendesha shughuli za kiuchumi kuititia Wakala wa mafuta kwa pamoja (BPS).

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kutohana na utekelezaji wa maeneo hayo ya kipaumbele, Wizara imepata mafanikio kadhaa ikiwemo makubwa yafuatayo:-

(i) Kutokuwa na mgao wa umeme katika kipindi chote cha utekelezaji wa mpango wa Bajeti Mwaka 2019/2020. Hii imetokana na uwepo wa umeme wa ziada wa *megawatts* 300 kwa siku kwa Mwaka 2019/2020 tofauti na awali tulipokuwa na upungufu wa umeme megawatts 100 hadi 170 Mwaka 2015;

(ii) Kuendelea na utekelezaji wa mradi mkubwa wa kuzalisha umeme *megawatts* 2115; (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ujenzi wa Bwawa hili kwa sasa utaifanya Tanzania kushika nafasi ya kwanza Afrika Mashariki na kuwa Bwawa la kwanza na hasa kwa Afrika na Nchi zinazoendelea na katika Mabwawa 70 Duniani sasa Tanzania inaingia katika ulingo huo. (*Makof*)

(iii) Kunganisha Mikoa ya Lindi, Mtwara, Njombe pamoja na Ruvuma katika gridi ya Taifa ambako kumeweza kusitisha mafuta katika kuzalisha umeme na Shirika la Umeme Nchini (*TANESCO*) kuokoa shilingi bilioni 15.3 kwa Mwaka;

(iv) Kuanza na kuendelea kujenga miundombinu ya umeme mkubwa kwa kuanganisha Treni katika gridi ya Taifa. Kwa Afrika Mashariki inakuwa ni Nchi ya kwanza kuanganisha umeme katika Treni kwa sasa; (*Makof*)

(v) Kuongezeka kwa kasi ya kusambaza umeme Vijiji. Hadi kufikia tarehe 30 Apili, 2020 Serikali kupitia *REA* na *TANESCO* imepeleka umeme katika Vijiji 9112 vya Tanzania ikilinganishwa na Vijiji 2018 Mwaka 2015. Hii ni sawa na ongezeko la Vijiji 7094 katika kipindi cha miaka mitano iliyopita sawa na ongezeko la asilimia 287. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Mwezi Juni, 2020 kulingana na mpango unaoendelea, Vijiji 10446 vitapata umeme na kufikia wastani wa asilimia 85.01 ya Vijiji vyote Nchini. Hatua hii tutaifanya Tanzania kuwa ya kwanza katika Afrika Mashariki na Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara kupeleka umeme katika Vijiji vyake kwa asilimia hiyo. (*Makof*)

(vi) Serikali kupitia *TANESCO* kuendelea kuunganisha umeme kwa shilingi 27,000 katika maeneo ya chini na kuondoa ghamama za kulipia nguzo, *transformer* pamoja na mita za Luku;

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine ya mafanikio ni:-

(vii) Kuunganisha gridi katika maeneo mbalimbali yakiwemo Tunduru na Nayumbu na kuokoa takribani shilingi bilioni 7.3;

(viii) Kuendelea kutumia vifaa vyta ndani katika ujenzi wa miundmbinu ya umeme na kusitisha uagizwaji wa vifaa hivyo kutoka nje ya Nchi na hivyo kuokoa shilingi bilioni 162.57 kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa nitumie nafasi hii kilitangazia Bunge lako Tukufu na Wananchi kuwa, hata vifaa vilivyobaki kuanzia tarehe 01 Julai, 2020 Serikali kupitia Wizara yetu haitaruhusu tena kuingiza vifaa kutoka nje ya nchi badala yake vitoke hapa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio ya maendeleo ni:-

(i) Kutekeleza miradi ya kujenga njia ya kusambaza umeme, kuunganisha Mikoa ya Kigoma na Katavi katika gridi ya Taifa. Mradi huu unasafirsha umeme kutoka Tabora-Urambo-Kaliua-Nguruka hadi Kidahwe Mjini Kigoma umbali wa kilometra 398 na kutoka Tabora-Ipole-Nyonga hadi Nsimbo Mkoani Katavi;

(ii) Shirika la Umeme nchini limeendelea kutohitaji ruzuku kutoka Serikalini na hivyo kuokoa shilingi bilioni 143 kwa Mwaka ambazo zilitumika kama ruzuku;

(iii) Masuala mengine yaliyofanikiwa kwa Serikali hii kupitia Wizara hii ni kuimarisha kwa mapato ya *TANESCO* kwa

kiwango cha ongezeko la shilingi bilioni 159 kwa mwezi hadi kufikia shilingi bilioni 161 kwa mwezi Mwaka huu;

(iv) Maendeleo yaliyofanyika mengine ni kuongezeka kwa watumiaji wa umeme kutoka asilimia 35 Mwaka 2015 na kufikia asilimia 85 ya Watanzania wote hivi sasa;

(v) Mafanikio mengine ni kuongeza mtandao wa kusambaza umeme na gesi asilia viwandani. Mtandao huu umewezesha kuanganisha wateja wa awali wa gesi asilia majumbani zaidi ya 2500 hadi mwezi Aprili, 2020 kutoka wateja 70 Mwaka 2015;

(vi) Mafanikio mengine ni kuongezeka kwa gesi asilia iliyogunduliwa kutoka futi za ujenzo trillioni 55.27 Mwaka 2015 na kufikia futi za ujenzo trillioni 57.54 Mwaka huu wa 2020;

(vii) Kupungua kwa uchakachuaji wa mafuta kutoka wastani wa asilimia 19.2 Mwaka 2015 na kufikia wastani wa asilimia nne tu Mwaka 2020 Mwezi Machi;

(viii) Kukamilika kwa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme *kilovolt* 220 kutoka Geita-Bulyankulu kilometa 55 yenye gharama za Dola za Marekani 23 na kufanya Mkoa wa geita na Mkoa wa Kagera kuanganishwa kwenye gridi ya Taifa.

(ix) Kuongezeka kwa ufanisi wa makusanyo na mapato kutoka serikalini ambapo *TPDC* imekusanya shilingi bilioni 484.33 sawa na asilimia 123 ya lengo la makusanyo;

(x) Kuendelea kutekeleza kazi za awali za mradi wa bomba la kusafirisha mafuta kutoka Hoima hadi Chongoleani Mjini Tanga. Kazi hizo zinakamilika Mwezi Juni Mwaka 2019. Kazi zingine za maandalizi zinaendelea. Gharama ya mradi ni Dola za Marekani bilioni 3.5;

(xi) Kuongeza matumizi ya gesi asilia kufikia futi za ujazo milioni 210 kwa siku kwa Mwaka 2019/2020 kutoka futi za ujazo milioni 95 kwa Mwaka, Mwaka 2015;

(xii) Kupungua kwa muda wa kususha mafuta katika Bandari zetu za Dar es salaam, Tanga na Mtwara kutoka siku 30 hadi 40 kwa Mwaka 2015 ilivyokuwa na kufikia siku tatu hadi sita tu; (*Makofi*)

(xiii) Kuongezeka kwa mafuta ya ziada ya wastani wa lita milioni 235. Haya ni mafuta ya *Diesel*, mafuta ya *Petrol* lita milioni 116, mafuta ya Ndege milioni sita na mafuta ya taa 650,000 na hivyo kufanya kuongezeka kwa mafuta kwa asilimia 42.

Mheshimiwa Naibu Spika, katia Mwaka 2019/2020 na Mwaka 2020/2021 Wizara ya Nishati itaendelea kutekeleza maeneo ya vipaumbele yakiwemo kuongeza uzalishaji wa umeme Nchini lili kufikia lengo la kuwa na umeme wa megawatts 10,000 kufika Mwaka 2025. Lengo hili litafikiwa kwa kutekelza miradi mikubwa kabambe ikiwemo kama nilivyo sema mradi wa Julius Nyerere wa megawatts 2115 na miradi mingine niliyoitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2020/2021, Serikali itaendelea kuimarisha mifumo ya usafirishaji wa umeme Nchini kwa kutekeleza miradi mbalimbali ikiwa ni pamoja na mradi wa Geita-Bulyankulu *kilovolt* 220, kilometa 55 pamoja na miradi ya *North West grid*, *kilovolt* 400 yenye urefu wa kilometa 1,384 inayojumuisha umeme kutoka Iringa, Mbeya, Sumbawanga, Mpanda, Kigoma hadi Nyakanazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Singida-Arusha-Namanga *kilovolt* 400, kilometa 414, mradi wa Rufiji-Chalinze-Dodoma, *kilovolt* 400, kilometa 512, mradi wa Rusumo-Nyakanazi, *kilovolt* 220, kilometa 98, Geita-Nyakanazi, *kilovolt* 220, kilometa 144, Tabora-Urambo-Kaliua-Nguruka hadi Kidawe-Kigoma, *kilovolt* 132, kilometa 391 na Tabora-Ipole-Nyonga hadi Nsimbo-Katavi, kilometa 385. Miradi mingine ni Badakuli-Sinyanga hadi Imariro-Simiyu, kilometa 160 na Kiteto hadi Kilindi-Tanga, *kilovolt* 33, kilometa 108. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya umeme Nchini; hali ya umeme Nchini imeendelea kuimarika. Katika Mwaka 2019/

2020 uwezo wa mitambo ya kuzalisha umme yaani *Installed capacity*imeongezeka na kufikia *megawatts* 1602.42 kutoka *megawatts* 1517.47 zilizofikiwa Mwaka 2017/2018. Hii nisawa na ongezeko la asilimia 5.6. kati ya jumla megawatts 1602.42 zilizopo nchini katika gridi ya Taifa zipo megawatts 1565.72 ikilinganishwa na ilivyokuwa hapo nyuma. Hii ni sawa imeongeza kwenye gridi ya Taifa *megawatts* nyingine 36.18 nje ya gridi.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme uliozalishwa Nchini uliongezekwa kutoka *Giga watts hour* 7114 Mwaka wa Fedha 2018/2019 na kufikia *Giga watts hour* 7644 Mwaka wa Fedha 2019/2020, hii ni sawa na ongezeko la asilimia 4.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Mwaka 2015, Nchi yetu ilikuwa ana uwezo wa kuzalisha umeme wa *megawatts* 1204 tu ikilinganishwa na uwezo wa sasa wa *megawatts* 1602.42 sawa na ongezeko la asilimia 34. Katika kutimiza azma ya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa viwanda, Serikali kupitia Wizara ya Nishati imelenga kuzalisha umeme *megawatts* 10000 ifikapo Mwaka 2020/2025. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa *kilovolt* 400; mradi huu utajenga umeme kwa *kilovolt* 400 yenyeye urefu wakutoka Singida hadi Namanga kupitia Arusha na kuunganisha Vijiji 22 vilivyopitiwa na mradi hu. Gharama ya mradi huu ni Dola za Marekani milioni 258.82 sawa na takribani shilingi bilioni 5,000,000,952.54

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kupeleka umeme katika Jiji la Kisasa la Dodoma; mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa *kilovolt* 220 kutoka Zuzu hadi Msalato na kutoka Zuzu hadi Kikombo pamoja na ujenzi wa vituo viwili vya kupooza umeme katika maeneo ya Msalato na Kikombo Mkoani Dodoma. Gharama ya mradi huu ni Dola za Marekani milioni 166.7 sawa na takribani bilioni 388.46.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zilizofanyika kwa mwaka 2020/2021 ni pamoja na kuendelea na taratibu wa kupata

ufadhili wa mradi kutoka Serikali ya Japan kupitia Shirika lake la Maendeleo ya Kimataifa JICA. Mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Juni mwaka huu 2020 na kukamilika mwaka 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatarajia kuanza ujenzi wa miundombinu ya umeme kwa kufanya Mji wa Dodoma kuwa wa kisasa na wa Kimataifa. Serikali kupitia TANESCO unadhamiria kusambaza umeme katika mji huo kwa kutumia nyaya za chini ya *underground cables* na gharama ya mradi inakadiriwa kuwa dola au Shilingi za Tanzania bilioni 16.9.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mradi wa kuchakata gasi LNG, kazi zilizotekelzeza kwa mwaka 2019/2020 ni kufanya mapitio ya mikataba (PSA) kukamilisha mpango wa uhamasishaji wa wananchi na wananchi 693 watakaopisha mradi na kukamilisha malipo ya fidia. Jumla ya shilingi bilioni 5.2 zimetengwa na zimeanza kutumika kulipa fidia kwa wananchi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi Uganda hadi Tanzania utapita katika mikoa minane ya Tanzania Bara. Mikoa hiyo ni Kagera, Geita, Tabora, Shinyanga, Manyara, Singida, Dodoma na hatimaye Tanga. Katika mwaka huu wa fedha, shilingi bilioni saba zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo na mradi utakamilika mwaka 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya upatikanaji wa mafuta nchini. Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara zimeendelea kupokea mafuta yanayoagizwa kwa kutumia mfumo huu kwa kuagiza mafuta kwa pamoja kwa kipindi kuanzia Januari, 2019 hadi Desemba, 2019. Jumla ya lita bilioni 6.15 za mafuta ziliagizwa sawa na ongezeko la asilimia 7.4 ikilinganishwa na lita bilioni 5.70 za mafuta zilizoagizwa mwaka 2018. Kati ya lita hizo, bilioni 3.54 sawa na asilimia 57.5 ya mafuta yote yaliyoagizwa yalikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya ndani na lita bilioni 2.62 sawa na asilimia 42.5 ya mafuta yote ni kwa ajili ya mafuta ya nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mafuta ya ziada yameongezeka kutoka lita milioni 185 mwaka 2018 na kufikia wastani wa lita milioni 365 kwa mwaka 2019/2020. Mafuta yanatosheleza kwa zaidi ya siku 40.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushirikiano wa Kikanda na wa Kimataifa, katika kipindi cha mwaka 2020/2021 Serikali kupitia Wizara ya Nishati itendelea kushirikiana kwa karibu na Washirika wa Maendeleo na wadau wengine watakaojitokeza ili kuhakikisha kuwa inakuwa *engine* katika kujenga uchumi wa viwanda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia fursa hii kumshukuru Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalo kwa kunisaidia kwa kiasi kikubwa na kwa dhati kabisa katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, napenda kumshukuru Katibu Mkuu - Mhandisi Zena Said kwa uchapakazi wake mahiri na anatusaidia vizuri katika kufanya kazi za Wizara pamoja na utendaji wake. Vile vile nawashukuru Makamishna, Wakuu wa Idara na Vitengo, Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi chini ya Wizara yetu pamoja na Watanzania wote walio tupu ushirikiano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee napenda nachukuwa nafasi hii sasa kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu zuri la Chato kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo katika Jimbo letu. Nawaahidi wazazi wangu kuwa sitawaangusha na nitaendelea kushirikiana nanyi katika kubuni mikakati mbalimbali ya kuendeleza Jimbo letu zuri la Chato.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana familia yangu ikiongozwa na mke wangu kipenzi mama Kalemani pamoja na wototo wangu wapendwa kwa kuendelea kuniombea na kuniunga mkono katika kutekeleza majukumu yangu ya Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Bajeti ya Mwaka 2020/2021 imelenga kutekeleza dhamira ya Serikali ya

kuhakikisha kuwa inazalisha umeme wa kutosha wa uhakika unaotabirika na wenyе gharama nafuu ambapo Sekta ya Nishati itabaki kuwa *engine* katika kujenga uchumi wa viwanja. Bajeti imelenga kuimarisha shughuli za utafutaji na biashara ya mafuta na gesi asilia ili kuwezesha kunufaika na rasilimali tulizonazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukuru sasa liidhinishe bajeti ya jumla ya shilingi 2,196,837,774,000/= kwa ajili ya matumizi ya Wizara na Taasisi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena kutoa shukrani kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika sasa naomba kutoa hoja.

**HOTUBA YA WAZIRI WA NISHATI MHE. DKT. MEDARD
MATOGOLO CHANANJA KALEMANI (MB.),
AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA
MATUMIZI YA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA
2020/21 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

A. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, kutohana na Taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2019/20 na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake kwa Mwaka 2020/21.

2. Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na uzima na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu leo kutoa taarifa ya utekelezaji wa Serikali kuitia Sekta ya Nishati. Namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi

wa rehemaa kwa kuendelea kuwajalia afya njema Viongozi wetu Wakuu wa Kitaifa, Waheshimiwa Mawaziri wenzangu, Waheshimiwa Wabunge na Viongozi wengine mbalimbali.

3. Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo yake thabiti yanayoniwezesha kusimamia vema Sekta ya Nishati. Ni dhahiri kuwa Rais wetu amekuwa chachu katika kutekeleza mipango mikubwa na yenye tija katika Sekta ya Nishati hapa nchini.

4. Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru Mhe. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo mbalimbali wanayonipatia katika kusimamia Sekta ya Nishati. Nikiri kuwa maelekezo na miongozo ya viongozi wetu hawa ni msingi wa mafanikio ya utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Nishati. Aidha, napenda kumpongeza Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kusimamia kwa umahiri utekelezaji wa shughuli za maendeleo katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

5. Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza Mawaziri walioteuliwa hivi karibuni na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nampongeza Mhe. George Boniface Simbachawene (Mb.), aliyyeteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb.), aliyyeteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Muungano na Mazingira na Mhe. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu (Mb.), aliyyeteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria.

Nawatachia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yao.

6. Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge, Wenyeviti wote wa Kamati Mbalimbali za Kudumu za Bunge pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge lako Tukufu kwa utendaji kazi wenu mahiri. Napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Mhe. Dunstan Luka Kitandula (Mb.), Makamu Mwenyekiti Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri (Mb.), na Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa ushauri na maelekezo wanayotupatia katika kuboresha utendaji kazi wa Wizara.

7. Mheshimiwa Spika, tarehe 15 Januari, 2020, Bunge lako Tukufu lilimpoteza Mhe. Rashid Ajali Akibar, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini, tarehe 20 Aprili, 2020 Bunge lako lilimpoteza Mhe. Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (CCM), tarehe 29 Aprili, 2020 Bunge lako pia lilimpoteza Mhe. Richard Mganga Ndassa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Sumve na tarehe 01 Mei, 2020 Bunge lilimpoteza Mhe. Augustine Phillip Mahiga aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria na pia Mbunge. Naungana na wabunge wenzangu kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu, familia za marehemu, ndugu, jamaa, marafiki na wote walioguswa na misiba hiyo. Tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

8. Mheshimiwa Spika, namshukuru Mhe. Subira Khamis Mgusu, (Mb.), Naibu Waziri wa Nishati kwa kunisiaidia kwa karibu katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, napenda kumshukuru Katibu Mkuu Mha. Zena Ahmed Said na Naibu Katibu Mkuu Mha. Leonard Robert Masanja kwa uchapakazi wao mahiri na ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza shughuli zangu za kila siku za Wizara. Namshukuru pia aliyekuwa

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Dkt. Hamisi Hassan Mwinyimvua kwa utumishi wake uliotukuka. Vilevile, nawashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo, Wenyevit na Wajumbe wa Bodi, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote kwa ujumla kwa ushirikiano wao na juhudzi zao wanazofanya kwa ajili ya kufanikisha malengo ya Wizara.

9. *Mheshimiwa Spika*, napenda nichukue fursa hii kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Chato kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo ya Jimbo. Wazazi wangu na wananchi wote wa Jimbo la Chato naomba mtembee kifua mbele, kijana wenu niko imara katika kuwawakilisha, na ninaahidi kuwa sitawaangusha na nitaendelea kushirikiana nanyi katika kuleta maendeleo ya Jimbo letu na Taifa kwa ujumla. Naishukuru sana familia yangu ikiongozwa na Mke wangu Mama Kalemani pamoja na watoto wangu kwa kuendelea kuniombea na kuniunga mkono katika kutekeleza majukumu ya kitaifa.

10. *Mheshimiwa Spika*, baada ya utangulizi huo, naomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Mapato, Matumizi na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara ya Nishati kwa Mwaka 2019/20 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2020/21.

B. TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA 2019/20 NA MWAKA 2020/21

Bajeti na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2019/20

11. *Mheshimiwa Spika*, Bajeti iliyopitishwa kwa ajili ya Wizara ya Nishati pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka 2019/20 ni jumla ya **Shilingi trilioni 2.143** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Katika ya fedha hizo, Bajeti ya Miradi ya Maendeleo ilikuwa **Shilingi trilioni 2.116** sawa na **asilimia 98.8** ya bajeti yote ya Wizara na Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ilikuwa

Shilingi bilioni 26.339 sawa na **asilimia 1.2** ya bajeti yote ya Wizara.

12. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi bilioni 611.149**. Kiasi hicho kilichopokelewa na Wizara kinaendana na Mpango Kazi uliopo. Aidha, Serikali inaendelea kutoa fedha kulingana na Mpango Kazi na mahitaji yaliyopo.

Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali

13. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati katika mwaka 2019/20 ilipangiwa kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 602.06**. Kati ya makusanyo hayo, jumla ya **Shilingi bilioni 602.05** zilitarajiwala kukusanya kupitia shughuli za mafuta na gesi asilia na **Shilingi milioni 12.0** kupitia shughuli za utawala. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020, Wizara kupitia shughuli za utafiti wa mafuta na mauzo ya gesi asilia pamoja na utawala imekusanya **Shilingi bilioni 501.06** Makusanyo hayo ni sawa na **asilimia 83.23** ya lengo.

C. MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2015/16 HADII 2020

14. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitano cha Serikali ya Awamu ya Tano, utekelezaji wa mipango ya maendeleo katika sekta ya nishati umepata mafanikio makubwa mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme nchini ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2020 uwezo wa mitambo ya kufua umeme nchini umeongezeka na kufikia jumla ya MW 1,601.84 kutoka MW 1,308 mwaka 2015;

(ii) Kukamilika kwa Miradi ya Kuzalisha Umeme ya Kinyerezi I MW 150 na Kinyerezi II MW 240. Ujenzi wa miradi ulikamilika kwa asilimia 100 mwaka 2016 na

mwaka 2018 mtawalia, ambapo jumla ya MW 398.22 zimeingizwa kwenye Gridi ya Taifa;

(iii) Kuendelea na Ujenzi wa Mradi wa Julius Nyerere Hydro Power Project (JNHPP) MW 2,115 ambao hadi sasa utekelezaji wake umefikia zaidi ya asilimia 85 kulingana na Mpango Kazi wa kazi zilizopangwa;

(iv) Kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Rusumo MW 80 ambao hadi sasa utekelezaji wake umefikia asilimia 61;

(v) Kuunganisha Mikoa ya Lindi, Mtwara, Njombe na Ruvuma katika Gridi ya Taifa ambako kumewezesha kusitisha uzalishaji wa umeme kwa kutumia mitambo ya mafuta mazito ambayo ilikuwa inaigharimu TANESCO wastani wa Shillingi billioni 15.3 kwa mwaka;

(vi) Kukamilika kwa Mradi wa njia ya kusafirisha umeme kV 220 kutoka Makambako hadi Songea ambao ulikamilika mwezi Septemba, 2018 na kuwezesha vijiji vyote 122 kuunganishiwa umeme;

(vii) Kuendelea na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa KV 220 kwa ajili ya Mradi wa Treni ya Mwendo Kasi (SGR) awamu ya kwanza (Lot I) yenyeye urefu wa kilomita 160 kutoka Dar es Salaam hadi Kingolwira, Morogoro;

(viii) Kuendelea na Utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijiji ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2020 jumla ya vijiji 9,112 vimeunganishiwa umeme ikilinganishwa na vijiji 2,018 vilivyokuwa vimeunganishwa umeme mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia 351.54;

(ix) Kuendelea kutokuwa na mgawo wa umeme nchini na kuwa na ziada ya umeme wa wastani wa MW 325 kwa siku;

- (x) Kuendelea na uzalishaji wa vifaa vyatia kujenga miradi ya umeme nchini na hivyo kusitisha uingizaji wa vifaa vyatia ujenzi wa miundombinu ya umeme ikiwemo nguzo, mashineumba, nyaya na mita za LUKU ndani ya nchi na hivyo kurahisisha upatikanaji wa vifaa hivyo. Uzalishaji huo pia umechangia ongezeko la ajira nchini;
- (xi) Kuunganishiwa umeme kwa wateja wapya 1,293,528 na kufanya jumla ya wateja waliounganishiwa umeme hadi mwezi Aprili, 2020 kufikia 2,766,745 ikilinganishwa na wateja 1,473,217 waliokuwepo hadi Juni, 2015 sawa na ongezeko la asilimia 88;
- (xii) Kuongezeka kwa kiwango cha upatikanaji wa umeme (*Overall Electricity Access rate*) nchini kutoka asilimia 67.8 mwaka 2016 na kufikia asilimia 84.6 mwaka 2020;
- (xiii) Serikali kupitia TANESCO na REA kuendelea kuunganisha umeme kwa Shilingi 27,000 katika maeneo yote ya vijijini kulingana na Mpango wa Kupeleka Umeme Vijijini;
- (xiv) Kuongezeka kwa gesi asilia iliyogunduliwa kutoka Futi za Ujazo Trillioni 55.27 mwaka 2015 na kufikia Futi za Ujazo Trillioni 57.54 mwaka 2020 sawa na ongezeko la futi za ujazo Trillioni 2.27;
- (xv) Kuimarika kwa shughuli za kaguzi za gharama katika Mikataba ya PSAs (*PSA Audit*) na hivyo kupelekeea kuokoa fedha Shilingi billioni 10.14 kwa kaguzi zilizofanyika kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2016 hadi 2018;
- (xvi) Kuanza kwa shughuli za utafutaji wa mafuta katika Kitalu cha Eyasi Wembere ambapo visima vifupi viwili (2) vyenye kina cha urefu wa mita 300 vimechorongwa

katika Wilaya ya Igunga Mkoa wa Tabora na Meatu Mkoani Shinyanga;

(xvii) Kuongezeka kwa kasi ya usambazaji wa gesi asilia ambapo katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Mtwara, jumla ya nyumba za wateja wa awali zaidi ya 1,000 zimefikishiwa miundombinu ya usambazaji gesi asilia na viwanda 48 vimeunganishwa kufikia mwezi Aprili, 2020. Aidha, zaidi ya magari 400 yamefungwa mifumo ya matumizi ya gesi asilia ikilinganishwa na magari 60 yaliyokuwa yameunganishwa mwaka 2015;

(xviii) Kuongezeka kwa uzalishaji wa gesi asilia kutoka wastani wa futi za ujazo bilioni 37 kwa mwaka 2015 hadi futi za ujazo bilioni 46 katika mwaka 2019 sawa na ongezeko la asilimia 24;

(xix) Kuongezeka kwa mchango wa gesi asilia katika kuzalisha umeme nchini kutoka asilimia 36 mwaka 2015 hadi asilimia 57 mwezi Aprili, 2020;

(xx) Kuongezeka kwa ushiriki wa Watanzania katika miradi ya mafuta na gesi asilia ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2020 kampuni 457 zimeorodheshwa katika kanzidata iliyowezesha kampuni hizo kushiriki katika miradi mbalimbali;

(xxi) Kuhuishwa kwa Bandari za Tanga na Mtwara katika kupokea Mafuta ambapo Bandari hizo zimeanza kupokea Mafuta kuanzia mwezi Julai, 2015 na Julai, 2018 mtawalia;

(xxii) Kuendelea kuimarika kwa Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (*Bulk Procurement System – BPS*) ambao umeongeza uhakika wa upatikanaji wa mafuta nchini na kupunguza ghamama za uagizaji;

(xxiii) Kujenga uwezo katika kusimamia Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia kwa kudhamini mafunzo ya ufundi stadi

kupitia vyuo vya ufundi stadi (VETA). Serikali imeendelea kutoa kozi mbalimbali zinazohusiana na mafuta na gesi katika vyuo vikuu hapa nchini kwa viwango vya Stashahada (*Diploma*), Shahada (*Bachelor*) na Uzamili (*Masters*);

(xxiv) Kupungua kwa uchafuzi (uchakachuaji) wa mafuta kutoka wastani wa asilimia 19.2 mwaka 2015 hadi kufikia wastani wa asilimia 4 mwezi Machi, 2020.

D. VIPAUMBELE VYA BAJETI KWA MWAKA 2019/20

15. Mheshimiwa Spika, maeneo ya kipaumbele ya Wizara ya Nishati kwa mwaka 2019/20 yalikuwa ni pamoja na: kuongeza uzalishaji wa umeme kwa kutekeleza miradi mikubwa ikiwemo Julius Nyerere (MW 2,115), Rusumo (MW 80), Kinyerezil –Extension (MW 185), Malagarasi (MW 45), Kakono (MW 87); na Mtwara (MW 300); ujenzi wa njia za kusafirisha umeme ikiwemo Singida – Arusha – Namanga KV 400, North – West Grid Extension (Mbeya – Sumbawanga – Mpanda – Kigoma – Nyakanazi) KV 400, Rufiji – Chalinze – Dodoma KV 400, Kinyerezi – Dodoma KV 400, Geita – Nyakanazi KV 220, Rusumo - Nyakanazi KV 220 na Bulyanhulu – Geita KV 220; kuendelea na utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya Mradi Kabambe wa Kupeleka Umeme Vijiji; kuimarisha shughuli za utafiti wa mafuta na gesi asilia na kuhakikisha upatikanaji wa mafuta ya kutosha kupitia utaratibu wa kuagiza mafuta kwa pamoja ili kuendesha shughuli za maendeleo.

16. Mheshimiwa Spika, Wizara pia ilizingatia maeneo mengine ambayo ni pamoja na: kuendelea kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara na Taasisi zake katika kusimamia Sekta ya Nishati; kuboresha mazingira ya ofisi kwa watumishi wa Wizara na Taasisi zake ili kutoa huduma bora zaidi; na kuendelea kuelimisha umma na kuboresha mawasiliano na wadau mbalimbali kuhusu masuala ya nishati.

E. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA WIZARA KWA MWAKA 2019/20 NA MPANGO WA BAJETI KWA MWAKA 2020/21

17. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2020/21, Wizara ya Nishati itaendelea kutekeleza maeneo ya vipaumbele mbalimbali yakiwemo: kuongeza uzalishaji wa umeme nchini kwa kutekeleza mradi mkubwa wa Julius Nyerere (**MW 2,115**) na miradi mingine ya Kinyerezi I - *Extension (MW 185)*, Rusumo **MW 80**, Ruhudji (**MW 358**), Rumakali (**MW 222**) na Malagarasi (**MW 45**). Aidha, Wizara imeendelea na taratibu za kushirikisha wawekezaji binafsi katika utekelezaji wa miradi ya umeme wa Jua MW 150, umeme wa Upepo MW 200 na Makaa ya Mawe MW 600 kwa njia ya ushindani. Miradi hiyo inatarajiwa kuanza kutekelezwa mwaka 2020/21.

18. Mheshimiwa Spika, pamoja na miradi hiyo ya uzalishaji wa umeme, Serikali pia itaendelea kutekeleza miradi ya kuimarisha mifumo ya usafirishaji wa umeme nchini kwa kutekeleza miradi mbalimbali. Miradi hiyo ni pamoja na: *North - West Grid Extension KV 400*, Singida – Arusha – Namanga **KV 400**, Rufiji - Chalinze – Dodoma **KV 400**, Rusumo – Nyakanazi **KV 220**, Geita – Nyakanazi **KV 220**, Geita – Bulyanhulu **KV 220**, Urambo – Kigoma **KV 132**, Ipole – Katavi **KV 132**, Ibadakuli – Imalilo **132 KV** na Kiteto – Kilindi **132 KV**.

19. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2020/21 maeneo mengine ya kisekta yatakayozingatiwa na Wizara ni: kuendelea na utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya Mradi Kabambe wa Kupeleka Umeme Vijijini; kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani Tanga nchini Tanzania (*East African Crude Oil Pipeline - EACOP*); kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Kusindika Gesi Asilia (LNG); kuimarisha shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia; kuongeza kasi ya usambazaji wa gesi asilia; kuvutia uwekezaji katika sekta ya nishati; na kuendelea kuimarisha utendaji

wa Taasisi chini ya Wizara; TANESCO, TGDC, REA, TPDC, PURA na PBPA ili kuongeza ufanisi katika Sekta ya Nishati. Aidha, Serikali itaendelea kuhakikisha uwepo wa mafuta ya kutosha kuendesha shughuli za kiuchumi kupitia Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja.

20. Mheshimiwa Spika, pamoja na maeneo hayo ya kisekta, Wizara pia itazingatia maeneo mengine yanayolenga kuleta tija katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na: kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara na Taasisi zake katika kusimamia Sekta; kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi ili kutoa huduma bora; na kuendelea kuelimisha umma kuhusu masuala ya nishati.

SEKTA NDOGO YA UMEME UWEZO WA MITAMBO YA KUZALISHA UMEME

21. Mheshimiwa Spika, uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme iliyounganishwa katika Gridi ya Taifa ni **MW 1,565.72** ambapo **MW 573.70** zinatokana na nguvu ya maji, **MW 892.72** gesi asilia, **MW 88.80** mafuta mazito na dizeli na **MW 10.50** mabaki ya mimea na mazao (*Biomass*). Uwezo wa mitambo hiyo unajumuisha mitambo inayomilikiwa na Serikali kupitia TANESCO ambayo huchangia **asilimia 86.50** na mitambo ya Wazalishaji Binafsi (*IPPs/SPPs*) ambayo huchangia **asilimia 13.50**. Aidha, TANESCO inamiliki mitambo ambayo haijaunganishwa katika Gridi ya Taifa yenye uwezo wa kufua **MW 36.12** na hivyo kufanya jumla ya uwezo wa mitambo ya kufua umeme nchini kufikia **MW 1,601.84**.

22. Mheshimiwa Spika, mahitaji ya juu ya umeme katika Gridi ya Taifa yameendelea kuongezeka kutokana na kuongezeka kwa shughuli za uchumi nchini. Tarehe 27 Februari, 2020 mahitaji ya juu ya umeme yalifikia **MW 1,151.66** ikilinganishwa na **MW 1,116.58** zilizofikiwa mwaka 2019. Ongezeko hili ni sawa

na **asilimia 3.14**. Aidha, umeme uliozalishwa nchini uliongezeka kutoka **GWh 7,374** mwaka 2018 na kufikia **GWh 7,692** mwaka 2019 sawa na ongezeko la **asilimia 4.3**.

MIRADI YA KUZALISHA UMEME

Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere Hydro Power Project (JNPPP) – MW 2,115

23. Mheshimiwa Spika, mradi huu unahu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa **MW 2,115** kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Rufiji. Mkandarasi ambaye ni Kampuni ya *Arab Contractors* yenye ubia na *Elsewedy Electric*, zote za nchini Misri tarehe 15 Juni, 2019 alianza rasmi utekelezaji wa mradi. Katika mwaka 2019/20 kazi zillizotekelizwa ni pamoja na: kuanza ujenzi wa bwawa (*main dam*); na kuanza ujenzi wa njia ya kuchepusha maji (*diversion tunnel*). Kwa ujumla utekelezaji wa mradi huu unaendelea vizuri kulingana na Mpango Kazi wake na unatarajiwa kukamilika ifikapo Juni, 2022.

24. Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zinazoendelea ni pamoja na ujenzi wa mgodi wa kuzalisha umeme, njia za kupeleka maji kwenye mitambo, manunuzi ya vifaa mbalimbali vya mradi ambapo shughuli hizo zote zinawiana na Mpango Kazi wake. Gharama za mradi huu ni **Shilingi triliioni 6.55** zinazotokana na fedha za ndani. Mradi huu unamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2020 Mkandarasi amelipwa **Shilingi triliioni 1.219** sawa na **asilimia 100** ya fedha alizotakiwa kulipwa kwa mujibu wa mkataba.

25. Mheshimiwa Spika, jumla ya wafanyakazi wapatao **3,897** wameajiriwa tangu utekelezaji wa mradi uanze ambapo kati ya wafanyakazi hao watanzania ni **3,422** sawa na **asilimia 87.81** na wafanyakazi kutoka nje ya nchi ni **475** sawa na

asilimia 12.19 ya wafanyakazi wote wa mradi. Hadi kukamilika kwa Mradi Watanzania 6,000 wataajiriwa katika shughuli za Mradi.

26. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2020/21, Serikali itaendelea na utekelezaji wa mradi ambapo kazi zitakazofanyika ni pamoja na kuendelea na: ujenzi wa bwawa (*main dam and spillways*); ujenzi wa njia kuu za kuitisha maji (*tunnels*); ujenzi wa eneo la kufunga mitambo ya kufua umeme (*power house*); na ujenzi wa kituo cha kusafirisha umeme (*switch yard*). Jumla ya fedha za ndani **Shilingi triliioni 1.44** zimetengwa katika mwaka 2020/21 kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo.

Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Rusumo – MW 80

27. Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa **MW 80** kwa kutumia maji ya Mto Kagera na unahusisha nchi tatu (3) za Tanzania, Burundi na Rwanda kwa mgawanyo sawa kwa kila nchi. Mradi unagharimu **Dola za Marekani milioni 113** sawa na takriban **Shilingi bilioni 263.87** kwa ufadhili wa Benki ya Dunia kwa upande wa Tanzania. Hadi sasa, uchimbaji wa eneo la kujenga mitambo (*power house*) umekamilika na ufungaji wa mitambo umefikia **asilimia 52**; kukamilika kwa milango ya kuingiza na kuchepusha maji (*spillway and intake gates*); kukamilika kwa ujenzi wa nyumba za wafanyakazi; na kuendelea na uchimbaji wa handaki la kuitishia maji ambao umefikia **asilimia 56**. Utekelezaji wa mradi kwa ujumla umefikia **asilimia 61**.

28. Mheshimiwa Spika, kazi zilizopangwa kufanyika mwaka 2020/21 ni: kuendelea na ufungaji wa mitambo pamoja na ujenzi wa mfumo wa kuitisha maji (*tunnelling system*); ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme; ujenzi wa kituo cha kusafirisha umeme (*switch yard*); na kukamilisha miradi ya kijamii kwa wananchi

wanaozunguka eneo la mradi (*Local Area Development Plan – LADP* na *Livelihood Restoration Program – LRP*). Jumla ya **Shilingi milioni 13.846** zimetengwa katika mwaka 2020/21 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi. Mradi huu uliana mwezi Februari, 2017 na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Februari, 2021.

Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Ruhudji – MW 358

29. Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa **MW 358** kwa kutumia ya maji ya Mto Ruhudji na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa **kV 400** yenye urefu wa kilomita 170 kutoka Ruhudji hadi katika eneo la Kisada, Iringa kitakapojengwa kituo cha kupoza umeme. Ujenzi wa mitambo ya kuzalisha umeme unakadirwa kugharimu **Dola za Marekani milioni 407.4** sawa na takriban **Shilingi bilioni 951.34** na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme unakadirwa kugharimu **Dola za Marekani milioni 53.2** sawa na takriban **Shilingi bilioni 124.23**. Kazi zilizofanyika mwaka 2019/20 ni pamoja na: uhuishaji wa Upembizi Yakinifu (*Updating of feasibility study*); usanifu wa awali wa mradi pamoja na uandaaji wa makabrasha ya zabuni ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa mradi.

30. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/21 kazi zitakazofanyika ni pamoja na: kukamilisha uhuishaji wa Upembizi Yakinifu (*Updating of feasibility study*); usanifu wa awali wa Mradi (*Conceptual Design*); na kumpata Mkandarasi wa kujenga mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 255.583** zimetengwa katika mwaka 2020/21 ili kutekeleza kazi hizo. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2021 na kukamilika mwezi Juni, 2024.

Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Kakono – MW 87

31. Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa **MW 87** kwa kutumia

maji ya Mto Kagera na njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa **kV 220** kutoka Kakono hadi Kyaka yenyе urefu wa kilomita 38.5. Katika mwaka 2019/20 kazi zilizokamilika ni pamoja na usanifu wa mradi na uandaaji wa makabrasha ya zabuni. Ujenzi wa mradi huu utagharimu **Dola za Marekani milioni 287.60** sawa na takriban **Shilingi bilioni 671.575**.

32. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2020/21 kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na: kulipa fidia wananchi watakaopisha mradi; na kukamilisha Tathmini ya Athari kwa Mazingira. Serikali kuititia TANESCO imetenga **Shilingi bilioni 1.56** kwa ajili ya kulipa fidia. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Desemba, 2021 na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2024.

Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Rumakali – MW 222

33. Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa **MW 222** kwa kutumia maji ya Mto Rumakali katika Mkoa wa Njombe na njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 220** yenyе urefu wa kilomita 150 kutoka Rumakali hadi kituo cha kupoza umeme cha Iganjo Mkoani Mbeya. Gharama za mradi huu zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 388.22** sawa na takriban **Shilingi bilioni 906.53**. Kwa mwaka 2019/20 kazi zilizotekeliza ni pamoja na: uhuishaji wa Upembusi Yakinifu (*Updating of feasibility study*); usanifu wa awali wa mradi; na kuandaa makabrasha ya zabuni ya ujenzi wa mradi.

34. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/21 kazi zitakazofanyika ni: kukamilisha kuhuishwa Upembusi Yakinifu na kuanza maandalizi ya ujenzi wa mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 23.033** zimetengwa katika mwaka 2020/21 ili kutekeleza kazi hizo. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2021 na kukamilika mwezi Juni, 2024.

Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Malagarasi- MW 45

35. Mheshimiwa Spika, mradi huu unahuusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa **MW 45** kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Malagarasi katika Mkoa wa Kigoma. Aidha, mradi utahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa **kV 132** yenye urefu wa kilomita 55 kutoka Malagarasi hadi Kidahwe Mkoani Kigoma. Gharama za utekelezaji wa Mradi ni **Dola za Marekani milioni 138.1** sawa na takriban **Shilingi bilioni 322.48.**

36. Mheshimiwa Spika, kazi zilizofanyika ni pamoja na: kukamilisha uhuishaji wa Upembuzi Yakinifu wa kituo cha kuzalisha umeme pamoja na uthamini katika kilomita 33 toka kijiji cha Mazungwe hadi Kidahwe.

37. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21 kazi zitakazofanyika ni pamoja na kukamilisha taratibu za kupata fedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na kuanza ujenzi wa mradi. Mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Septemba, 2020 na kukamilika mwezi Septemba, 2023. Kiasi cha **Shilingi milioni 100** kimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Kikonge – MW 300

38. Mheshimiwa Spika, mradi huu unahuusu ujenzi wa Mtambo wa kuzalisha umeme wa **MW 300** kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Ruhuhu katika Mkoa wa Njombe na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 220** yenye urefu wa kilomita 53 kutoka Kikonge hadi kituo cha kupoza umeme cha Madaba. Gharama za utekelezaji wa Mradi zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 750** sawa na takriban **Shilingi trilioni 1.75.**

39. Mheshimiwa Spika, kazi zilizotekelizwa katika kipindi cha mwaka 2019/20 ni pamoja na: kukamilika

kwa Tathmini ya Mazingira ya Kimkakati (*Strategic Environmental & Social Assessment – SESA*); na kuendelea na Upembuzi Yakinifu (*Feasibility Study*).

40. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/21 kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na: kukamilisha Upembuzi Yakinifu (*Feasibility Study*); na kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii; pamoja na kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa mradi. Kiasi cha **Shilingi bilioni 1.038** zimetengwa katika mwaka 2020/21 ili kutekeleza kazi hizo. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Novemba, 2021 na kukamilika mwezi Desemba, 2023.

Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Kinyerezi I Extension – MW 185

41. Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusu upanuzi wa kituo cha Kinyerezi I – MW 150 kwa kuongeza mitambo itakayozalisha **MW 185** na hivyo kufanya kituo hicho kuzalisha jumla ya **MW 335**. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa **asilimia 100** kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 188** sawa na takriban **Shilingi bilioni 439.1**. Kwa ujumla ujenzi wa mradi umefikia **asilimia 84**.

42. Mheshimiwa Spika, Kutokana na mkandarasi wa awali kushindwa kukamilisha mradi huu, Serikali kuititia TANESCO inakamilisha taratibu za kumpata mkandarasi wa kukamilisha kazi zilizobaki. Fedha za ndani **Shilingi bilioni 138.0** zimetengwa katika mwaka 2020/21 kwa ajili ya kukamilisha mradi huu. Ujenzi wa mradi huu unatarajia kukamilika mwezi Desemba, 2020.

Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Mtwara – MW 300

43. Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusu ujenzi wa mitambo ya kuzalisha umeme wa **MW 300** kwa kutumia gesi asilia katika Mkoa wa Mtwara. Gharama za mradi

zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 421.1** sawa na takriban **Shilingi bilioni 983.31**. Mradi utahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **KV 400** yenye urefu wa kilomita 270 kutoka Mtwara hadi Somanga Fungu kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 113** sawa na takriban **Shilingi bilioni 263.87** na vituo vya kupoza umeme ambavyo vitagharimu **Dola za Marekani milioni 166.2** sawa na takriban **Shilingi bilioni 388.09**. Katika mwaka 2019/20 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: kukamilika kwa Upembuzi Yakinifu wa kituo cha kuzalisha umeme na njia ya kusafirisha umeme; na Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii katika miundombinu wezeshi (maji, barabara na bomba la gesi).

44. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/21 kazi zitakazofanyika ni kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi na kukamilisha taratibu za upatikanaji wa fedha za ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme. Serikali imetenga **Shilingi milioni 500** kuwezesha utekelezaji wa kazi hizo. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwaa kuanza mwezi Agosti, 2021 na kukamilika mwezi Septemba 2024.

Miradi wa Kuzalisha Umeme ya Nishati Jadidifu (Umeme Jua MW 150, Upepo MW200) na Makaa ya Mawe MW 600

45. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/20 Serikali imeendelea na taratibu za kuwapata Wazalishaji Binafsi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hii. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2020 tathmini ya zabuni (*tender evaluation*) kwa kampuni 11 zilizorudisha zabuni kati ya 38 zilizopita mchujo wa kwanza (*Shortlisted*) ilikamilika. Kazi inayoendelea sasa ni kukamilisha maandalizi kwa ajili ya kuanza majadiliano na kampuni hizo.

46. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2020/21, Serikali itakamilisha taratibu za kuwapata Wawekezaji Binafsi wenye gharama na masharti nafuu

katika kutekeleza miradi hiyo. Utekelezaji huo unatarajiwa kuanza mwezi Novemba, 2020 na kukamilika mwezi Oktoba, 2022.

MIRADI YA KUSAFIRISHA UMEME

Mradi wa Kusafirisha umeme kutoka Singida – Arusha – Namanga kV 400

47. Mheshimiwa Spika, mradi huu unahuishisha ujenzi wa njia ya umeme msongo wa **kV 400** yenye urefu wa kilomita 414 kutoka Singida hadi Namanga kuititia Arusha. Aidha, mradi unahuishisha ujenzi wa kituo kipyaa cha kupoza umeme cha Kisongo Mkoani Arusha na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Singida. Kazi nyingine ni usambazaji wa umeme katika vijiji 19 vilivyo jirani na mkuza wa njia ya umeme katika Mikoa ya Singida, Manyara na Arusha. Gharama za mradi ni **Dola za Marekani milioni 258.82** sawa na takriban **Shilingi bilioni 604.37**. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2020 jumla ya nguzo 621 kati ya 1,072 zimesimikwa na hivyo kufanya utekelezaji wa mradi kufikia **asilimia 67**.

48. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huu unaenda sambamba na utekelezaji wa mradi wa *Backbone* awamu ya pili (*Backbone Phase II*) unaolenga kuongeza uwezo (*Upgrade*) wa vituo vya kupoza umeme kutoka **kV 220** mpaka **kV 400** katika Mikoa ya Iringa, Shinyanga, Singida na Dodoma ambapo utekelezaji umefikia **asilimia 83**.

49. Mheshimiwa Spika, kazi zilizopangwa kufanyika mwaka 2020/21 ni: kuendelea na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na vituo vya kupoza umeme vya Dodoma na Singida. Jumla ya **Shilingi bilioni 30.21** fedha za nje zimetengwa katika mwaka 2020/21 ili kutekeleza kazi hizo. Mradi huu ulianza kutekelezwa mwezi Machi, 2018 na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Desemba, 2020.

Mradi wa njia ya kusafirisha Umeme kutoka Makambako hadi Songea kV 220 na Usambazaji wa Umeme Vijiji kwa Mikoa ya Njombe na Ruvuma

50. Mheshimiwa Spika, mradi huu unahu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa **kV 220**, yenye urefu wa kilomita 250 kutoka Makambako hadi Songea kuitia Madaba pamoja na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Madaba na Songea na upanuzi wa kituo cha Makambako. Mradi huu umekamilika kwa **asilimia 100** mwezi Septemba, 2018 na kazi ya kuunganisha wateja wapya inaendelea.

51. Mheshimiwa Spika, Vilevile, kazi ya kufunga *reactor* na *distribution panel* katika kituo cha Madaba ilikamilika mwezi Septemba, 2019 na kwa sasa hali ya upatikanaji umeme katika Mkoa wa Ruvuma imeimarika. Serikali kuitia TANESCO na REA inaendelea kuwahamasisha wananchi wajitokeze kwa wingi kuunganishiwa umeme.

Mradi wa Njia ya kusafirisha Umeme kutoka Bulyanhulu – Geita kV 220

52. Mheshimiwa Spika, Mradi huu unahu ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa **kV 220** yenye urefu wa kilomita 55 kutoka Bulyanhulu hadi Geita na kituo cha kupoza umeme cha Geita, upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Bulyanhulu, usambazaji wa umeme katika Vijiji 10 vilivyopo katika eneo la mradi na kuunganisha wateja wa awali 1,500 katika Mkoa wa Geita. Gharama za mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 23.0** sawa na takriban **Shilingi bilioni 53.71**. Kazi ya ujenzi na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme na ujenzi wa njia za kusafirisha umeme zimekamilika kwa **asilimia 82**. Mkandarasi wa usambazaji umeme vijiji anaendelea na kazi za ufungaji wa mashineumba na kuunganishia wateja. Kazi ya usambazaji umeme imefikia **asilimia 92** na hivyo kufanya utekelezaji mzima wa mradi kufikia **asilimia**

85. Ujenzi wa mradi huu ulianza mwezi Januari, 2019 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2020. Aidha, kwa mwaka 2020/21 Serikali itaendelea kufuatilia na kutathmini ubora wa kazi zilizotekelozwa.

Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kutoka Geita – Nyakanazi kV 220

53. Mheshimiwa Spika, Mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 220** yenye urefu wa kilomita 144, ujenzi wa vituo vya kupoza umeme Geita na Nyakanazi na kusambaza umeme katika vijiji 32 vinavyopitiwa na mradi katika maeneo ya Geita Mjini hadi Bwanga na Nyakanazi hadi Kakonko. Gharama za utekelezaji wa Mradi huu ni **EURO milioni 45** sawa na takriban **Shilingi bilioni 117.79**. Katika mwaka 2019/20 kazi zilizofanyika ni pamoja na: upimaji wa udongo na usanifu wa mradi; ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; na kuanza ujenzi wa kituo cha kupoza umeme.

54. Mheshimiwa Spika, kazi zilizopangwa kutekelezwa mwaka 2020/21 ni pamoja na: kukamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Geita hadi Nyakanazi; kukamilisha ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Geita; na kusambaza umeme katika vijiji 32 vitakavyopitiwa na mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 25.33** zimetengwa katika mwaka 2020/21 kwa ajili ya shughuli za mradi huu. Ujenzi wa mradi huu ulianza mwezi Agosti, 2019 na unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2021.

Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kutoka Rusumo – Nyakanazi kV 220

55. Mheshimiwa Spika, Mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 220** yenye urefu wa kilomita 98 kutoka kituo cha kuzalisha umeme cha Rusumo hadi Nyakanazi. Gharama za Mradi ni **Dola**

za Marekani milioni 35 sawa na takriban **Shilingi bilioni 81.73**. Katika mwaka 2019/20 kazi zilizofanyika ni pamoja na: upimaji wa njia (*detail survey*); kusafisha njia ya umeme na ujenzi wa barabara za kuwezesha kufikia eneo la mradi (*access roads*); na usanifu wa nguzo (*Tower Spotting*). Ujenzi wa mradi huu ulianza mwezi Oktoba, 2019 na unatarajiwa kukamilika mwezi Novemba, 2020.

Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kutoka Iringa - Mbeya - Tunduma - Sumbawanga - Mpanda - Kigoma - Nyakanazi (North West Grid) KV 400

56. Mheshimiwa Spika, mradi huu unahu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **KV 400** kutoka Iringa – Mbeya – Tunduma – Sumbawanga – Mpanda – Kigoma – Nyakanazi yenye urefu wa kilomita 1,384. Mradi utatekelezwa kwa awamu tatu kama ifuatavyo:

Awamu ya Kwanza: Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kutoka Iringa - Mbeya - Tunduma hadi Sumbawanga KV 400

57. Mheshimiwa Spika, awamu hii inahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **KV 400** kutoka Iringa kupitia Mbeya, Tunduma hadi Sumbawanga yenye urefu wa kilomita 624 na vituo vya kupoza umeme vya Kisada, Mbeya, Tunduma na Sumbawanga. Awamu hii itagharimu jumla ya **Dola za Marekani milioni 465** sawa na takriban **Shilingi triliioni 1.085**. Kazi zilizotekeliza kwa mwaka 2019/20 ni pamoja na: kudurusu taarifa ya awali ya Upembuzi Yakinifu kati ya Mbeya na Sumbawanga; kukamilisha uthamini wa mali zitakazopitiwa na mradi na uainishaji wa mipaka ya mkuza wa mradi.

58. Mheshimiwa Spika, kazi zilizopangwa kufanyika kwa mwaka 2020/21 ni: ulipaji wa fidia wananchi watakaopisha mradi; kuhuisha Tathmini ya Athari kwa Mazingira; kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa mradi;

na kuanza ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na vituo vinne (Kisada, Mbeya, Tunduma na Sumbawanga) vya kupoza umeme. Jumla ya **Shilingi bilioni 1** zimetengwa katika mwaka 2020/21 ili kutekeleza kazi hizo. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Septemba, 2020 na kukamilika mwezi Novemba, 2022.

Awamu ya Pili: Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kutoka Nyakanazi hadi Kigoma KV 400

59. Mheshimiwa Spika, awamu hii itahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **KV 400** kutoka Nyakanazi hadi Kigoma yenyе urefu wa kilomita 280, ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Kidahwe Mkoani Kigoma, upanuzi wa kituo cha kupoza umeme Nyakanazi na usambazaji wa umeme vijijiini. Gharama ya Mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 187** sawa na takriban **Shilingi bilioni 433.17**. Kazi zilizofanyika kwa mwaka 2019/20 ni pamoja na: kuendelea na kazi ya Upembizi Yakinifu na uandaaji wa nyaraka za kumpata Mkandarasi wa ujenzi; kukamilisha ununuzi wa vifaa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kuwaunganishia umeme wateja 5,000 katika Mkoa wa Kigoma; na kukamilika kwa tathmini na kuanza kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa mradi katika kituo cha kupoza umeme cha Kidahwe.

60. Mheshimiwa Spika, kazi zilizopangwa kutekelezwa mwaka 2020/21 ni pamoja na: kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; kukamilisha Upembizi Yakinifu; na kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 34.28** zimetengwa ili kutekeleza kazi hizo. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Juni, 2020 na kukamilika mwezi Juni, 2022.

Awamu ya Tatu: Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kutoka Sumbawanga – Mpanda – Kigoma KV 400

61. Mheshimiwa Spika, awamu hii inahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **KV 400** kutoka Sumbawanga hadi Kigoma kupitia Mpanda yenye urefu wa kilometra 480. Mradi huu unakadirwa kugharimu **Dola za Marekani milioni 200** sawa na takriban **Shilingi bilioni 463**. Kwa sasa Mradi upo katika hatua ya kumpata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kuandaa ripoti ya mazingira. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2022 na kukamilika mwezi Juni, 2024.

Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kutoka Kituo cha Kuzalisha Umeme Cha Julius Nyerere KV 400

62. Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **KV 400** kutoka kituo cha kuzalisha umeme cha Julius Nyerere hadi Dodoma kupitia Chalinze na Chalinze hadi Kinyerezi. Mradi utatekelezwa kwa awamu mbili kama ifuatavyo:

Awamu ya Kwanza: Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kutoka Kituo cha Kuzalisha Umeme cha Julius Nyerere – Chalinze – Dodoma KV 400

63. Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa **KV 400** wenye urefu wa kilomita 505 kutoka kituo cha kuzalisha umeme cha Julius Nyerere kupitia Chalinze mkoani Pwani hadi Dodoma na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme vya Chalinze na Dodoma. Gharama za mradi ni **Dola za Marekani milioni 305.21** sawa na takriban **Shilingi bilioni 712.71**. Kazi zilizofanyika mwaka 2019/20 ni kukamilika kwa Upembizi Yakinifu, uandaaji wa makabrasha ya zabuni na tathmini ya mali za wananchi watakaopisha mradi.

64. Mheshimiwa Spika, kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka 2020/21 ni: kulipa fidia wananchi watakaopisha mradi; kumpata Mkandarasi wa ujenzi; na kuanza ujenzi wa mradi. **Shilingi bilioni 8.14** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Agosti, 2020 na kukamilika mwezi Desemba, 2021.

Awamu ya Pili: Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kutoka Chalinze hadi Kinyerezi kV 400

65. Mheshimiwa Spika, mradi huu utahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 400** yenye urefu wa kilomita 115 kutoka Chalinze hadi Kinyerezi pamoja na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Kinyerezi. Gharama za mradi ni **Dola za Marekani milioni 112** sawa na takriban **Shilingi bilioni 261.53**. Kazi zilizotekeliza kwa mwaka 2019/20 ni kukamilisha Upembizi Yakinifu; na tathmini ya mali za wananchi watakaopisha mradi.

66. Mheshimiwa Spika, kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka 2020/21 ni pamoja na: kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Kinyerezi; kuanza kulipa fidia wananchi watakaopisha mradi; na kuanza ujenzi wa mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 3.89** zimetengwa katika mwaka 2020/21 kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Agosti, 2020 na kukamilika mwezi Desemba, 2021.

Mradi wa kuunganisha Mikoa ya Kigoma na Katavi katika Gridi ya Taifa

67. Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 132** kwa ajili ya kuunganisha mikoa ya Kigoma na Katavi katika Gridi ya Taifa. Mradi huu ulizinduliwa na Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania tarehe 11 Oktoba, 2019. Mradi huu unatekelezwa katika awamu mbili kama ifuatavyo:

(i) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kwa Ajili ya Kuunganisha Mkoa wa Kigoma katika Gridi ya Taifa kutokea Tabora KV 132

68. Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **KV 132** kutoka Tabora hadi Kigoma kupitia Urambo na Nguruka umbali wa kilomita 395 pamoja na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Urambo, Nguruka na Kidahwe. Gharama za mradi huu zinakadiriwa kuwa takriban **Shilingi bilioni 66.7**.

69. Mheshimiwa Spika, kazi zilizotekelawa mwaka 2019/20 ni pamoja na kukamilisha: Upembuzi Yakinifu; upatikanaji wa maeneo ya kujenga vituo vya kupoza umeme vya Urambo, Nguruka na Kidahwe; upimaji wa njia ya kusafirisha umeme (*route survey*); na uwekaji wa alama za mipaka ya njia (*route demarcation*) ya kusafirisha umeme pamoja na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Urambo.

70. Mheshimiwa Spika, kazi zilizopangwa kufanyika kwa mwaka 2020/21 ni: kuendelea na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme; kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; na kuanza ujenzi wa njia za kusafirisha umeme kwenda Kigoma kutoka Tabora. **Shilingi bilioni 5** zimetengwa ili kutekeleza kazi hizo. Kazi za ujenzi wa Mradi zilianza mwezi Oktoba, 2019 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2021.

(ii) Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kwa Ajili ya Kuunganisha Mkoa wa Katavi katika Gridi ya Taifa Kutoka Tabora KV 132

71. Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **KV 132** kutoka Tabora hadi Katavi kupitia Ipole na Inyonga

umbali wa kilomita 381 pamoja na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Ipole, Inyonga na Mpanda mkoani Katavi. Gharama za mradi zinakadiriwa kuwa **Shilingi bilioni 64.5.**

72. Mheshimiwa Spika, kazi zilizofanyika mwaka 2019/20 ni pamoja na kukamilisha: Upembuzi Yakinifu wa awali (*Pre-feasibility Study*); upatikanaji wa maeneo ya kujenga vituo vya kupoza umeme vya Ipole, Inyonga na Mpanda; na uwekaji wa alama za mipaka (*route demarcation*) ya njia ya kusafirisha umeme. Aidha, tathmini ya mali za wananchi watakaopisha ujenzi wa mradi na Tathmini ya Athari kwa Mazingira zinaendelea. Ujenzi wa kituo cha Mpanda ulianza mwezi Septemba 2019 na kituo cha Inyonga umeanza mwezi Aprili 2020.

73. Mheshimiwa Spika, kazi zilizopangwa kufanyika kwa mwaka 2020/21 ni: kukamilisha ujenzi wa vituo vya kupoza umeme; kulipa fidia wananchi watakaopisha mradi; na kuanza ujenzi wa njia za kusafirisha umeme kwenda Kigoma kutokea Tabora. **Shilingi bilioni 5** zimetengwa ili kutekeleza kazi hizo. Mradi ulianza mwezi Januari, 2019 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2021.

Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme KV 220 na Kituo cha Kupoza Umeme katika Mkoa wa Simiyu

74. Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **KV 220** yenye urefu wa kilomita 160 kutoka Ibadakuli Mkoani Shinyanga hadi Imalilo Mkoani Simiyu. Gharama ya mradi inakadiriwa kuwa **Shilingi bilioni 75**. Hadi sasa, ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Imalilo umekamilika.

75. Mheshimiwa Spika, kazi zilizopangwa kufanyika kwa mwaka 2020/21 ni pamoja na kukamilisha: Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii; uainishajii

wa mipaka ya mkuza wa njia ya kusafirisha umeme; na tathmini ya mali za wananchi watakaopisha mradi. Katika mwaka 2020/21, Serikali kupitia TANESCO imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 1** kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2021 na kukamilika mwezi Desemba, 2022.

Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kwa Ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Mwendo Kasi (Standard Gauge Railway – SGR) Awamu ya Kwanza (Lot I) KV 220

76. Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya umeme msongo wa **kV 220** yenye urefu wa kilomita 160 kutoka Kinyerezi - Dar es Salaam hadi Msamvu - Morogoro kwa ajili ya kuendesha Treni ya Mwendokasi (*Standard Gauge Railway – SGR*) awamu ya kwanza. Gharama ya mradi ni **Shilingi bilioni 76.23** na unagharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa **asilimia 100**.

77. Mheshimiwa Spika, kazi zilizofanyika ni pamoja na: ujenzi wa misingi ya minara ya umeme (*Tower Foundations*) 444 kati ya 456 imejengwa; ujenzi wa minara (*Towers erections*) 404 kati ya 456; uvutaji wa nyaya kwa urefu wa kilomita 88 kati ya 160 na kulipa fidia wananchi waliopisha mradi. Utekelezaji wa mradi huu kwa ujumla umefikia **asilimia 89**. Mradi ulianza kutekelezwa mwezi Januari, 2019, na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Mei, 2020.

Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kwa Ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Mwendo Kasi (Standard Gauge Railway – SGR) Awamu ya Pili (Lot II) KV 220

78. Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 220** yenye urefu wa kilometra 410 kutoka Msamvu, mkoani Morogoro hadi Makutupora, mkoani Singida kwa ajili ya kuendesha treni ya mwendokasi. Mradi huu

umegawanyika katika sehemu kuu mbili (2) ambapo sehemu ya kwanza ni kutoka Morogoro hadi Ihumwa - Dodoma, yenye urefu wa kilomita 236 na sehemu ya pili ya mradi huu ni kutoka Ihumwa hadi Kintinku - Singida wenyе urefu wa kilomita 174. Kazi za ujenzi wa mradi huu zinatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi Mei, 2020 na kukamilika mwezi Julai 2021. Gharama za mradi huu zinakadiriwa kuwa **Shilingi bilioni 201**.

MIRADI YA KUBORESHA NJIA ZA USAMBAZAJI UMEME

Mradi wa Kuboresha Mfumo wa Usambazaji Umeme Katika Jiji la Dodoma

79. Mheshimiwa Spika, mradi huu utahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa **KV 220** kutoka Zuzu kwenda Msalato na kutoka Zuzu kwenda Kikombo pamoja na ujenzi wa vituo viwili (2) vipyta vya kupoza na kusambaza umeme katika maeneo ya Msalato na Ihumwa Jijini Dodoma. Gharama ya mradi ni **Dola za Marekani milioni 167.7** sawa na takriban **Shilingi bilioni 388.46**. Kazi zilizofanyika kwa mwaka 2019/20 ni pamoja na kukamilisha Upembuzi Yakinifu wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **KV 220** na njia za kusambaza umeme msongo wa **KV 33**. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Juni, 2021 baada ya kukamilika taratibu za kupata ufadhilli na wakandarasi wa kutekeleza mradi. Mradi unategemewa kukamilika mwezi Julai, 2023.

Mradi wa Usambazaji Umeme kwa Maeneo ya Mijini (Urban Electrification Program)

80. Mheshimiwa Spika, mradi huu unalenga kuwezesha TANESCO kuongeza kasi ya kuunganisha wateja maeneo ya mijini na kupanua miundombinu ya usambazaji umeme ili kuhamasisha ujenzi wa viwanda. Katika mwaka 2019/20, kazi zilizofanyika ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa njia za usambazaji umeme katika maeneo mbalimbali nchini ambapo

jumla ya kilomita 312 za msongo wa **KV 33** na kilomita 578 msongo wa **KV 0.4** zimejengwa. Aidha, mashineumba 216 zimefungwa na wateja wapya 9,071 wameunganishwa.

81. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2020/21, kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kujenga jumla ya kilomita 280.16 za njia ya msongo wa **KV 11**, kilomita 734.8 za msongo wa **KV 33**, kilomita 4,126.74 za msongo wa **KV 0.4**, kufunga mashineumba 1,161, kuunganisha wateja wapya 149,098 na maboresho ya miundombinu ya usambazaji. Jumla ya **Shilingi bilioni 209.8** zimetengwa katika mwaka 2020/21 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo. Utekelezaji wa mradi huu ni endelevu katika mikoa yote.

MIRADI YA KUSAMBAZA UMEME VIJJINI

82. Mheshimiwa Spika, mradi wa Kusambaza Umeme Vijiji Awamu ya Tatu unalenga kufikisha umeme katika vijiji 7,873. Aidha, hadi kufikia Desemba 2015, jumla ya vijiji 2,018 vilikuwa vimefikiwa na huduma ya umeme. Idadi hiyo imeongezeka na kufikia 9,112 mwezi Aprilli, 2020 sawa na ongezeko la vijiji 7,094.

83. Mheshimiwa Spika, Vijiji 1,822 ambavyo ni sawa na asilimia 14.86 vitakavyobakia baada ya mwezi Juni, 2020 vitapelekewa umeme kupitia Mradi wa Kupeleka Umeme Vijiji Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili (*Turnkey Phase III – Round II*) uliopangwa kutekelezwa katika Mwaka 2020/21. Kukamilika kwa mradi huo kutafanya vijiji vyote kufikiwa na umeme.

84. Mheshimiwa Spika, kazi zitakazofanyika mwaka 2020/21 ni pamoja na: kujenga miundombinu ya kusambaza umeme; kuendelea kusambaza umeme katika maeneo yaliyopo pembezoni mwa Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani; kusambaza umeme kwenye vitongoji vilivyopitiwa na miundombinu ya usambazaji umeme wa msongo wa kati kupitia Mradi wa ujazilizi

(*Densification*); kuunganisha wateja na ufungaji wa mifumo ya nishati jadidifu katika maeneo yaliyo mbali na Gridi zikiwemo Taasisi za Umma, visiwa katika Bahari ya Hindi, Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika na Delta ya Rufiji.

85. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Aprili, 2020 jumla ya Wilaya na Halmashauri 36 za Tanzania Bara vijiji vyake vyote vimefikiwa na ujenzi wa miundombinu ya umeme. Vitongoji na maeneo ambayo hayajafikiwa na miundombinu ya umeme yataendelea kupelekewa umeme kuanzia mwezi Juni, 2020.

86. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwezi Januari, 2016 hadi Machi 2020, jumla ya Taasisi **11,164** zimeunganishiwa umeme ikilinganishwa na Taasisi **4,036** zilizokuwa zimeunganishiwa kufikia mwezi Desemba, 2015 sawa na ongezeko la **asilimia 184.88**. Ongezeko hilo linafanya jumla ya Taasisi zilizouanganishiwa umeme kufikia **15,200**.

Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu - Mzunguko wa Kwanza

87. Mheshimiwa Spika, lengo la mradi huu ni kufikisha umeme katika vijiji 3,559 ambavyo havijafikiwa na umeme. Gharama za mradi ni **Shilingi trilioni 1.157**. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020 jumla ya vijiji 2,659 sawa na **asilimia 70.21** vimepatiwa umeme na kuunganisha jumla ya wateja 75,210 kati ya 180,768 waliolengwa. Mradi ulianza mwezi Julai, 2018 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2020. Katika mwaka 2020/21, Serikali itaendelea kusimamia na kutathmini ufanisi wa mradi.

Miradi ya Usambazaji Umeme katika Maeneo ambayo yamefikiwa na Miundombinu ya Umeme (*Densification*)

(i) Mradi wa Ujazilizi Mzunguko wa Pili A

88. Mheshimiwa Spika, mradi huu unalenga kupeleka umeme kwenye vitongoji ambavyo havijapatiwa umeme katika mikoa tisa (9) ya Dodoma, Kilimanjaro, Tabora, Shinyanga, Mwanza, Singida, Pwani, Tanga, na Mbeya ambapo jumla ya vitongoji 1,103 na wateja wa awali 69,079 wataunganishiwa umeme. Mradi huu utagharimu **Shilingi bilioni 197.8**. Utekelezaji wa mradi huu umeanza mwezi Mei, 2020 na unatarajiwa kukamilika mwezi Machi, 2021.

(ii) Mradi wa Ujazilizi Mzunguko wa Pili B

89. Mheshimiwa Spika, mradi huu utahusisha kupeleka umeme katika vitongoji ambavyo havijafikiwa na umeme katika mikoa 16 ya Kagera, Geita, Mara, Simiyu, Kigoma, Katavi, Rukwa, Iringa, Njombe, Morogoro, Ruvuma, Mtwara, Lindi, Manyara, Arusha na Songwe ambapo jumla ya vitongoji 2,400 vitapatiwa umeme na kuunganishwa wateja wa awali 95,000 kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 100**. Mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2020 na kukamilika mwezi Mei, 2021.

Mradi wa Usambazaji Umeme katika Vijiji vilivyopo Pembezoni mwa Miji (vijiji miji) – Peri Urban

90. Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusisha kusambaza umeme katika maeneo yaliyopo pembezoni mwa miji (vijiji miji) katika wilaya za Mkoa wa Pwani na Wilaya ya Kigamboni ambapo ulianza kutekelezwa mwezi Agosti, 2019 katika mitaa 50, vijiji 36, vitongoji 76 na maeneo 88. Mradi unahusisha ujenzi wa njia za msongo wa kati za urefu wa kilomita 623.65, msongo mdogo kilomita 1,277.8, ufungaji wa mashineumba 442 na kuunganisha wateja wa awali 37,713 kwa

gharama ya **Shilingi bilioni 74.33**. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2020 ambapo jumla ya vijiji, vitongoji na mitaa 218 vinatarajiwa kuunganishiwa umeme. Aidha, katika Mwaka 2020/21, Serikali imepanga kutekeleza mradi wa kusambaza umeme katika maeneo yaliyopo pembezoni mwa Jiji la Dodoma na Mwanza. Jumla ya **Shilingi bilioni 29** zimetengwa kutekeleza mradi huo.

Mradi ya Uendelezaji wa Nishati Jadidifu - Off-Grid

91. Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusu usambazaji wa nishati jadidifu katika maeneo yaliyo nje ya mfumo wa gridi ya Taifa pamoja na visiwa. Katika Awamu ya Kwanza, jumla ya Kampuni Binafsi 14 zimepatiwa **Shilingi bilioni 16.88** na hivyo kuwezesha vijiji 102 kati ya 119 vilivyopo kwenye Mpango kupatiwa umeme ambayo ni sawa na **asilimia 86**. Vijiji vilivyobaki 57 kati ya vijiji vyote 176 vitapatiwa umeme kupitia Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili uliopangwa kutekelezwa katika mwaka 2020/21.

92. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2019/20 Wizara ilitangaza zabuni za kuwapata waendelezaji wa miradi ya nishati jadidifu nje ya mfumo wa Gridi ya Taifa (*Call for Proposal – Round 2*) mwezi Novemba, 2019 ambapo maandiko ya miradi (*Project proposals*) kutoka Kampuni 18 yenye thamani ya **Shilingi bilioni 36** yamepokelewa. Hatua inayofuata ni waombaji waliokidhi vigezo kuwasilisha taarifa kamili za mradi na mpango biashara kwa ajili ya uhakiki na kuanza utekelezaji.

Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu - Mzunguko wa Pili

93. Mheshimiwa Spika, mradi huu utahusisha kusambaza umeme katika vijiji 1,822 vilivyobaki. Kazi za mradi zitahusisha ujenzi wa kilometra 35,581 za njia za umeme za msongo wa kati (kV 33), ujenzi wa kilomita 21,777 za msongo mdogo (kV 0.4), kufunga

mashineumba 7,386 na kuunganisha wateja wa awali zaidi ya 582,937. Ujenzi wa mradi utaanza mwezi Julai, 2020 na kukamilika mwezi Juni, 2021. Katika mwaka wa fedha wa 2020/21 jumla ya **Shilingi bilioni 297.43** zimetengwa kugharamia utekelezaji wa mradi huo.

SEKTA NDOGO YA NISHATI JADIDIFU

Uzalishaji Umeme Kutumia Vyanzo vya Nishati Jadidifu

94. Mheshimiwa Spika, nishati jadidifu ni mojawapo ya vyanzo vya nishati ambavyo vimejengewa mazingira wezeshi ili kuchangia upatikanaji wa nishati nchini. Katika mwaka 2019/20, Wizara kwa kushirikiana na EWURA na TANESCO imekamilisha durusu za Kanuni za uendelezaji miradi midogo ya umeme kupitia wazalishaji wadogo *Electricity (Development of Small Power Projects) Rules, 2019*. Kutokana na Kanuni hizo, kuanzia mwezi Juni 2019, Serikali kupitia EWURA imeanza kudhibiti bei zinazotozwa na makampuni yanayotoa huduma za umeme katika maeneo ambayo hayajafikiwa na Gridi ya Taifa ili kuweka ulinganifu wa bei za umeme kwa watumiaji.

95. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/20 Serikali kupitia EWURA imesajili miradi 12 midogo ya uzalishaji na usambazaji umeme nchini yenye uwezo wa **KW 317.78** kwa kutumia nguvu ya juu. Miradi hiyo inaendeshwa na Kampuni za PowerCorner (T) Ltd na PowerGen Renewable Energy Ltd katika Kijiji cha Kiegei Wilaya ya Nachingwea; Kijiji cha Lukumbule, Wilaya ya Tunduru; Kijiji cha Holola, Wilaya ya Nanyumbu; Kijiji cha Kalya, Wilaya ya Uvinza; Kijiji cha Kagerankanda, Wilaya ya Kasulu; Kijiji cha Itabagumba, Wilaya ya Buchosa; katika vijiji vya Busenge, Kanyala, Iglansoni, Mwenge na Mgambo, Wilaya ya Sikonge. Vilevile, EWURA imetoa leseni za kipindi kifupi kwa Kampuni ya Mwenga Hydro Ltd kwa mradi wa kuzalisha umeme **MW 2.5** kwa kutumia

nguvu za maji. Umeme huu utaingizwa katika Gridi ya Taifa na kuuzwa kwa wananchi wa Vijiji vya jirani.

Matumizi Bora ya Nishati (*Energy Efficiency*)

96. Mheshimiwa Spika, Mpango wa Matumizi Bora ya Nishati unalenga kutoa mwongozo wa utekelezaji wa masuala ya matumizi sahihi ya nishati katika sekta za ujenzi, usafiri, umeme na nishati kwa matumizi ya nyumbani ikiwemo kupikia. Katika mwaka 2019/20, Wizara imeshiriki katika maandalizi ya mradi wa kikanda wa *Energy Efficient Lighting and Appliances* (EELA).

97. Mheshimiwa Spika, kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka 2020/21 ni pamoja na: kuhuisha Mkakati wa Kitaifa wa Matumizi Bora ya Nishati (*National Energy Efficiency Strategy*) katika Mpango Kazi wa Matumizi Bora ya Nishati; kuzijengea uwezo wa kitaalamu na vifaa taasisi zitakazoshiriki katika utekelezaji wa Mpango Kazi wa Matumizi Bora ya Nishati; na kuanzisha miradi ya Mfano kwa nia ya kuhamasisha matumizi bora ya nishati nchini.

Programu ya NishatiEndelevu kwa Wote (Sustainable Energy for All – SE4ALL)

98. Mheshimiwa Spika, programu hii inafadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa-UNDP. Kupitia programu hii, mwaka 2018 Wizara kwa kushirikiana na TANESCO ilihakiki na kubainisha maeneo yanayofaa kwa uzalishaji wa nishati ya umeme-jua katika maeneo ya Same (Kilimanjaro), Zuzu (Dodoma) na Manyoni (Singida). Mwaka 2019 ulifanyika Upembuzi Yakinifu wa Awali (*Pre-feasibility Study*) katika eneo la Mkwese, Manyoni na kubaini uwezekano wa kuzalisha **MW 150** za umeme Jua. Kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka 2020/21 ni kukamilisha Upembuzi Yakinifu katika eneo la Mkwese na kuanza hatua za awali za utekelezaji wa mradi.

Jumla ya **Shilingi milioni 460** zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo.

Kuridhia na Kutekeleza Mikataba ya Kimataifa Katika Uendelezaji wa Nishati Jadidifu

99. Mheshimiwa Spika, katika jitihada za uendelezaji wa nishati jadidifu hapa nchini, mwaka 2019 Serikali kupitia Wizara ya Nishati ilikamilisha taratibu za kujunga na Ushirikiano wa Kimataifa wa Nishati ya Jua (*International Solar Alliance – ISA*). Kupitia Bunge lako Tukufu, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliridhia Mkataba huo mwezi Novemba, 2019. Kujiunga na Taasisi hiyo kutainufaisha Tanzania katika kupata misaada, mikopo nafuu, teknolojia pamoja na utaalam katika uendelezaji wa miradi ya nishati ya jua.

Uendelezaji wa Rasilimali ya Jotoardhi (Geothermal)

100. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Kampuni Tanzu ya TANESCO (TGDC), katika mwaka 2019/20 imeendelea na utekelezaji wa miradi mitano (5) ya kimkakati ya jotoardhi ambayo ni Ngozi, Kiejo-Mbaka, Songwe, Luhoi na Natron. Sambamba na utekelezaji wa miradi hiyo, Serikali imeendelea kuweka mazigira wezeshi ikiwemo kuandaa Sheria mahsus kwa ajili ya kusimamia na kuendeleza jotoardhi nchini. Maandalizi ya Sheria hiyo yamefikia hatua nzuri ambapo wadau husika wametoa maoni. Aidha, kukamilika kwa Sheria hiyo kutaimairisha mfumo wa kitaasisi katika uendelezaji, usimamizi na udhibiti wa rasilimali ya jotoardhi nchini. Kwa mwaka 2019/20, Serikali kupitia TGDC imeendelea na utekelezaji wa miradi mitatu (3) ya kipaumbele ambayo ni Ngozi, Songwe na Kieji - Mbaka kama ifuatavyo:-

(i). Mradi wa Ngozi (Mbeya)

101. Mheshimiwa Spika, mradi huu unahuishisha uzalishaji umeme wa **MW 30** katika chanzo cha mlima

wa volkano wa Ngozi. Kwa mwaka 2019/20 kazi zilizoteklezwa ni pamoja na: kumpata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kuandaa Mpango Kazi wa uchorongaji na kusimamia uchorongaji; usanifu wa visima; uainishaji wa vigezo vya mitambo kwa ajili ya uchorongaji; kununua mtambo wa uchorongaji wa visima; kubainisha njia ya miundombinu ya barabara na maji pamoja na kukamilisha usanifu wa awali wa miundombinu.

102. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/21, Serikali kupitia TGDC itakamilisha shughuli za uchorongaji wa visima vitatu (3) vya utafiti kwa ajili ya uhakiki wa rasilimali ya jotoardhi katika maeneo hayo. Jumla ya **Shilingi milioni 419** zimetengewa kwa ajili ya kazi hizo.

(ii). Mradi wa Songwe

103. Mheshimiwa Spika, mradi huu unahu unahusu uzalishaji wa umeme wa **MW 5** na matumizi mengineyo (*direct heat uses*) katika eneo la Majimoto-Songwe. Kazi zilizofanyika ni pamoja na: upatikanaji wa leseni ya eneo la Songwe; kusanifu mradi wa matumizi mengine pamoja na kutwaa ardhi kwa ajili ya uendelezaji wa miradi ya matumizi mengine.

104. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2020/21, kazi zitakazoteklezwa ni kufanya maandalizi ya uchorongaji wa visima vya utafiti ili kuhakiki rasilimali ya jotoardhi kwa ajili ya uzalishaji wa umeme na kukamilisha uendelezaji wa miradi ya matumizi mengine katika eneo la Songwe. Katika mwaka 2020/21 jumla ya **Shilingi milioni 816.76** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo.

(iii). Mradi wa Kiejo-Mbaka

105. Mheshimiwa Spika, mradi huu unahu unahusisha uzalishaji wa umeme wa **MW 10** na matumizi mengineyo katika maeneo ya Kiejo na Mbaka, mkoani Mbeya. Kazi zilizoteklezwa ni pamoja na:

kukamilika kwa uainishaji wa maeneo ya kuchoronga visima vifupi kwa ajili ya mradi wa matumizi mengine; kumpata Mkandarasi wa uchorongaji na kukamilisha uainishaji wa mahitaji ya ardhi kwa ajili ya mradi wa matumizi mengine.

106. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/21, kazi zilizopangwa ni: kukamilisha uchorongaji wa visima vifupi; kutekeleza mradi wa matumizi mengine; na kufanya maandalizi ya uchorongaji wa visima virefu vya utafiti. Jumla ya **Shilingi bilioni 4.53** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

Shughuli za Udhibiti wa Sekta Ndogo ya Umeme

107. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia EWURA imeendelea kusimamia na kudhibiti utendaji wa mafundi umeme wanaofanya kazi za kuunganisha mifumo ya umeme majumbani, viwandani na sehemu za biashara. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 Serikali kupitia EWURA imetoa leseni 782 kwa lengo la kuimarisha usalama wa wananchi na mali zao. Serikali kupitia Wizara ya Nishati inatoa rai kwa wananchi kutumia mafundi waliosajiliwa na kuacha kuwatumia mafundi wasiokuwa na leseni (vishoka).

108. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia EWURA katika mwaka 2019/2020 vilevile, imeendelea kuweka mazingira stahiki ya kiudhibiti ili kuwezesha utekelezaji wa miradi na kufanya ukaguzi katika miundombinu ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme.

SEKTA NDOGO YA MAFUTA NA GESI ASILIA

Shughuli za Utafutaji, Uendelezaji, Uzalishaji na Usambazaji wa Mafuta na Gesi Asilia Nchini

109. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2019/20 shughuli za utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia nchini zimeendelea. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2020 takriban **Futi za Ujazo Trilioni**

57.54 za gesi asilia zimegunduliwa. Kati ya kiasi hicho, gesi iliyogunduliwa nchi kavu ni **futi za ujazo Trilioni 10.41** na kwa upande wa kina kirefu cha bahari ni **futi za ujazo Trilioni 47.13**. Shughuli za uzalishaji zinafanyika katika vitalu viwili (2) vya Songo Songo na Mnazi Bay. Kiwango cha juu cha uzalishaji wa gesi asilia kimeongezeka kutoka **futi za ujazo milioni 95** kwa siku mwaka 2015/16 hadi **futi za ujazo milioni 210** kwa siku mwaka 2019/20 sawa na **ongezeko la asilimia 121.05**. Kiasi hiki cha gesi kinatumika katika uzalishaji wa umeme, viwandani, majumbani, taasisi pamoja na kwenye magari.

110. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia PURA imeendelea na udhibiti wa shughuli za mkondo wa juu zinazohusu utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia katika vitalu 11 nchini kupitia mikataba ya Uzalishaji na Ugawanaji Mapato (*Production Sharing Agreement - PSAs*). Vilevile, EWURA imeendelea kutunga kanuni ndogo (*rules*) na miongozo ya kuimarisha kazi ya udhibiti katika mkondo wa kati na wa chini wa mafuta na gesi ili kuboresha huduma zinazotolewa.

UTAFUTAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA KATIKA VITALU VYA KIMKAKATI UNAOTEKELEZWA NA SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLI TANZANIA (TPDC)

111. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia TPDC imeendelea na utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika vitalu vya kimkakati vikiwemo Mnazi Bay Kaskazini na Eyasi – Wembere. Utekelezaji na mipango ya miradi ya utafutaji na uendelezaji mafuta na gesi asilia nchini katika eneo la Mnazi Bay na Eyasi Wembere ni kama ifuatavyo:

(i). Kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini

112. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia TPDC imepanga kuchoronga visima viwili (2) ambapo kisima

kimoja ni cha utafutaji na kingine cha uhakiki. Uamuzi wa kuendeleza kitalu hiki umezingatia taarifa za awali katika eneo hilo zinazoonesha uwepo wa mashapo yenye uwezekano wa kuwa na gesi asilia. Kazi zilizotekelozwa mwaka 2019/20 ni pamoja na kukamilika kwa tathmini ya taarifa za kijiolojia na kijiofizikia na kumpata Mtaalamu Mshauri wa uchorongaji (*Drilling Management Consultant*). Katika mwaka 2020/21, kazi zitakazofanyika ni pamoja na kuchoronga visima vya utafutaji na uhakiki na kukamilisha rasimu ya Mkataba katika Serikali na TPDC kuhusu utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia katika kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini. Jumla ya **Shilingi biliioni 102** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo.

(ii). Kitalu cha Eyasi – Wembere

113. Mheshimiwa Spika, mradi huu umelenga kufanya shughuli za utafutaji wa mafuta katika kitalu cha Eyasi – Wembere kwa kufanya utafiti wa kijiolojia, kijiofizikia na kijioskemia ili kujiridhisha kuhusu uwepo wa mafuta katika kitalu hicho. Shughuli za awali za utafiti zilizotekelozwa kwa mwaka 2019/20 ni pamoja na: kukamilisha uchorongaji wa visima viwili (2) vifupi katika maeneo ya Kining'inila- Igunga na Nyaranja-Meatu kwa kutumia wataalamu wa TPDC na STAMICO; kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira; na kutoa elimu kwa jamii kuhusu mradi.

114. Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka 2020/21, kazi zitakazofanyika ni pamoja na: kuchoronga kisima kifupi cha utafutaji katika eneo la Luono - Singida; kukusanya, kuchakata na kutafsiri data za kijioskemia; kutayarisha moduli ya 3D ya *Airbone Gravity Gradiometry (AGG)*; kukamilisha taarifa za kimaabara za sampuli zilizokusanya kutoka visima vitatu (3); kuendelea na Tathmini ya Athari kwa Mazingira na kukusanya data za mitetemo za 3D. Katika mwaka 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 500** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

MIRADI YA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA USAFIRISHAJI NA USAMBAZAJI GESI ASILIA

(i) *Usambazaji wa Gesi Asilia kwa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani*

115. Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusu ujenzi wa miundombinu ya usambazaji gesi asilia katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani ambao utahusisha ujenzi wa miundombinu ya usambazaji kwa njia ya mabomba na gesi asilia iliyoshindiliwa (CNG) ambapo vituo vitano vitajengwa katika maeneo ya Chuo kikuu cha Dar es Salaam, Kituo cha mabasi Ubungo, Soko la Samaki Feri, Hospitali ya Taifa Muhimbili na Kibaha. Vituo hivi vitawezesha usambazaji wa gesi viwandani, kwenye magari na majumbani katika maeneo husika.

116. Mheshimiwa Spika, kazi zilizoteklezwa mwaka 2019/20 ni pamoja na: kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya usambazaji gesi asilia (*trunk-lines*) yenye urefu wa kilomita 18 yenye uwezo wa kuunganisha zaidi ya wateja 10,000 wa majumbani katika Mkoa wa Dar es Salaam katika maeneo ya Sinza, Mlalakuwa, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Ubungo Msewe na nyumba za Polisi Kurasini. Hadi kufikia Aprili, 2020, jumla ya wateja wapatao 500 wa majumbani na viwanda 48 vimeunganishwa na gesi asilia. Vilevile, magari zaidi ya 400 yametumia gesi asilia hadi futi za ujazo milioni 11.1 kwa mwaka 2019 kutoka futi za ujazo milioni 1.9 kwa mwaka 2018, kiasi hiki ni **ongezeko la asilimia 500** ya matumizi ya gesi kwenye magari kulinganisha na mwaka 2018. Katika eneo la Mkuranga mkoani Pwani, miundombinu yenye urefu wa kilomita 6 yenye uwezo wa kuunganisha viwanda zaidi ya 20 imejengwa.

117. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mradi wa CNG, maeneo yatakapo jengwa miundombinu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Soko la Samaki Feri,

Muhimbili na Kibaha yamepatikana; Usanifu wa kina wa kihandisi pamoja na Tathmini ya Athari kwa Mazingira vinaendelea. Mpango wa Serikali ni kuhakikisha mikoa mingi inanufaika na gesi asilia iliyogunduliwa Tanzania. Kwa kuanzia, TPDC ina mpango wa kusambaza gesi kwa kutumia CNG, Mini LNG na mabomba kwa mikoa ya Morogoro, Dodoma, Tanga, Arusha, Mwanza, Shinyanga, Kagera, Manyara, Geita na Kilimanjaro.

118. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/21, kazi zilizopangwa kufanyika katika Mkao wa Pwani ni pamoja na: kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira; na kumpata Mkandarasi (*EPC contractor*) kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya usambazaji katika maeneo ya Mwanambaya na Mkiu. Vilevile, kazi nyingine zilizopangwa kufanyika katika Mkao wa Dar es Salaam ni pamoja na kulipa fidia ya kutwaa ardhi kwa ajili ya maeneo yatakayowekwa mradi wa CNG katika maeneo ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; kufanya Tathmini za Athari kwa Mazingira katika mkuza wa miundombinu pamoja na ujenzi wa bomba kutoka Mwenge hadi Mbezi Beach na kutoka Tegeta (Wazo Hills) hadi Bagamoyo. Serikali imetenga **Shilingi bilioni 1.1** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

(ii) *Usambazaji wa Gesi Asilia Mkoani Lindi na Mtwara*

119. Serikali kupitia TPDC inaendelea na kazi za kusambaza gesi asilia kwa wateja wote walio karibu na miundombinu ya usambazaji katika Mikoa ya Mtwara na Lindi. Kazi zilizotekeliza mwaka 2019/20 ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya usambazaji gesi asilia (*trunk-lines*) yenye urefu wa Kilomita 17 yenye uwezo wa kuunganisha zaidi ya wateja 3,000 kwa Mkao wa Mtwara katika maeneo ya Chuo cha Ufundı, Chuo cha Ualimu Mtwara, Sekondari ya Ufundı na Gereza la Lilungu na Mitaa ya Magomeni, Shangani, Reli, Chikongola na Tandika. Hadi sasa, nyumba 425 zimefikiwa na miundombinu

ya usambazaji wa gesi asilia na uunganishaji unaendelea.

120. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/21, kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na: kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira katika mikoa ya Lindi na Mtwara; kumpata Mkandarasi (EPC *contractor*) kwa ajili ya ujenzi wa bomba lenye urefu wa Kilomita 7.8 kutoka kwenye bomba la usafirishaji gesi asilia hadi Mnazi Mmoja – Lindi; ununuzi wa Mtambo wa kupima kiwango cha gesi, kupunguza msukumo na kuweka harufu kwa ajili ya usalama (*Metering Pressure Reduction System and Odorization unit*); Mradi huu unalenga kujenga miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia katika Manispaa ya Lindi kuitia Mnazi Mmoja ambapo takriban wateja wa awali zaidi ya 1,000 wataunganishwa. **Shilingi billioni 10.1** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

(iii) Mradi wa Kusafirisha Gesi Asilia kutoka Tanzania kwenda Uganda

121. Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusu ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Tanzania hadi Uganda, ambao utasambaza gesi asilia maeneo ya Tanzania yatakayopitiwa na bomba hilo. Katika mwaka 2019/20, kazi zilizotekelawa ni pamoja: kuandaliwa kwa rasimu ya taratibu na kanuni za manunuzi; kukamilika kwa *Expression of Interest (EOI)* kwa ajili ya kumpata Mshauri Mwelekezi wa kufanya Upembuzi Yakinifu wa mradi; kuandaliwa kwa kanuni zitakazoongoza Kamati ya Pamoja ya Wataalamu; na kuandaliwa kwa rasimu ya Makubaliano ya Pamoja (*Bilateral Agreement*) kati ya Serikali ya Tanzania na Uganda.

122. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2020/21 kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na: kukamilisha kanuni na taratibu za manunuzi; kumpata Mshauri Mwelekezi wa kufanya upembuzi yakinifu; na kufanya

tafiti nyingine kwa ajili ya mradi. Jumla ya **Shilingi milioni 355.4** zimetengwa ili kutekeleza kazi hizo.

MRADI WA KUCHAKATA NA KUSINDIKA GESI ASILIA (*Liquefied Natural Gas - LNG*)

123. Mheshimiwa Spika, mradi huu unalenga kusindika gesi asilia iliyogunduliwa katika eneo la kina kirefu cha bahari katika Vitalu Na. 1, 2 na 4 kuwa kimiminika ili iuzwe nje ya nchi na nyingine itumike ndani ya nchi. Kazi zilizotekelawa kwa mwaka 2019/20 ni pamoja na: kuendelea kwa tafiti za namna ya kuzalisha na kusafirisha gesi kutoka bahari kuu hadi eneo la mradi; kuendelea na majadiliano ya Mikataba Hodhi (*Host Government Agreement - HGA*) baina ya Serikali na Kampuni za utafutaji na uendelezaji zitakazotekelawa mradi na ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi. Jumla ya **shilingi bilioni 5.2** zimeanza kulipwa kuanzia mwezi Mei 2020 kwa wananchi wapatao 693 watakaopisha mradi. Katika mwaka 2020/21, kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na: kuendelea na tafiti mbalimbali za kitaalam na kuendelea na majadiliano ya mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 2.6** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

UTEKELEZAJI WA MPANGO KABAMBE WA MATUMIZI YA GESI ASILIA (NATURAL GAS UTILIZATION MASTER PLAN – NGUMP)

124. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Matumizi ya Gesi Asilia (NGUMP) ambao unatoa mwongozo kuhusu matumizi bora ya gesi asilia, uboreshaji wa miundombinu ya gesi asilia pamoja na kuweka misingi ya kuhakikisha Sekta zote za uchumi zinanufaika na matumizi ya gesi asilia. Katika Mpango huo, jumla ya **Futi za Ujazo Trilioni 18.7** za gesi asilia zimepangwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya soko la ndani katika uzalishaji umeme, viwandani, kuzalisha mbolea, majumbani, taasisi na magari.

125. Mheshimiwa Spika, katika kufanikisha utekelezaji wa NGUMP, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Japan kupitia JICA imeanzisha stadi za Mpango wa Kuhamasisha Matumizi ya Gesi Asilia Nchini (DNGPP). Mpango huo umeainisha matumizi ya teknolojia nafuu katika usambazaji wa gesi asilia hususan katika maeneo ambayo soko la gesi asilia bado ni changa. Teknolojia nafuu inayopendekezwa ni pamoja na matumizi ya gesi kimiminika iliyosindikwa na gesi iliyoshindiliwa (Mini-LNG & CNG) katika kusambaza gesi asilia maeneo mbalimbali nchini.

126. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2019/20 kazi zilizotekelawa ni pamoja na: kuandaa Rasimu ya Mpango wa Kuhamasisha Matumizi ya Gesi Asilia Nchini (*Draft Domestic Natural Gas Promotion Plan – DNGPP*), uhakiki wa awali wa mahitaji ya gesi asilia nchini; uchambuzi wa awali wa kiuchumi na kiufundi wa teknolojia mbalimbali za usafirishaji na usambazaji wa gesi asilia; pamoja na uchambuzi wa awali wa Mradi wa mfano wa usambazaji gesi asilia katika Jiji la Dodoma.

127. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/21 kazi zitakazotekelawa ni pamoja na: kufanya upembuzi yakinifu wa kina wa teknolojia zilizopendekezwa kwenye Mpango wa DNGPP; kuhakiki mahitaji ya gesi asilia nchini na kuhamasisha matumizi ya gesi asilia katika maeneo mbalimbali nchini; na kuanza hatua za awali za utekelezaji Mradi wa Mfano katika Jiji la Dodoma.

MIRADI YA KUHIFADHI NA KUSAFIRISHA MAFUTA

(i) Uhifadhi na Biashara ya Mafuta

128. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na taratibu za uanzishaji na usimamizi wa Hifadhi ya Kimkakati ya Mafuta ya Akiba ya Dharura na kushiriki katika biashara ya kuagiza na kuuza mafuta. Kazi zilizotekelawa kwa mwaka 2019/20 ni pamoja na:

kukamilika kwa stadi za biashara ya mafuta; kukamilika kwa usajili ili kuanza kuagiza mafuta; na kuanza taratibu za kutwaa maeneo ya kimkakati katika mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Morogoro na Dodoma.

129. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/21, kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na: kuendelea na utwaaji wa maeneo yaliyoainishwa, kuanza biashara ya mafuta na kulipa gharama mbalimbali za uendeshaji. Serikali kupitia TPDC imetenga **Shilingi bilioni 31.2** kutekeleza kazi hizo.

(ii) Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Uganda hadi Tanzania (East African Crude Oil Pipeline)

130. Mheshimiwa Spika, mradi huu unahusu ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi (*crude oil*) kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania). Katika kipindi cha mwaka 2019/20 kazi zilizotekeliza ni pamoja na: kukamilika kwa kazi ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira; na kuendelea na utoaji wa elimu kwa umma kwa maeneo ya pembezoni mwa eneo la mradi.

131. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2020/21 kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na: kukamilisha majadiliano ya mikataba ikiwemo ya Nchi Hodhi na Wawekezaji (HGA), Mkataba wa Ubia (SHA), Mkataba wa Bandari, Mkataba wa Pango la Ardhi (*Land Lease Agreement*) na kulipa fidia. Jumla ya **Shilingi bilioni 1** zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo. Mradi unatarajiwa kuanza mwezi Aprili, 2021 baada ya kufanyika kwa Maamuzi ya Mwisho ya Uwekezaji (*Final Investment Decision – FID*)

(iii) Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Safi (Refined Petroleum Products) kutoka Dar es Salaam (Tanzania) hadi Ndola (Zambia)

132. Mheshimiwa Spika, mradi huu umepangwa kutekelezwa kwa ushirikiano wa Serikali za Tanzania

na Zambia. Mradi unahusu ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta safi kutoka Dar es salaam (Tanzania) hadi Ndola (Zambia) likiwa na matoleo ya mafuta (*take-off points*) katika maeneo ya Morogoro, Iringa, Njombe, Mbeya na Songwe. Mradi huu utaiwezesha Serikali kuongeza mapato, ajira, kuongeza uhakika wa upatikanaji wa mafuta katika maeneo linapopita bomba, pamoja na kuepusha uharibifu wa miundombinu ya barabara, kupunguza gharama za usafirishaji wa mafuta na kupunguza msongamano wa magari jijini Dar es Salaam. Mradi utaongeza fursa za biashara katika ukanda wa nyanda za juu kusini.

133. Mheshimiwa Spika, kazi zilizotekelawa ni pamoja na: kukamilika kwa andiko la awali la mradi; Hadidu za Rejea za Upembuzi Yakinifu na Athari kwa Mazingira na Kijamii pamoja na kupata ridhaa ya kufanya kwa Upembuzi Yakinifu.

134. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2020/21, kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja kuendelea kukamilisha kumpata Mshauri Mwelekezi wa kufanya Upembuzi Yakinifu. Jumla ya **Shilingi milioni 500** zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo.

UDHIBITI WA SHUGHULI ZA MKONDO WA JUU WA MAFUTA NA GESI ASILIA

135. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu la kudhibiti shughuli za mkondo wa juu wa petroli kwa mwaka 2019/20, Serikali kuitia PURA imepitisha Mpango Kazi wa uchorongaji wa visima vinne (4) na uchukuaji wa data za mitetemo za 2D kilomita 450 za mstari na za 3D kilomita 717 za mraba. Aidha, PURA ilisimamia uchorongaji wa visima viwili vifupi (*stratigraphic boreholes*) katika maeneo ya Kining'inila na Nyaranja - Kitalu cha Eyasi Wembere. PURA imekamilisha ukaguzi na uhakiki wa gharama za uwekezaji, na mapato yatokanayo na uzalishaji wa

gesi asilia kwa mwaka 2016 hadi 2018 na kuokoa zaidi ya **Shilingi Bilioni 10.14** ambazo mwekezaji aliziveka kama gharama za uwekezaji. Hatua hii imepelekea kuongezeka kwa pato la Serikali katika mgao wake wa uuzaaji gesi asilia.

136. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/21, Serikali kupitia PURA itaendelea kusimamia na kudhibiti shughuli za mkondo wa juu wa petroli. Shughuli hizo ni pamoja na: uchorongaji wa kisima kimoja (1) cha utafutaji (Chikumbi-1) katika kitalu cha Ruvuma; visima viwili (2) vya utafutaji (Mruka-1 na Mtarawanda- 1), kisima kimoja (1) cha uendelezaji (Mambakofi- 2) katika kitalu cha Ruvu; na uchorongaji wa visima vya utafutaji na uhakiki katika kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini. Kwa mwaka 2020/21, Jumla ya **Shilingi bilioni 1.69** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza majukumu hayo.

HALI YA UAGIZAJI NA UPATIKANAJI WA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI NCHINI

137. Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (*Bulk Procurement System - BPS*) unaosimamiwa na Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (*PBPA*) umeendelea kutumika kuagiza mafuta ya petroli, dizeli, mafuta ya taa na mafuta ya ndege. Katika mwaka 2019 jumla ya lita **bilioni 6.15** zilliingizwa nchini ikilinganishwa na lita **bilioni 5.70** zilizoagizwa mwaka 2018 sawa na ongezeko la **asilimia 7.4**. Kati ya kiasi hicho, lita **bilioni 3.54** sawa na **asilimia 57.5** ya mafuta yote yaliyoagizwa yalikuwa ni mafuta kwa ajili ya matumizi ya hapa nchini na lita **bilioni 2.62**, sawa na **asilimia 42.5** yalikuwa kwa ajili ya kusafirishwa kwenda nchi jirani.

138. Mheshimiwa Spika, muda wa kupakua mafuta kutoka kwenye meli umepungua kutoka wastani wa siku 30 hadi 60 kabla ya mwaka 2015 na kufikia wastani wa siku 1 hadi 3 kwa mwaka 2020. Aidha, kiasi cha mafuta ya ziada kimeongezeka kutoka lita milioni 185

mwaka 2018 hadi lita milioni 365 mwaka 2019 sawa na **ongezeko la asilimia 97.3**. Mafuta haya yanatosheleza wastani wa matumizi ya zaidi ya siku 40 kwa kila aina ya mafuta.

139. Mheshimiwa Spika, kiasi cha gesi ya mitungi (*Liquefied Petroleum Gas - LPG*) kilichoingizwa nchini kimeendelea kuongezeka ambapo kwa mwaka 2019 kilifikia **tani 166,436** ikilinganishwa na **tani 142,940** mwaka 2018 sawa na ongezeko la **asilimia 16.4**. Aidha, matumizi ya gesi hiyo nchini yameendelea kuongezeka ambapo kwa mwaka 2019 yalifikia **tani 106,301** ikilinganishwa na **tani 92,492** mwaka 2018 sawa na ongezeko la **asilimia 15**. Ongezeko hilo limechangiwa na juhudhi mbalimbali za Serikali kwa kushirikiana na Kampuni zinazouza LPG katika kuelimisha Jamii juu ya umuhimu wa kutumia LPG katika kutunza mazingira na kupunguza madhara ya kiafyah yanayotokana na matumizi ya kuni na mkaa.

MWENENDO WA BEI ZA MAFUTA

140. Mheshimiwa Spika, bei za mafuta katika soko la Dunia zimeendelea kushuka kutoptoka na sababu mbalimbali ikiwemo uhitaji na upatikanaji wa bidhaa hii muhimu katika shughuli za kiuchumi. Wastani wa bei ya mafuta ghafi katika soko la dunia katika mwezi Aprili, 2020 ilifikia Dola za Marekani 23.27 kutoka Dola za Marekani 60.39 kwa pipa mwaka 2019 sawa na punguzo la asilimia 61.5.

141. Mheshimiwa Spika, kushuka kwa bei ya mafuta ghafi katika soko la Dunia kumesababisha kushuka kwa bei ya mafuta yaliyosafishwa ambapo wastani wa bei ya mafuta yaliyosafishwa katika soko la dunia ilikuwa **Dola za Marekani 593, 578** na **612** kwa tani kwa mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa/ndege mtawalia, ikilinganishwa na wastani wa **Dola za Marekani 646, 606** na **575** kwa tani kwa kipindi kama hicho mwaka 2018. Hii ni sawa na pungufu ya **asilimia**

8 na **asilimia 5** kwa mafuta ya petroli na dizeli mtawalia. Aidha, bei ya mafuta ya taa/ndege imeongezeka kwa **asilimia 6**.

142. Mheshimiwa Spika, kutokana na kushuka kwa bei ya mafuta ya petroli na dizeli katika soko la Dunia, bei za mafuta haya katika soko la ndani pia zilishuka. Kwa mwaka 2019, wastani wa bei za mafuta katika soko la ndani kwa mafuta yaliyopokelewa kupitia bandari ya Dar es Salaam ilishuka ikililinganishwa na wastani wa bei za mafuta katika kipindi hicho mwaka 2018. Wastani wa bei za mafuta kwa Mkoa wa Dar es Salaam kwa mwaka 2019 kwa lita moja ilikuwa kama ifuatavyo: Petroli **Shilingi 2,200**, Dizeli **Shilingi 2,159** na Mafuta ya Taa **Shilingi 2,114** wakati wastani wa bei za mafuta hayo kwa mwaka 2018 ilikuwa **Shilingi 2,318** mafuta ya Petroli, **Shilingi 2,229** kwa mafuta ya Dizeli na **Shilingi 2,188** kwa Mafuta ya Taa ambazo ni sawa na punguzo la **asilimia 5, 3 na 3** mtawalia. Aidha, kwa wakati wote bei ya Mafuta ya Ndege hapa nchini ni sawa na bei ya mafuta ya taa kabla ya kodi na tozo za Serikali.

UDHIBITI WA UBORA WA MIUNDOMBINU NA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI NA GESI ASILIA

143. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia EWURA imeendelea kusimamia na kuhakikisha miundombinu ya mafuta inajengwa na kuendeshwa kwa kuzingatia viwango stahiki. EWURA pia imeendelea kutoa leseni kwa miundombinu ambayo inakidhi viwango ambapo katika kipindi cha Januari 2019 hadi Machi, 2020, imetoa jumla ya leseni 570 za aina mbalimbali na vibali 197 vya ujenzi wa miundombinu ya mafuta. Aidha, EWURA imetoa kibali kwa Kampuni ya Dangote- Mtwara kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kujaza gesi asilia iliyyoshindiliwa kwenye magari (*Compressed Natural Gas*) ili kuyawezesha magari ya kampuni hiyo kutumia gesi asilia.

144. Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa mafuta vijijini umeendelea kusimamiwa na kuzipatia ufumbuzi changamoto zilizopo kutokana na uhaba wa vituo vya mafuta katika maeneo hayo. Katika mwaka 2019/20, Serikali imeandaa utaratibu utakaorahisisha uwekezaji katika vituo vya mafuta ambao utapunguza gharama za uwekezaji kwa vituo vya mafuta vijijini ili mafuta yaweze kusambazwa katika njia bora na salama. Vilevile, Serikali inaandaa utaratibu utakaorahisisha usambazaji wa gesi asilia na LPG kwa maeneo ya vijijini. Taratibu hizo zinatarajia kukamilika mwezi Juni, 2020.

145. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia EWURA imeendelea kusimamia ubora wa bidhaa za mafuta ya petroli zinazosambazwa na kuuzwa nchini. Katika kipindi cha mwaka 2019, EWURA ilipima sampuli 280 ambapo kati hizo, sampuli 30 sawa na **asilimia 10.3** hazikukidhi viwango na hatua stahiki za kisheria zilichukuliwa dhidi ya wafanyabiashara waliokutwa na mafuta ambayo hayakidhi viwango.

146. Mheshimiwa Spika, njia nyingine inayotumika kudhibiti ubora na ukwepaji wa kodi katika biashara ya mafuta ni uwekaji wa vinasaba (*molecular marker*) katika mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa yanayotumika hapa nchini. Utaratibu huu umesaidia kudhibiti uchakachuaji, ukwepaji wa kodi na kuimarisha ushindani katika biashara ya mafuta. Katika mwaka 2019, EWURA ilipima vinasaba kwenye mafuta kutoka katika vituo vya mafuta 718 na kati ya vituo hivyo, vituo 23 sawa na **asilimia 3.2** vilikutwa na mafuta ambayo hayakuwa na kiwango sahihi cha vinasaba kwa mujibu wa kanuni. Hatua stahiki zilichukuliwa dhidi ya wafanyabiashara ambao mafuta yao hayakuwa na kiwango sahihi cha vinasaba ikiwemo kutozwa faini na kufikishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa ajili ya kulipa kodi stahiki walizokwepa.

147. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/21 Serikali itaendelea kusimamia sekta ya mafuta nchini ili kuhakikisha uwepo wa mafuta ya kutosha, yenye ubora stahiki, miundombinu ya mafuta yenye kukidhi ubora, usalama na utunzaji wa mazingira pamoja na ushindani ulio sawa wakati wote.

MIRADI YA KUJENGA UWEZO KATIKA SEKTA NDOGO YA MAFUTA NA GESI ASILIA

(i) Mradi wa Usimamizi wa Rasilimali za Ndani na Usimamizi wa Rasilimali za Asili Tanzania

148. Mheshimiwa Spika, Mradi huu ulianza kutekelezwa kuanzia mwezi Juni, 2017 na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2021. Gharama za mradi ni kiasi cha **Dola za Marekani milioni 29.54** ambapo Mfuko wa Maendeleo wa Afrika unachangia **Dola za Marekani milioni 26.59** sawa na **Shilingi bilioni 62.08** na Serikali ya Tanzania itachangia **Dola za Marekani milioni 2.95** sawa na **Shilingi bilioni 6.90**.

149. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/20 kazi zilizotekelawa ni pamoja na: ununuzi na kuanza ufungwaji wa skana ya kukagulia mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam; kukamilika kwa awamu ya kwanza ya uboreshaji wa mfumo wa kielectroniki wa uondoaji wa shehena bandarini na katika mipaka (*Electronic Single Window System*); kukamilika kwa ununuzi na ufungwaji wa mifumo ya ukusanyaji mapato; na kukamilisha ununuzi na ufungaji wa vifaa vyya kuhifadhi data za petroli.

150. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/21 kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na: kukamilisha ufungwaji na kuanza kutumika skana ya kukagulia mizigo; kukamilisha awamu ya pili ya uboreshaji wa mfumo wa kielectroniki wa uondoaji wa shehena bandarini na mipakani; na kukamilisha stadi za: mifumo ya bei ya gesi asilia, mchango wa sekta ya

gesi asilia kwenye uchumi, mahitaji ya gesi asilia nchini; pamoja na uanzishwaji wa kituo cha utunzaji taarifa za mkondo wa juu (*data centre*) cha PURA. Jumla ya **Shilingi bilioni 25.8** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizi.

(ii) Mradi wa Oil For Development Programme (OfD) - Institutional Cooperation In the Upstream Petroleum Sub-Sector

151. Mheshimiwa Spika, mradi huu una lengo la kujengea uwezo Wizara na Taasisi za Serikali zinazohusika na masuala ya usimamizi wa mafuta na gesi asilia nchini ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi. Wanufaika wa mradi huu ni pamoja na Wizara ya Nishati, Wizara ya Fedha na Mipango, PURA, TPDC, TRA, NEMC, TASAC na OSHA kwa upande wa Tanzania Bara. Kwa upande wa Zanzibar ni, Wizara ya Ardhi, Maji, Nyumba na Nishati; ZPRA; ZPDC; ZEMA; ZMA; na DOSH. Pamoja na kuzijengea uwezo Wizara na Taasisi husika, Mradi huu pia unasaidia katika kuandaa kanuni na miongozo mbalimbali itakayoimarisha usimamizi katika sekta ya mafuta na gesi asilia. Mradi ulianza kutekelezwa mwaka 2017 na utakamilika Julai, 2020.

152. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/20 kazi zilizotekelawa ni pamoja na kuwajengea uwezo maafisa 61 kutoka taasisi husika katika maeneo ya utunzaji wa takwimu, masuala ya mazingira na usalama mahala pa kazi pamoja na usimamizi wa mapato yatokanayo na shughuli za mafuta na gesi asilia.

USHIRIKI WA WATANZANIA KATIKA SEKTA NDOGO YA MAFUTA NA GESI ASILIA

153. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha Watanzania wanashiriki kikamilifu katika shughuli za mafuta na gesi asilia nchini. Mwaka 2018 Serikali

ilianzisha Kanzidata ya Watoa Huduma wa Ndani (*Local Suppliers and Service Providers Database - LSSP*). Hadi mwezi Aprili, 2020, jumla ya Kampuni za Watanzania na zile za ubia 457 zimesajiliwa kwenye Kanzidata hiyo.

UIMARISHAJI WA MAWASILIANO KATI YA WIZARA NA JAMII

154. *Mheshimiwa Spika*, pamoja na majukumu mengine, Wizara imeendelea na kazi ya utoaji taarifa kwa wadau kupitia Televisheni, Magazeti na Redio. Aidha, utoaji wa taarifa unajumuisha kupitia Tovuti ya Wizara, mitandao ya kijamii ya Wizara ambayo ni *facebook, Twitter, Instagram* na YouTube pamoja na Jarida la Wizara ya Nishati linalotolewa kila mwezi.

155. *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka 2019/20 Wizara iliendelea kutoa taarifa mbalimbali za miradi mikubwa inayotekelawa chini yake ikiwemo miradi ya uzalishaji na usafirishaji umeme, miradi ya mafuta na usambazaji wa gesi asilia na miradi ya usambazaji umeme vijijini. Katika mwaka 2020/21 Wizara itaendelea kutoa taarifa mbalimbali katika maeneo muhimu ya miradi mikubwa inayotekelawa chini ya Wizara.

AJIRA NA MAENDELEO YA RASILIMALIWATU

156. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kusimamia maendeleo ya Watumishi wake pamoja na kutekeleza vema Muundo wake ulioidhinishwa mwaka 2018 kwa kujaza jumla ya nafasi 7 za Uongozi zilizokuwa wazi. Katika mwaka 2020/21 Wizara inatarajia kuwapandisha vyeo Watumishi 67, kuajiri Watumishi 14 na kujaza nafasi 3 za uteuzi. Vilevile, jumla ya watumishi 58 wamepangwa kuajiriwa katika Taasisi zilizo chini ya Wizara kama ifuatavyo: TPDC (25), REA (10), PURA (8) na PBPA (15).

157. Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa kuwawezesha na kuwajengea uwezo Watanzania katika masuala mbalimbali ya mafuta na gesi asilia, Wizara imeendelea kushirikiana na Washirika wa Maendeleo kwa kuwapatia ufadhili wa masomo Watanzania katika Shahada ya Kwanza, Uzamili na Uzamivu ili kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na wataalamu wa kutosha katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia. Vilevile, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo wataalam kupitia Mpango wa Uendelezaji wa Rasilimaliwa wa Wizara. Katika mwaka 2019/20, Watanzania 17 walipatiwa fursa ya ufadhili wa masomo kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China katika fani ya mafuta na gesi asilia. Wizara pia iliwajengea uwezo watumishi 9 na watumishi 104 katika mafunzo mbalimbali ya muda mrefu na muda mfupi mtawalla.

158. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/21, Watanzania 20 wanatarajiwa kwenda masomoni kupitia ufadhili wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China katika fani ya mafuta na gesi asilia. Aidha, Wizara itawezesha ufadhili wa mafunzo ya muda mrefu kwa Watumishi 12 na mafunzo ya muda mfupi kwa Watumishi 63.

USHIRIKIANO WA KIKANDA NA KIMATAIFA

159. Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Serikali napenda kuwashukuru Washirika wa Maendeleo na nchi wahisani ambao wameendelea kutoa michango yao katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara. Napenda kutambua mchango wa: Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), Benki ya Ushirikiano wa Kimataifa ya Japan (JBIC), United Bank for Africa (UBA); Economic Development Cooperation Fund (EDCF - Korea), Mfuko wa Uendelezaji Jotoardhi (Geothermal Risk Mitigation Facility - GRMF) pamoja na Taasisi na Mashirika ya: JICA (Japan), KfW (Germany), AFD

(Ufaransa), Sida (Sweden), NORAD (Norway); Umoja wa Ulaya (EU), Benki ya Exim (China), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Maendeleo la Canada (CIDA) na USAID (Marekani).

160. Mheshimiwa Spika, pia natoa shukrani kwa Serikali za Nchi za Burundi, Canada, China, Iceland, Japan, Kenya, Norway, Uingereza, Sweden, Marekani, Urusi, Afrika Kusini, Korea ya Kusini, Malawi, Misri, Msumbiji, Sweden, Rwanda, Ufaransa, Uganda na Zambia kwa ushirikiano wao katika kuendeleza Sekta ya Nishati. Vilevile, nishukuru Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kwa ushirikiano katika masuala ya kikanda yanayohusu Sekta hii. Kwa kipindi cha mwaka 2020/21, *Serikali kupitia Wizara ya Nishati itaendelea kuimarisha ushirikiano na Washirika wa maendeleo na wadau wengine ili kuhakikisha kuwa Sekta ya Nishati inachangia katika kutimiza azma ya Serikali ya kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.*

HITIMISHO

161. Mheshimiwa Spika, kupitia Bajeti ya Mwaka 2020/21 Wizara inalenga kutekeleza dhamira ya Serikali ya kuhakikisha kuwa inazalisha umeme wa kutosha, wa uhakika, na wa gharama nafuu. Vilevile, bajeti imelenga kuimarisha shughuli za utafutaji na biashara ya mafuta na gesi asilia pamoja na kuwezesha wananchi kunufaika na rasilimali hizo.

162. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/21, Wizara ya Nishati inakadiria kutumia jumla ya **Shilingi trilioni 2.197** ikilinganishwa na **Shilingi trilioni 2.142** iliyotengwa kwa Mwaka 2019/20, sawa na ongezeko la **asilimia 2.5**.

163. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa liidhinishe bajeti ya jumla ya **Shilingi 2,196,836,774,000** kwa ajili ya matumizi ya

Wizara ya Nishati na Taasisi zake. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:

(i) **Shilingi 2,168,437,184,000** sawa na **asilimia 98.7** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo za maendeleo, **Shilingi 1,967,689,292,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 200,747,892,000** ni fedha za nje; na

(ii) **Shilingi 28,399,590,000** sawa na **asilimia 1.3** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 15,025,821,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **Shilingi 13,373,769,000** kwa ajili ya mishahara (PE) ya watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake.

164. Mheshimiwa Spika, kwa unyenyeketu mkubwa sana naomba tena nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuniskiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anuani ya www.nishati.go.tz. Vilevile, Hotuba hii ina vielelezo mbalimbali ambavyo vimeambatishwa kwa ajili ya ufanuzi wa masuala muhimu yanayohusu Sekta ya Nishati.

165. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa tutaendelea na utaratibu wetu. Namwita MwenyeKITI wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Dunstan Kitandula.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGESA YA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezei Mungu kwa kutujalia afya njema na uhai katika kuiona siku ya Leo. Nami naomba niungane na Wabunge

wenzangu katika kutoa pole kwa familia zote ambazo zimepoteza pendwa wao katika kipindi hiki. Mwenyezi Mungu awajalie pumziko la amani ndugu zetu waliotangulia mbele za haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kukupongeza wewe, Mheshimiwa Spika na Wenyeziti wote wa Bunge kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuliongoza Bunge hili. Mungu awajalie afya njema, hekima na busara katika kuendelea kutekeleza wajibu huu mkubwa tuliowakabidhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini kwa Waziri wa Nishati - Mheshimiwa Dkt. Medard Matogolo Kalemani, Mheshimiwa Subira Khamis Mgali - Naibu Waziri wa Nishati pamoja na Katibu Mkuu, dada yangu Eng. Zena na Watendaji wote katika Wizara hii kwa kusimamia vyema shughuli za Wizara na kwa ushirikiano wao mkubwa kwa Kamati yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa namna ya pekee naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa umakini wao mkubwa waliouonesha wakati wote wa kutekeleza majukumu ya Kamati. Kwa heshima kubwa naomba majina yao yaingie katika kumbukumbu rasmi za Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, naomba kumshukuru Katibu wa Bunge pamoja na wasaidizi wake wote ikiwemo Makatibu wetu wa Kamati, Ndugu Felister Mgonja na Ndugu Herman Berege kwa ushirikiano na mratibu mzuri wa shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha taarifa hii kwa wakati. kwa sababu ya muda sitawenza kusoma taarifa yote, hivyo naomba taarifa hii kama ilivyowasilishwa mezani kwako iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati (Fungu 58) kwa

mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 98(1) na 98(2) ya Kanuni za Bunge Toleo la Januari, 2016, Kamati ilifanya kazi zifuatatazo: kwanza, ilitembelea na kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2019/2020, lakini vile vile ilifanya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Maelezo kuhusu ukaguzi wa miradi ya maendeleo, changamoto zilizobainika yanaonekana katika ukurasa wa pili hadi 12 wa taarifa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijielekeze hali ya Upatikanaji wa mafuta nchini. Kamati illichambua taarifa kuhusu hali ya upatikanaji wa mafuta nchini na kubaini kuwa kwa kipindi chote cha Julai, 2019 hadi Februari, 2020 hali ya upatikanaji wa mafuta nchini ilikuwa nzuri ambapo nchi ilikuwa na akiba ya mafuta ya kutosha kwa wastani wa zaidi ya siku 40 kwa kila aina ya mafuta wakati wote. Hili ni ongezeko la asilimia 55 ikilinganishwa na siku 15 za akiba ya mafuta zinazotakiwa kwa mujibu wa kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeridhishwa na hali ya upatikanaji wa mafuta hapa nchini pamoja na usimamizi mzuri wa uagizaji wa mafuta unaofanywa na Wizara kupitia Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja kwa kushirikiana na mamlaka nyingine. Ni matumaini ya Kamati kuwa Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa pamoja utaendelea kusimamia Sekta ya Mafuta kwa ufanisi kwa manufaa ya uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati inatumaini kuwa Wakala utaendelea kushirikiana na wadau wengine kwa lengo la kuendelea kuimarisha mfumo wa uagizaji wa mafuta nchini hususan katika kipindi hiki ambapo ulimwengu unakabiliwa na changamoto kubwa ya ugonjwa wa Homa ya Mapafu, changamoto ambayo Taasisi mbalimbali za

Utafiti za Kimataifa kama *IMF*, *World Bank*, *UNECA* na nyinginezo zinatabiri kutokea kwa m dororo wa uchumi ulimwenguni utakaoathiri shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari ulimwengu umeanza kushuhudia Sekta za Usafiri wa Anga na Utalii kusimama, biashara na uzalishaji viwandani kushuka na hivyo kushuka kwa kiasi kikubwa kwa matumizi ya mafuta. Kufuatia kushuka kwa matumizi ya mafuta ulimwenguni, tumeshuhudia vilevile katika siku za hivi karibuni bei ya mafuta katika Soko la Kimataifa kushuka kwa kiwango ambacho hakijawahi kushuhudiwa. Hivyo basi, kufuatia mkanganyiko huu na mwenendo usiotabirika wa Soko la Mafuta Ulimwenguni, ipo haja kwa nchi yetu kuweka mikakati thabiti ya kuhakikisha nchi inakuwa na akiba ya mafuta ya kutosha wakati wote.

Aidha, Serikali itumie mwanya huu wa m dororo wa bei ya mafuta ulimwenguni kuzungumza na nchi rafiki zinazozalisha mafuta ili kama nchi tuweze kupata mafuta kwa masharti nafuu na kuitia *TPDC* tuweze kuanzisha hifadhi ya mafuta ya kimkakati kwa ajili ya kuhami uchumi wetu katika siku zijazo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze katika hali ya upatikanaji umeme nchini. Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada kubwa zinazofanyika katika kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na umeme wa kutosha, wenye uhakika na unaotabirika wakati wote kutoka katika vyanzo mchanganyiko kwa kushirikisha wazalishaji wadogo ili kulinda uwekezaji ambao tayari wazalishaji wadogo wa umeme wameufanya na hivyo kuweza kuhudumia zaidi ya wateja 100,000 hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ili kuendelea kujenga imani kwa wawekezaji kuwa mazingira ya ufanyaji biashara hapa nchini yanatabirika, Kamati inaona ipo haja kwa Serikali kuharakisha mchakato wa kutafuta suluhu ya mkanganyiko wa bei ya kuuzia umeme unaozalishwa na wazalishaji wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yako ilichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Umeme Vijijiini (*REA*) na kufanya tathmini ya namna ya utekelezaji wake. Hadi kufikia tarehe 26 Machi, 2020 jumla ya fedha shilingi bilioni 457 sawa na asilimia 53 za gharama nzima ya mradi kwa upande wa fedha za ndani na USD milioni 80.92 sawa na asilimia 77 ya gharama nzima ya mradi kwa upande wa fedha za kigeni, zimelipwa kwa Wakandarasi kwa ajili ya kazi za mradi pamoja na ununuzi wa vifaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilibaini kuwa hali ya utekelezaji wa mradi wa umeme unaridhisha. Kamati pia inaona ipo haja ya Wakandarasi kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi hii. Aidha, Serikali inapaswa kuendelea kuweka nguvu ya kusimamia na kufuatilia Wakandarasi wanaotekeleza miradi ili kuhakikisha kuwa miradi hii inakamilika kwa wakati na kwa ubora ullokusudiwa kulingana na matakwa ya mikataba. Ipo haja vilevile kwa Serikali kupanua wigo ya utekelezaji wa miradi hii ili kuwafikia Watanzania wengi kwa wakati mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo linalofuata ni Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Uzingatiaji wa Maoni ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2019/2020, Wizara ya Nishati ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 602.05. Kati ya makusanyo hayo, jumla ya shilingi bilioni 602.04 zilitarajiwa kukusanywa kuitia shughuli za mafuta na gesi asilia na shilingi milion 12 kuitia shughuli za Utawala. Mapato haya yanatokana na vyanzo mbalimbali vikiwemo shughuli za *TPDC* za utafiti wa mafuta, mauzo ya gesi asilia na mauzo ya nyaraka za zabuni. Kamati inatoa rai kuwa Wizara iendeleze jitihada za kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali kutoka kwenye vyanzo vya mafuta na gesi asilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya upatikanaji wa fedha kutoka hazina, katika kipindi cha mwaka 2019/2020, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liliidhinisha Bajeti ya shilingi trilioni 2.14 kwa Wizara ya Nishati. Kati ya fedha hizo,

Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ni shilingi trilioni 2.116 sawa na asilimia 98 ya bajeti yote ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya fedha za ndani iliyotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni shilingi tirioni 1.956 sawa na asilimia 92 ya Bajeti yote ya Maendeleo. Shilingi bilioni 1.6 sawa na asilimia 7.6 ni fedha za nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyotengwa kwa Mwaka 2019/2020 ni shilingi bilioni 26 sawa na asilimia 1.2 ya bajeti yote ya Wizara. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 15, ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 11, kwa ajili ya kulipa mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zilizopo chini Wizara yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni rai ya Kamati kuwa mara baada ya madai husika kuwasilishwa kwa miradi inayoendelea kwa utekelezaji wake, fedha hizo ziweze kutolewa mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati. Katika uchambuzi wa Bajeti ya mwaka 2019/2020 Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 7(1). Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, sehemu kubwa ya ushauri uliotolewa na Kamati umezingatiwa na baadhi unaendelea kufanyiwa kazi. Mionganoni mwa maeneo ambayo bado utekelezaji wake unafanyiwa kazi, ni suala la miundo wezeshi ya mradi wa umeme wa Mto Rufiji hasa barabara, madaraja na makalavati. Kamati inaona ni vyema maeneo haya barabara hizi zikawa za kudumu zinazoweza kupitika wakati wote ili kuhakikisha kuwa ujenzi wa mradi unatekelezwa bila vikwazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni ulipaji fidia kwa wananchi. Kamati inaona kwamba Serikali ilipe fidia kwa wakati kwa wananchi wote wanaotoa maeneo yao kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hapa tunaomba kuipongeza sana Serikali kwa kuanza mchakato wa kulipa

takribani shilingi bilioni 5.2 kwa wananchi waliopisha utekelezaji wa mradi wa Gesi Asilia katika Mkoa wa Lindi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi, katika Mwaka 2020/2021, Wizara ya Nishati - Fungu 58 inakadiria kutumia jumla ya shilingi trillioni 2.142 ikililinganishwa na shilingi trillioni 1.142,793 zilizotengwa kwa mwaka 2019/2020 na hii sawa na ongezeko la asilimia 2.52

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa bajeti ya maendeleo, utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika mwaka 2020/2021 unakadiria kutumia jumla ya shilingi trillioni 2.168 ambazo ni sawa na asilimia 98.7 ya bajeti yote ya Wizara. Aidha, kwa upande wa Bajeti ya matumizi ya kawaida Wizara inakadiria kutumia shilingi billioni 28.399 sawa na asilimia 1.1 ya bajeti yote ya Wizara katika fedha zilizoombwaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa ukusanyaji wa maduhuli, Wizara inakadiria kukusanya jumla ya shilingi bilioni 160.622. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 160.601 zitakusanya kupitia shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia na shilingi milloni 20 zitakusanya kupitia shughuli za Utawala. Kamati inatoa angalizo kwa Serikali kuwa upo uwezekano mkubwa wa kuwepo kwa m dororo wa shughuli za uwekezaji ulimwenguni kutokana na uwepo wa janga la *Corona* hali ambayo inaweza kuathiri makisio ya makusanyo yaliyowekwa. Kwa muktadha huu, Kamati inashauri Serikali kufuatilia kwa karibu hali ya uwekezaji inavyoendelea ulimwenguni ili kufanya mapitio ya haraka kwenye mipango iliyowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Baada ya Kamati kutekeleza majukumu yake ya kinanuni ambayo ni ukaguzi wa miradi ya maendeleo na uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Kamati

ina maoni na ushauri ufuatao. Kamati imetoa jumla ya maoni 12 na kwa sababu ya muda nitasoma machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza ni utekelezaji wa Mradi wa Julius Nyerere. Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maji katika Bonde la Mto Rufiji una umuhimu wa kimkakati kwa uchumi wa Taifa letu. Na kwa kuwa katika mwaka 2019/2020 utekelezaji wake ulijiwekeza katika ujenzi wezeshi na kwamba kwa mwaka 2021 mradi unaingia katika hatua muhimu sana ya utekelezaji ikiwemo kuanza ujenzi wa bwawa, ujenzi wa njia kuu ya kupidisha maji, ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme na ujenzi wa kuzalisha kituo cha kusafirisha umeme. Kamati inatoa rai kwa Serikali kuhakikisha kuwa inaongeza usimamizi na kuhakikisha fedha za uendelezaji wa mradi zinapatikana kwa wakati kama zilivyo tengwa na kuidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni utekelezaji wa Mradi wa Kinyerezi. Kamati ilibaini kuwa mkandarasi anayetekeleza Mradi wa Kinyerezi ameshindwa kutekeleza majukumu yake ya kimkataba na kuacha mradi bila kumalizika. Kutokana na changamoto hiyo, Kamati inatoa raikwa Serikali kuhakikisha kwamba anapatikana mkandarasi mwininge wa kumalizia mradi anapatikana kwa haraka. Aidha, Serikali ifanye jitihada za makusudi kuhakikisha *subcontractors* wote ambao walikuwa wanatoa huduma kwa wakandarasi wa awali wanalipwa fedha zao kwa wakati ili kuwaepusha na hatari ya kufilisika kutokana na kupanda kwa riba za mikopo waliyochukua kwenye mabenki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya kuzalisha vifaa vya umeme hapa nchini. Uwezo wa uzalishaji wa viwanda vilivyopo unazidi mahitaji ya soko hapa nchini na kwa kuwa hata uzalishaji kwa ajili ya soko la ndani unafanyika bila wazalishaji kupata takwimu halisi za mahitaji kwa mwaka hivyo kushindwa kukadiria vyema mahitaji ya malighafi na kujipanga kwenye mzunguko wa uzalishaji. Hivyo basi, Kamati inatoa ushauri kwa Serikali kuvisaidia viwanda vyetu kutafuta

masoko nje ya nchi kwa kuweka mkakati mabsusi wa kuzishirikisha ofisi zetu za Balozi kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki na nchi za *SADC*. Kwa kufanya hivyo, siyo tu kutawezesha bidhaa za viwanda hivyo kupanya kwenye masoko ya nchi hizo bali pia itaongeza mapato ya kikodi kwa nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Kamati inaishauri *REA* na *TANESCO* kutangaza mapema mahitaji yao ya mwaka ya mashine umba ili kuwezesha viwanda hivi kujipanga na kuzalisha kwa ufanisi.

Sambamba na hili, baadhi ya malighafi muhimu za kutengeneza mashine umba *HS-code* zake kuhitaji kulipiwa *import duty* hivyo kuongeza gharama za uendeshajji na kuathiri bei ya bidhaa. Na kwa kuwa mfumo wa ukaguzi wa bidhaa bandarini huchakua muda mrefu hivyo kusababisha mali ghafi kuchelewa na viwanda kulazimika kusimamisha uzalishajji.

Vilevile kutokana na Cheti cha Mazingira kutoka *NEMC* kutopatikana kumesababisha kutokupatikana kwa kibali cha ubora wa kimataifa wa bidhaa za kampuni ya *Europe Inc.* na hivyo kuathiri ushindani wa soko la nje ya nchi. Kamati inashauri Serikali iangalie namna bora ya kushughulikia changamoto hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 58 ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makof*)

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA
MADINI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA
NISHATI (FUNGU 58) KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020
PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA
MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 -
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

[Imetolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016]

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) na Kanuni ya 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati (Fungu 58) kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Fasili ya 6(9) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati inao wajibu wa kusimamia majukumu na shughuli zinazotekelawa Wizara ya Nishati. Aidha, majukumu ya Kamati kuhusiana na Uchambuzi wa bajeti ya kila mwaka ya Wizara inazosimamia yamefafanuliwa katika Fasili ya 7(1)(a).

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni, Kamati ilifanya kazi zifuatatazo;

- a) Kutembelea na Kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa Fedha kwa mwaka wa Fedha 2019/2020 [**Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Bunge Toleo la Januari, 2016**]; na
- b) Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 [**Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Bunge Toleo la Januari, 2016**].

1.1 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitekeleza matakwa ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016 kwa kufanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelizwa na Wizara ya Nishati (Fungu 58). Ziara hizo zilifanyika katika Mikoa ya Pwani na Dar es Salaam. Lengo la ziara ni kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo chini ya Wizara ya Nishati iliyotengewa Fedha kwa mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, miradi iliyokaguliwa na Kamati yako kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ni kama ifuatavyo;

- (i) Miradi ya usambazaji wa gesi asilia majumbani na viwandani mkoa wa Dar es Salaam na Pwani;
- (ii) Miradi ya umeme Vijijini REA III Mkoa wa Pwani;
- (iii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Kinyerezi I Extension – MW 185;
- (iv) Kiwanda cha kutengeneza Nyaya na Mashine Umba (Transfoma) cha Africab Mivinjeni Kurasini na Europe Inc Dar es Salaam

1.2 Maelezo na Matokeo ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni maelezo ya miradi pamoja na changamoto ambazo Kamati ilizibaini kwa kila mradi wakati wa ukaguzi wake:

i. Mradi wa Usambazaji wa Gesi Majumbani Mkoa wa Pwani na Dar Es Salaam

Mheshimiwa Spika, Miradi ya usambazaji wa gesi asilia nchini inatekelezwa na Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya petroli (TPDC). Miradi hii inatekelezwa

katika maeneo ambayo tayari kuna miundombinu wezeshi hususani mabomba ya msukumo mkubwa na mdogo ya kusafirisha na kusambaza gesi asilia. Hadi mwezi Februari, 2020 miradi hiyo imeendelea kutekelezwa katika mikoa ya awali ikihusisha mkoaa wa Pwani na Dar es Salaam. Uunganishwaji wa wateja wa majumbani na viwandani umeendelea katika mikoa hiyo ambapo wateja hutumia gesi asilia kama nishati mbadala. Sambamba na matumizi haya ya gesi asilia pia gesi hii inatumika katika kuendeshea magari kwa mfumo wa CNG.

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha mwezi Juni 2019 hadi kufikia mwezi Februari 2020 Shirika limejenga miundombinu wezeshi yenye urefu wa kilomita 10.8 yenye uwezo wa kuanganisha nyumba zaidi ya 10,000. Hadi kufikia mwezi Februari 2020 zaidi ya nyumba 385 zimeunganishwa pamoja na "cafeteria" nne za chuo kikuu cha Dar es Salaam. Lengo ni kufikia nyumba za awali zaidi ya 1,385 jijini Dar es Salaam ifikapo mwezi Juni, 2021. Shirika limetenga jumla ya **Shilingi bilioni 3.2** kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea eneo la Mlalakuwa, survey pamoja na eneo la makazi Mikocheni, Dar Es Salaam pamoja na viwanda vya gesi Wilayani Mkuranga na kujionea namna ambavyo gesi imeunganishwa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuwepo kwa viwanda vingi maeneo ya Mwanambaya - Mkuranga, Shirika lilitoboa bomba kuu (*hot tapping*) linalotoka Mtwara hadi Dar es Salaam na kutoa toleo kwa ajili ya kuanganisha wateja eneo hilo. Zoezi la utoboaji bomba liliokamilika mwezi Septemba, 2018 limetoa fursa kwa wateja wengi zaidi kuanganishwa na matumizi ya gesi.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya hiyo ya Mkuranga, Kamati ilitembelea kiwanda cha *Lodhia Group* eneo la Kisemvule na kuona namna ambavyo mteja ameunganishwa na matumizi ya gesi asilia katika kuendeleza shughuli mbalimbali katika kiwanda hiki.

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha chuma cha *Lodhia Group of Industries* kilianza kutumia gesi asilia mwezi Juni, 2019. Kiwanda hiki kinatumia gesi asilia wastani wa futi za ujazo milioni 0.1 - 0.2 kwa siku sawa na makusanyo ya zaidi ya **Shilingi milioni 70** kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, wakati wa ziara ya ukaguzi wa miradi hii, changamoto iliyobainika ni mahitaji makubwa ya matumizi ya gesi ikilinganishwa na wateja wanaotumia gesi. Aidha, wateja walionesha kiu ya kutaka kuunganishiwa na huduma ya gesi asilia lakini bado utekelezaji wa mradi huu haujafikia wateja wengi.

Hatahivyo, Kamati inaipongeza Serikali kupitia Shirika la maendeleo ya Petroli nchini (TPDC) kwa kutoa pesa kwa ajili ya kuunganisha miundombinu ya gesi asilia ambayo imapelekea baadhi ya wateja kufikiwa na huduma ya gesi asilia. Aidha, Kamati inatoa Rai kwa Serikali kupitia TPDC kuongeza kasi ili kufikia wateja wengi zaidi kwa kuwa gesi bado **ipo ya kutosha na watuamiaji wengi bado hawajafikiwa**.

Mheshimiwa Spika, Uunganishwaji wa gesi asilia majumbani unahitaji kuwekewa mkazo ili uwiane na uharibifu wa mazingira unaosababishwa na matumizi makubwa ya nishati ya mkaa. Utafiti wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii unaonesha kuwa ukataji wa misitu unasababisha kuzalishwa kwa **tani 1,000,000** za mkaa kila mwaka ambapo nusu yake (**tani 500,000**) za mkaa zinatumika jijini Dar es Salaam pekee. **Hivyo ili tuweze kunusuru nchi yetu na janga hili la uharibifu wa**

mazingira, hatuna budi kuwekeza zaidi na kuruhusu sekta binafsi kushiriki katika miradi ya usambazaji na uunganishaji wa gesi majumbani.

ii. Miradi ya Wakala wa Umeme Vijijini (REA) Mkoa Wa Pwani

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Pwani umekuwa ukinufaika na Miradi ya umeme inayofadhiliwa na Serikali kuititia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na kusimamiwa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO). Miradi ambayo imetekelizwa katika Mkoa wa Pwani mpaka sasa ni REA Awamu ya kwanza (REA I), Mradi wa Mpito (Interim), REA Awamu ya pili (REA II), Ujazilizi awamu ya kwanza ('Densification' I), REA awamu ya tatu mzunguko wa kwanza na sasa wanatekeleza Mradi kabambe wa *Peri - Urban*.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea wilaya ya Mkuranga kijiji cha kisemvule na kuona utekelezaji wa miradi wa REA awamu ya tatu. Mkandarasi anayetekeleza Mradi huu wenyenamba AE/008/2017 - 18/HQ/G/39 Lot 3 ni Ceylex (pvt) Limited. Hata hivyo, mradi huu uko katika hatua za awali za utekelezaji na una thamani ya shilingi **Bilion 11.64**.

Mheshimiwa Spika, wakati wa ukaguzi wa mradi huu changamoto zifuatazo zilibainika;

- (a) Mwitikio mdogo wa uunganishwaji wa wateja na huduma ya umeme;
- (b) Kasi ndogo ya usambazaji wa umeme;
- (c) Maeneo ya vijiji na baadhi ya nyumba kutofikiwa na umeme katika zoezi la kusambaziwa na huduma ya umeme;
- (d) Uelewa mdogo wa wananchi juu ya gharama za uunganishwaji na huduma ya umeme;

- (e) Wizi wa Mafuta ya Mashine Umba (Transfoma) hivyo kupelekea baadhi kuungua na kukoseshaa huduma wananchi walio wengi;
- (f) Baadhi ya wananchi kuendelea kudai fidia kwa kupitiwa na miundombinu ya umeme licha ya kupewa elimu juu ya kutolipwa fidia.

iii. Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Kinyerezi I Extension – MW 185

Mheshimiwa Spika, mradi wa *Kinyerezi I Extension* unahusisha uzalishaji wa umeme wa MW 185 kwa kutumia gesi Asilia. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa **asilimia 100** kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 188** sawa na takriban **Shilingi bilioni 435.48**. Ujenzi wa mradi huu ulianza mwezi Novemba, 2016 na ultarajiwaa kukamilika mwishoni mwa mwezi Disemba, 2019.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea eneo la Kinyerezi na kujionea hali ya utekelezaji wa mradi huu ambapo kazi zilizokuwa zimeteklezwa ni pamoja na kukamilika kwa utengenezwaji wa mitambo yote minne (4) ya kufua umeme na kuanza kufungwa katika eneo la Mradi; kukamilika kwa upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha *Kinyerezi I Extension*; na kuendelea na upanuzi (*upgrade*) wa njia ya msongo wa **KV 132** kutoka Kinyerezi I hadi kituo cha kupoza umeme cha Gongo la Mboto.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla ujenzi wa mradi ulikuwa umefikia **asilimia 84**. Aidha, Kamati ilibaini kwamba, kutokana na matatizo ya kifedha yanayo mkabili mkandarasi aliyekuwa anatekeleza mradi huu ilipelekea mradi huu kusimama utekelezaji wake. Hivyo hadi wakati kamati yako inatembelea mradi ulikuwa umesimama utekelezaji wake.

Aidha, Wizara ilitoa taarifa kuwa wako katika hatua za kutafuta mkandarasi mwingine na matarajio ya Wizara ni kukamilisha mradi huu ifikapo mwezi Disemba, 2020.

iv. Kiwanda cha Europe Inc na Kilimanjaro Cables

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Kwanza unatekelezwa ipasavyo na kwa haraka, Serikali kuitia Wizara ya Nishati iliwaelekeza wakandarasi wote wanaotekeleza mradi kununua vifaa vyote muhimu vya mradi kutoka kwa wazalishaji wa ndani ya Nchi. Vifaa hivyo ni pamoja na mashine umba (*transfoma*), nyaya na "cables". Aidha, kuhusu vifaa ambavyo havizalishwi ndani ya nchi, Wakandarasi waliruhusiwa kuviajiza kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi 2020, Tanzania ina jumla ya viwanda vitano (5) ambavyo vinafanya uzalishaji wa nyaya zinazotumika kwenye ujenzi wa miradi ya usambazaji wa umeme zenyejumla ya urefu wa kilomita **196,435** za ukubwa mbalimbali kwa Mwaka, wakati mahitaji ya miradi ya REA na TANESCO ni kilometra takiribani **73,654** kwa Mwaka.

Uwezo wa Uzalishaji wa Nyaya kwa Mwaka			Uwezo wa Uzalishaji kwa Mwaka (km)
Na.	Kiwanda	Mahali kilipo	
1.	East Africa Cables	Vingunguti – DSM	12,000
2.	Europe Inc. Industries Ltd	Mikocheni – DSM	85,435
3.	Multi Cables Ltd	Chang'ombe - DSM	25,000
4.	Kilimanjaro Cables /Africab Ltd	Mivjeni – DSM	24,000
5.	Everwell Cables	Mkuranga – Pwani	50,000
Jumla			196,435

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi 2020, Tanzania ina jumla ya viwanda vitatu (3) ambavyo ni TANELEC, Europe Inc. Industries Ltd na Kilimanjaro Cables (T) Ltd vyenye uwezo wa kuzalisha jumla ya mashine umba (Transfoma) **24,800** za uwezo mbalimbali kwa Mwaka wakati mahitaji ya miradi ya REA na TANESCO ni mashine umba takribani **11,000** kwa Mwaka. Uwezo wa uzalishaji kwa kila kiwanda kwa mwaka ni kama inavyoonekana;

Uwezo wa Uzalishaji wa Mashine umba kwa Mwaka

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ziara katika kiwanda cha European inc pamoja na Kilimanjaro Cables vilivyopo Dar es Salaam na kujiona hali ya uzalishaji wa Mashine-umba (transfoma), nyaya na *cables*. **Kamati inaipongeza Serikali kuititia Wizara ya Nishati kwa uamuzi huo unaotoa fursa kwa Makampuni ya ndani kujenga uwezo na kutoa ajira kwa Watanzania.** Aidha, Kamati inazipongeza kampuni hizi kwa kuonesha uzalendo wa hali ya juu katika kuitikia wito wa kuwekeza hapa nchini na kuzalisha kwa wingi vifaa hivi muhimu.

Mheshimiwa Spika, wakati wa ziara hiyo Changamoto zifuatazo zilibainika;

- a) Wakandarasi wengi pamoja na watoa huduma ya vifaa kutokuwa na uzoefu wa kutumia "letter of credits" (LC's);

- b) Bado hakuna uelewa wa pamoja kwa makampuni ya vifaa katika kutoa huduma kwa wakandarasi wanaotekeleza miradi ya REA, hali ambayo imechangia kampuni chache kuweza kupata na kushinda zabuni za kutoa huduma ya kuwauzia wakandarasi vifaa hivi;
- c) Madeni ya Kampuni za kuzalisha vifaa kutolipwa kwa wakati na taasisi husika hivyo kufanya uzalishaji kuwa mgumu na vilevile kukwamisha ulipiaji malighafi bandarini kwa wauzaji wa malighafi na gharama nyingine za kiuendeshaji;
- d) Baadhi ya malighafi za kutengenezea Mashine-umba (Ambient Catalyst for XLPE conductor production; GALVANISED Stranded steel wire for ACRS and Arming process) HS-code zake kuhitaji kulipiwa "import duty" hivyo kuongeza gharama za uendeshaji na kuathiri bei ya bidhaa;
- e) Mfumo wa ukaguzi bidhaa bandarini kuchukua muda mrefu na hivyo kusababisha malighafi kuchelewa sana kuruhusiwa kutoka bandarini hivyo kuchelewesha upatikanaji wa malighafi na viwanda kulazimika kusimamisha uzalishaji;
- f) Ucheleweshaji wa kupatikana kwa cheti cha mazingira kutoka NEMC kwa kampuni ya EUROPE Inc. kumesababisha kutopatikana kibali cha ubora wa kimataifa ISO na hivyo kuleta athari kwenye ushindani wa soko la nje ya nchi.

1.3 Maoni ya Jumla Kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

Mheshimiwa Spika, kutokana na ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

- a) Pamoja na mafanikio makubwa yaliyofikiwa katika usambazaji wa umeme vijijini, Kamati inaona kuwa yapo

maeneo mengi ya vijiji na vitongoji yanayohitaji kusambaziwa huduma ya umeme. Kamati inaishauri Serikali kuongeza wigo (scope) kwa wakandarasi ili kuweza kukidhi mahitaji ya wananchi kufikiwa na nishati ya umeme katika maeneo mbalimbali.

- b) Kamati inashauri Serikali kuendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya gharama za uunganishwaji wa huduma ya umeme ili wananchi wafahamu malipo halisi wanayostahili kulipa wanapohitaji kuanganishiwa huduma ya umeme;
- c) Serikali iendelee kusimamia na kufuatilia kwa karibu mienendo ya wawekezaji binafsi hususan kwenye eneo la usalama wa wafanyakazi ili kuhakikisha kuwa kanuni za usalama kwa watumishi pamoja na upatikanaji wa maslahi ya watumishi ikiwemo mikataba ya ajira yanazingatiwa;
- d) Kufuatia Mkandarasi anaetekeleza mradi wa Kinyerezi I Extension 185MW kushindwa kukamilisha mradi na hivyo kuacha mradi bila kumalizika, Kamati inatoa rai kwa Serikali kuhakikisha kuwa "sub-contractors" wote ambao walikuwa wanatoa huduma kwa kampuni hii wanalipwa fedha zao kwa wakati kwani makampuni mengine yana mikopo kwenye mabenki; hivyo jinsi wanavyochelewa kulipwa ndivyo ambavyo riba za mikopo hiyo inavyozidi kupanda na hivyo kuhatarisha uhai wa kampuni hizo;
- e) Kwa kuwa hapa nchini ipo gesi ya kutosha, ipo haja kwa TPDC kuongeza kasi ya uungwanishwaji wa wateja wanaohitaji kutumia gesi. Mathalan wakati ambapo katika maeneo ya viwanda yaliyopo Mkuranga miundombinu ya gesi tayari imefika, lakini uunganishwaji wa wateja haujafikia kiwango cha juu cha mahitaji.
- f) Ni vyema kabla Mkandarasi hajapewa mkataba wa kazi ya kupeleka Umeme kwenye Vijiji mbalimbali, kazi ya upembuzi yakinifu kwenye maeneo tajwa ishirikishe wawakilishi wa Wananchi katika ngazi zote ili kuondoa tatizo la Wakandarasi kupewa wigo mdogo wa kazi kinyume na uhalisia wa maeneo/Vijiji husika.

g) Wananchi wengi wa vijiji ni hawana uelewa mpana wa namna huduma za umeme vijiji ni zinavyo patikana pamoja na gharama halisi wanazo paswa kulipia ili kuunganishwa huduma ya umeme hali inayosababisha kuwa na muamko mdogo wa kuunganishwa na huduma za umeme. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutoa elimu ya kina kwa wananchi katika eneo hili.

1.4 Sekta Ndogo ya Gesi Asilia

Mheshimiwa Spika, Kiasi cha gesi kilichogunduliwa *Gas Initially In Place (GIIP)* katika maeneo ya nchi kavu na baharini kufikia Februari 2020, ni takribani **futi za ujazo Trilioni 57.54**. Kati ya kiasi hicho, gesi iliyo gunduliwa nchi kavu (*onshore*) ni **futi za ujazo Trilion 10.46** na kwa upande wa Bahari Kuu (*offshore*) ni **futi za ujazo Trillion 47.08**. Shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi katika maeneo mbalimbali nchini zinaendelea kufanyika ingawa kwa kipindi kirefu makampuni mengi yalipunguza kasi kwa kuwa yalikuwa yakisubiri kukamilika kwa mapitio ya Mikataba (PSAs).

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kwamba kwakuwa mapitio ya mikataba yamekamilika kwa upande mwingine, TPDC iendelee na shughuli za awali za utafutaji wa mafuta na gesi katika eneo la Eyasi Wembere katika mikoa ya Rukwa, Singida na Manyara ili baadaye maeneo hayo nayo yaendelezwe.

Mheshimiwa Spika, Katika uchambuzi wa taarifa ya sekta ndogo ya gesi, Kamati ilibaini kuwa, Hali ya upatikanaji wa Mafuta, Gesi Asilia na Gesi ya Mitungi nchini imeendelea kuwa nzuri na yenye kuimarika. Ambapo, hadi kufikia mwezi Februari 2020 uwezo wa jumla wa kuhifadhi mafuta katika maghala yaliyo katika bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara ni mita za ujazo 1,127,611. Aidha, miundombinu ya kupokea na kuhifadhi Gesi ya Mitungi (*Liquefied Petroleum Gas - LPG*) katika bandari ya Dar es Salaam na Tanga imefikia uwezo wa kuhifadhi tani 15,600 kwa mara moja. Vilevile, upatikanaji wa Gesi ya Mitungi umeendelea kuwa wa kuridhisha ambapo matumizi yamefikia tani 145,800 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na hatua hiyo, hali ya mindombinu ya uchakataji, usafirishaji na matumizi ya gesi asilia nchini imeendelea kuwa yakuridhisha. Hadi kufikia mwezi Februari 2020, uwezo wa uzalishaji (uchakataji) wa gesi asilia nchini umefikia futi za ujazo (mmscf) milioni 210 kwa siku kutoka futi za ujazo (mmscf) milioni 95 kwa siku mwaka 2015.

1.5 Umuhimu wa kufanya marejeo ya Mikataba (PSAs)

Mheshimiwa Spika, Kamati yako ilipitia na kufanya uchambuzi kwa kina kuhusu taarifa ya uendelezaji wa mikataba ya gesi asilia nchini ambapo hadi kufikia Januari 2020, mikataba hai ya utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia iliyopo nchini ni kumi na mbili (12) ambayo inatekelezwa na kampuni za kimataifa nane (8). Mikataba mitatu (3) kati ya hiyo ipo katika hatua za uzalishaji ambayo ni Songo Songo, Mnazi Bay na Kiliwani North; mikataba tisa (9) iko katika hatua ya utafutaji ambayo ni Kitalu Na. 1 na 2, Kitalu Na. 4, Ruvuma, Ruvi, Tanga, Rukwa, Kilosa-Kilombero, Bigwa Rufiji Mafia na Nyuni.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa, kwa sasa Shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi katika maeneo mbalimbali nchini zinaendelea kufanyika ingawa makampuni mengi yamepunguza kasi kwa kuwa yalikuwa yakisubiri kukamilika kwa mapitio ya Mikataba (PSAs) ili yaweze kuhuishiwa leseni zao. Kimsingi mapitio ya mikataba ya utafutaji na uzalishaji mafuta na gesi asilia (PSAs) yanalenga kuhakikisha kuwa Serikali inanufaika ipasavyo kupitia mikataba hiyo.

Mheshimiwa Spika, Uwekezaji katika Sekta hii unahitaji mtaji mkubwa, ambapo Serikali nydingi duniani hushirikisha sekta binafsi kwenye utafutaji na uendelezaji wa sekta ya mafuta na gesi asilia. Tanzania inashindana kuvutia uwekezaji na nchi mbalimbali za Afrika kama vile Kenya, Uganda, Angola, Ghana, Mozambique na Nigeria pamoja na nchi za bara la Asia kama vile Qatar, Oman, Trinidad & Tobago na Papua New Guinea. Maamuzi ya Serikali yana mchango mkubwa katika kuvutia au kutokuvutia wawekezaji. Tunaishukuru Serikali kwa kuanza kuhuisha leseni tajwa katika muda

muafaka kwakuwa kuchelewa kufanya hivyo kungeleta athari za kupunguza uwekezaji kwa muda katika Sekta hii.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, pamoja na umuhimu wa kuhuisha leseni husika kwa wakati, madhara makubwa zaidi yanaweza kutokea endapo leseni hizo zitahuishwa bila kufanyika uchambuzi wa kina na wa kutosha katika mikataba (PSAs) iliyopo, umakini mkubwa unahitajika katika zoezi hili la mapitio ya mikataba. Ni matumaini ya Kamati kuwa kazi ya kupitia mikataba (PSAs) itawezesha Serikali na Taifa kwa ujumla kunufaika ipasavyo na rasilimali ya gesi asilia.

1.6 Hali ya Upatikanaji wa Mafuta Nchini

Mheshimiwa Spika, majukumu ya jumla ya Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA) ni pamoja na kutathmini mahitaji ya Mafuta nchini na kuratibu uagizaji wa Mafuta hayo kwa mfumo wa manunuzi ya pamoja (Bulk procurement System – BPS). Vile vile Wakala amepewa jukumu la kuhakikisha mafuta yanayoletwa nchini yanakidhi mahitaji na ubora unaotakiwa. Aidha, Taasisi hii imepewa mamlaka ya kuhakikisha mafuta yananunuliwa kwa njia yenye ufanisi (*efficient procurement*) kwa manufaa ya taifa. Pia kuhakikisha uhakika wa usalama wa upatikanaji wa mafuta nchini (*Security of Supply*), na kuiwezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Taasisi mbalimbali za Serikali kukusanya mapato na tozo zitokanazo na mafuta yaliyoagizwa na kwa muda uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, jumla ya **lita 4,161,067,814.92** za mafuta ya dizeli, petroli, ndege na taa ziliingizwa kwa matumizi ya ndani ya nchi (*local*) na nchi za jirani (*transit*) kwa kipindi cha Julai 2019 hadi Februari 2020. Katika kiasi hiki cha mafuta, jumla ya **lita 2,398,969,342.12** sawa na asilimia 58 kilikuwa kwa ajili ya matumizi ya ndani, na **lita 1,762,098,472.80** sawa na asilimia 42 kwa ajili ya nchi za jirani. Ufuatao ni mchanganuo wa kiasi cha Mafuta kilicho agizwa kwa kipindi husika.

Mwezi	Dzeli (Utaza ujazo)	Petidi (Utaza ujazo)	Mafuta ya ndege/ Mafuta ya taa (Utaza ujazo)	Jumla Kuu
JUA	263,073,231.000	174,424,348.000	34,614,214.000	472,111,793.000
AGOSTI	278,804,029.000	178,908,894.000	33,002,819.000	490,715,742.000
SEPTEMBA	267,476,245.000	155,776,242.000	35,887,357.000	459,139,844.000
OKTOBA	340,729,901.000	215,889,022.000	41,205,525.000	597,824,448.000
NOVEMBA	361,809,665.000	230,528,705.000	42,452,937.000	634,791,307.000
DESEMPA	321,653,123.000	232,376,002.000	26,202,176.000	580,231,301.000
JANUARI	303,686,416.000	224,310,123.000	32,433,934.000	560,430,473.000
FEBRUARI	126,566,339.767	213,407,392.817	25,849,174.587	365,822,907.172
JUMAKU	2,263,798,949.767	1,625,620,728.817	271,648,136.587	4,161,067,815.172


Chanzo; Taarifa ya Utekelezaji wa Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA) kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua taarifa kuhusu hali ya upatikanaji wa mafuta nchini na kubaini kuwa, kwa kipindi chote cha Julai 2019 hadi Februari 2020 hali ya upatikanaji wa Mafuta nchini ilikuwa nzuri ambapo nchi ilikuwa na akiba ya Mafuta ya kutosha kwa wastani wa zaidi ya siku 40 kwa kila aina ya Mafuta wakati wote. Hii ni ongezeko la asilimia 55% ikilinganishwa na siku 15 za akiba ya Mafuta zinazotakiwa kwa mujibu wa kanuni.

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa BPS (Bulk procurement System) umewezesha kupungua kwa gharama za meli kusubiri kupakua mafuta. Hii imetokana na upangaji na usimamizi mzuri wa uletaji meli za mafuta (*laycan*) ambao umepelekea muda wa meli kusubiri kupungua kutoka wastani wa siku 45 kwa siku za nyuma hadi wastani wa siku 5 kwasasa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa, kwa kipindi cha Julai 2019 hadi Februari 2020 gharama za Meli kusubiri imepungua kwa **asilimia 18.4** ikilinganishwa na kipindi kama hicho kwa mwaka 2018/2019. Ufualao ni mchanganuo wa gharama husika;

MONTH	SPM		KOJ1		AVERAGE	
MONTH	Y2018/19	Y2019/20	Y2018/19	Y2019/20	Y2018	Y2019
Jul	1.6321	1.2882	4.4243	1.3612	3.0448	1.3182
Aug	1.7682	1.4277	4.9680	1.2314	3.1017	1.5236
Sep	2.2745	1.8200	4.5162	1.1303	3.2114	1.6820
Oct	1.4084	1.3747	2.7909	1.2254	1.9559	1.3149
Nov	1.8162	1.9164	1.4815	1.1363	1.6679	1.6037
Dec	1.7824	2.3169	1.8874	2.7974	1.8295	2.5263
Jan	2.8816	1.4651	1.9527	4.8693	2.4942	2.9472
Feb	1.4179	1.6519	3.0135.7539	4	2.0990	2.7334
OVERALL	1.8883	1.6951	3.1013	2.3459	2.4028	1.9610



Chanzo; Taarifa ya Utekelezaji wa Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA) kwa mwaka 2019/20.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na hali ya upatikanaji wa mafuta nchini pamoja na usimamizi mzuri wa uagizaji wa mafuta unaofanywa na Wizara kuitia Wakala wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja (PBPA) kwa kushirikiana na mamlaka nyingine. Ni matumaini ya Kamati kuwa Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja utaendelea kusimamia sekta ya mafuta kwa ufanisi kwa manufaa ya uchumi wa nchi yetu.

Aidha, Kamati ina matumaini kuwa Wakala utaendelea kushirikiana na Wadau wengine kwa lengo la kuendelea kuimarisha mfumo wa uagizaji wa Mafuta nchini hususan katika kipindi hiki ambapo Ulimwengu unakabiliwa na changamoto kubwa ya Ugonjwa wa homa ya Mapafu (COVID -19); changamoto ambayo Taasisi mbalimbali za Utafiti za Kimataifa kama IMF, World Bank, UNECA, na Fitch Solutions zinatabiri kutokea kwa m dororo wa uchumi ulimwenguni utakaoathiri shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Tayari Ulimwengu umeanza kushuhudia Sekta za Usafiri wa Anga na Utalii kusimama, biashara na uzalishaji viwandani kushuka na hivyo kushuka kwa kiasi kikubwa kwa matumizi ya mafuta. Kufuatia kushuka kwa matumizi ya mafuta ulimwenguni tumeshuhudia vilevile katika siku za hivi karibuni bei ya mafuta kwenye soko la kimataifa kushuka kwa kiwango kikubwa ambacho hakijawahi kushuhudiwa. **Hivyo basi kufuatia mkanganyiko huu na mwenendo usiotabirika wa soko la mafuta ulimwenguni, ipo haja kwa nchi yetu kuweka mikakati thabiti ya kuhakikisha nchi inakuwa na akiba ya mafuta ya kutosha wakati wote.** Aidha, Serikali itumie mwanya huu wa m dororo wa bei ya mafuta ulimwenguni kuzungumza na nchi rafiki zinazozalisha mafuta ili kama nchi tuweze kupata mafuta kwa masharti nafuu sasa, na kuitia TPDC tuweze kuanzisha hifadhi ya mafuta ya kimkakati kwa ajili ya kuhami uchumi wetu kwa siku zijazo.

1.7 Hali ya Upatikanaji wa Umeme Nchini

Mheshimiwa Spika, Shirika la Umeme nchini (TANESCO) linaendesha mfumo uliouunganishwa wa Gridi ya Taifa wenye

mitambo ya kufua umeme kwa kutumia maji, gesi asilia na mafuta.

Mheshimiwa Spika, Kamati yako ilifanya uchambuzi kuhusu taarifa ya hali ya upatikanaji umeme nchini na kubaini kuwa, hadi kufikia mwezi Februari, 2020 uwezo wa mitambo ya kufua umeme iliyounganishwa katika mfumo wa Gridi ya Taifa ulikuwa **Megawati 1,565.72** ambapo Megawati 573.70 (36.64%) zinatokana na vyanzo vya nguvu ya maji, Megawati 892.72 (57.02%) ni vyanzo vya gesi asilia, Megawati 88.80 (5.67%) zinatokana na Mafuta na Megawati 10.50 (0.67%) zinazalishwa kutokana na mabaki ya mimea na mazao (Biomass). Uwezo wa mitambo hiyo unajumuisha mitambo inayomilikiwa na TANESCO ambayo huchangia **asilimia 86.50** na mitambo ya wazalishaji binafsi (IPPs/SPPs) ambayo huchangia **asilimia 13.50**. Aidha, Shirika linamiliki mitambo ambayo haljaunganishwa katika mfumo wa gridi ya Taifa yenye uwezo wa kufua **Megawati 36.598** na hivyo kufanya jumla ya uwezo wa mitambo ya kufua umeme nchini kufikia **Megawati 1,602.318**.

Mheshimiwa Spika, Kamati yako ilibaini kuwa mahitaji ya juu ya umeme katika mfumo wa gridi ya Taifa yameendelea kukua kwa kasi ambapo kwa mwezi Februari, 2020 pekee mahitaji yameongezeka kutoka **Megawati 1,125.36** zilizofikiwa tarehe 07 Februari, 2020 saa 3 usiku na kufikia **Megawati 1,151.66** zilizofikiwa tarehe 27 Februari, 2020 saa 3 usiku. Hili ni sawa na ongezeko la **asilimia 3.14** ukilinganisha na **Megawati 1,116.58** zilizokuwa zimefikiwa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, TANESCO pia hununua umeme kutoka kwa wazalishaji wadogo (SPPs) ndani ya nchi ambao ni: Mwenga **MW 4**; TPC **MW 9**; TANWAT **MW 1.5**; Yovi **MW 0.95**; Tulila **MW 5**; Darakuta **MW 0.32**; Andoya **MW 0.5**; na Matembwe **MW 0.59**. Aidha, TANESCO ina mikataba ya kununua umeme kutoka nje ya nchi (imports) ambapo **MW 17** ni kutoka Uganda kwa ajili ya Mkoa wa Kagera; **MW 1** ni kutoka Kenya kwa ajili ya Wilaya ya Longido; na **MW 5** ni kutoka Zambia kwa ajili ya Mkoa wa Rukwa. **Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada kubwa zinazofanyika katika**

kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na umeme wa kutosha, uhakika na unaotabirika wakati wote kutoka katika vyanzo mchanganyiko kwa kushirikisha wazalishaji wadogo (Small Power Projects – SPP). Aidha, ili kulinda uwekezaji ambao tayari wazalishaji wadogo wa umeme wameufanya na hivyo kuweza kuhudumia zaidi ya wateja 100,000 hapa nchini na vilevile kuendelea kujenga imani kwa wawekezaji kuwa mazingira ya ufanyaji biashara hapa nchini yanatabirika, Kamati inaona ipo haja kwa Serikali kuharakisha mchakato wa kutafuta suluhi ya mkanganyiko wa bei ya kuuzia umeme unaozalishwa na wazalishaji wadogo.

1.8 Tathmini ya Miradi ya Umeme Vijijini (REA III) Mzunguko wa Kwanza

Mheshimiwa Spika, Jumla ya vijiji vilivyokuwa vimefikiwa na umeme hadi kufikia **31.12.2015** ni **2,018**. Aidha, Jumla ya vijiji vilivyofikiwa na umeme Tanzania Bara hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020 ni 9,112. Jumla ya vijiji vitakavyofikiwa na umeme Tanzania Bara (miradi ya **Off-grid(REA & Private)**, **REA III – Round I, Densification I** na **REA II pamoja na miradi ambayo inatekelezwa na TANESCO**) itakapokamilika mwezi Juni 2020 ni: **10,446**. Jumla ya vijiji vitakavyobaki bila umeme ifikapo 01.07.2020 ni: **1,822**. Aidha, Jumla ya vijiji Tanzania Bara kwa mujibu wa TAMISEMI 2015 ni: **12,268**. Jumla ya taasisi zilizofikiwa na umeme hadi 31.12.2015 ni **4,036** na Jumla ya taasisi zilizofikiwa na umeme hadi 29.02.2020 ni **11,377**.

Mheshimiwa Spika, Kamati yako ilichambua taarifa ya Utekelezaji wa miradi ya REA na kufanya tathmini ya namna ya utekelezaji wake ambapo Mradi wa REA awamu ya tatu unatekelezwa katika mikoa 25 ya Tanzania Bara. Mradi umegawanya katika mafungu 29 (29 Lots) ambayo yanatekelezwa na jumla ya wakandarasi 16 ambapo kati yao, wakandarasi 11 ni wazawa na wakandarasi 5 ni kutoka nje ya nchi. Mradi huu unatarajwa kukamilika mwezi Juni 2020.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa pamoja na changamoto ndogo ndogo za Wananchi wengi kuhitaji

umeme, hali ya utekelezaji wa mradi wa umeme vijijini kwa wastani unaridhisha.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 26.03.2020 jumla ya TZS **457,477,112,939.87 (VAT Inclusive)** sawa na **asilimia 53** za gharama nzima ya mradi kwa upande wa fedha za ndani na **USD 80,912,192.86 (VAT Inclusive)** sawa na **asilimia 71** za gharama nzima ya mradi kwa upande wa fedha za kigeni zimelipwa kwa wakandarasi kwa ajili ya kazi za mradi pamoja na ununuzi wa vifaa.

Mheshimiwa Spika, tarehe 31.12.2019 Wakala ulifanya tathmini ya wakandarasi wanaotekeleza mradi wa kusambaza umeme vijijini awamu ya tatu mzunguko wa kwanza (REA III Round I) na kubaini kuwa jumla ya mikataba **22** kati ya **29** sawa na **asilimia 75.9** ilikuwa inatekelezwa vizuri juu ya malengo. Aidha, mikataba **5** kati ya **29** ilikuwa katika wastani na **mikataba 2** ilikuwa inatekelezwa chini ya malengo. Kufuatia kubainika kwa mikataba 2 ambayo utekelezaji wake ulikuwa chini ya malengo, hatua za kimkataba zilichukuliwa ambapo wakandarasi wanaotekeleza waliandikiwa barua (Notice of Default) tarehe 10.01.2020 yenyeye Kumb. Na.: AG 143/171/09/Vol. II/85 ikieleza nia ya Muajiri kutaka kuvunja mkataba na kuwapatia kipindi cha siku 14 kufanya marekebisho ya mapungufu yote na kuhakikisha mikataba inakamilika kwa wakati. **Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza kuchukua hatua hizo. Hatua hizo zimeyafanya Makampuni kuongeza kasi katika utendaji wake.**

Mheshimiwa Spika, Pamoja na kazi nzuri inayoendelea kufanywa na Wakala wa Umeme vijijini (REA) zipo changamoto kadhaa zinazohitaji kuboreshwa. Maeneo hayo ni pamoja na mwamko mdogo wa wananchi kuunganishwa na huduma ya umeme katika baadhi ya maeneo ambayo tayari miundombinu imefika.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inaona ipo haja ya wakandarasi kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi hii, hatahivyo, Serikali inapaswa kuendelea kuweka nguvu ya kiusimamizi na ufuatiliaji wa wakandarasi wanaotekeleza

miradi hii kuhakikisha kuwa miradi hii inakamilika kwa wakati na kwa ubora uliokusudiwa kulingana na matakwa ya mikataba. Aidha, iko haja ya Serikali wa kupanua wigo (scope) ya utekelezaji wa miradi hii ili kuwafikia Watanzania wengi kwa wakati mfupi.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa Bajeti kwa kuzingatiaji mambo makuu matatu ambayo ni:-

- a) Makusanyo ya Maduhuli kwa mwaka wa Fedha 2019/2020;
- b) Hali ya upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina na;
- c) Uzingatiaji wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati ya Nishati na Madini wakati huo.

2.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli na Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka 2019/2020

- a) **Makusanyo ya Maduhuli kwa mwaka wa Fedha 2019/2020;**

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2019/2020, Wizara ya Nishati ilipangiwa kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 602.05**. Kati ya makusanyo hayo, jumla ya **Shilingi bilioni 602.04** zillitarajiwa kukusanya kuititia shughuli za mafuta na gesi asilia na **Shilingi 12,000,000.00** kuititia shughuli za utawala. Mapato hayo yanatokana na vyanzo mbalimbali vikiwemo: Shughuli za TPDC za utafiti wa mafuta; Mauzo ya gesi asilia; na Mauzo ya Nyaraka za Zabuni.

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha mwezi Julai 2019 hadi Februari 2020 jumla ya **Shilingi bilioni 377.15** zilikusanya kutokana na shughuli za mafuta na gesi asilia zilizoratibisha na TPDC. Kamati ilibaini kuwa Kiasi hicho ni sawa na **asilimia**

89.5 ya lengo la makusanyo ya **Shilingi bilioni 421.36** kwa kipindi hicho. Aidha, **Kamati inatoa rai kwa Wizara kuendelea na jitihada za kuimarishe ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali kutoka vyanzo vya mafuta na gesi asilia.**

b) Hali ya upatikanaji wa fedha kutoka Hazina;

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka 2019/2020, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liliidhinisha Bajeti ya Jumla ya **Shilingi 2,142,793,309,000** kwa Wizara ya Nishati. Kati ya Fedha hizo, Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ni **Shilingi 2,116,454,000,000** sawa na **asilimia 98.8** ya bajeti yote ya Wizara. Bajeti ya Fedha za ndani iliyotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi 1,956,372,000,000** sawa na **asilimia 92.4** ya Bajeti yote ya Maendeleo. **Shilingi 160,084,000,000** sawa na **asilimia 7.6** ni fedha za nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyotengwa kwa Mwaka 2019/2020 ni **Shilingi 26,339,309,000** sawa na **asilimia 1.2** ya bajeti yote ya Wizara. Kati ya fedha hizo **Shilingi 15,025,821,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (O.C) na **Shilingi 11,313,488,000** kwa ajili ya kulipa mishahara (P.E) ya watumishi wa Wizara na Taasisi zilizopo chini yake.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2019 hadi Februari 2020 Fedha zilizopokelewa kwa bajeti ya Wizara ya Nishati ni **Shilingi bilioni 686.63** sawa na **asilimia 68.4** ya lengo la miezi minane (8). Kati ya Fedha hizo zilizopokelewa, **Shilingi bilioni 9.91** ni fedha za matumizi mengineyo (O.C) ambayo ni sawa na **asilimia 98.9** ya lengo na **Shilingi bilioni 6.5** ni mishahara sawa na **asilimia 86.3** ya lengo.

Aidha, **Shilingi bilioni 670.20** ni za miradi ya maendeleo sawa na **asilimia 67.9** ya lengo la fedha za maendeleo. Fedha za ndani zilizopokelewa ni **Shilingi bilioni 572.34** sawa na **asilimia 65.8** ya lengo la fedha za ndani na **Shilingi bilioni 97.88** sawa na **asilimia 83.9** ya lengo la fedha za nje. Kamati ilibaini kuwa Fedha hizo zimetokana na kazi ambazo tayari zimekamilika na hati za madai (*certificates and invoices*) kuwasilishwa na kuhakikiwa.

Kwa kazi ambazo zinaendelea, Kamati ilielezwa kuwa madai yake hayajawasilishwa kwa ajili ya malipo, na kwamba pindi kazi husika zikikamilika na hati za madai husika kuwasilishwa; madai hayo yatalipwa. Aidha, baadhi ya miradi hupokea fedha za ndani na za nje kulingana na wakandarasi wanavyowasilisha madai (*certificates and invoices*), na baadhi ya miradi hupokea fedha za nje moja kwa moja (*direct to Project funds*) ambazo taarifa zake huingizwa (kuhesabiwa) katika hesabu za Wizara mwisho wa mwaka husika.

Ni Rai ya Kamati kuwa mara baada ya madai husika kuwasilishwa, Fedha za Miradi ya Maendeleo zitatolewa kwa wakati.

MUHTASARI WA FEDHA ZILIZOPOKELEWA KWA MWAKA 2019/2020 HADI KUFIKIA MWISHONI MWA MWEZI FEBRUARI 2020

Chanzo; Taarifa ya Utekelezaji wa Wizara ya Nishati (Fungu 58) kwa mwaka wa Fedha 2019/2020

c)Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa KamatiMheshimiwa **Spika**, katika uchambuzi wa Bajeti ya Mwaka 2019/2020 Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekoz, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Toleo la Januari, 2016 inayoelezea majukumu ya Kamati ya kusimamia na kufuatilia utendaji kazi wa shughuli za Wizara. Napenda kiliarifu Bunge lako tukufu kuwa, sehemu kubwa ya ushauri uliotolewa na Kamati umezingatiwa na baadhi

unaendelea kufanyiwa kazi zaidi na Serikali. Maoni ambayo kamati inaamini ni muhimu na yanahitaji kufanyiwa kazi zaidi ni yafuatayo:-

i. **Miundombinu wezeshi ya mradi wa umeme wa mto Rufiji (Nyerere hydropower)** hasa barabara, madaraja na makalavati ni vema ikawa imara na ya kudumu na kuweza kuitika wakati wote ili kuhakikisha kuwa ujenzi wa mradi unatekelezwa bila vikwazo.

ii. **Mfumo wa gawio la mapato yatokanayo na Mafuta na Gesi** - Upo umuhimu wa Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya mafuta na Gesi ya mwaka 2015 kuangaliwa upya ili pamoja na mambo mengine ibadili mfumo wa kuigawia TPDC fedha za mfuko wa Gesi Asilia na Mafuta kwa kutegemea uchangiaji wa Pato la Taifa (GDP) kwa asilimia 3.

iii. **Ulipaji Fidia wananchi** - Serikali ilipe fidia kwa wakati kwa wananchi wote wanaotoa maeneo yao kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. **Aidha, Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kulipa fidia ya takribani kiasi cha Shilingi bilioni 5.2 kwa wananchi waliopisha utekelezaji wa mradi wa gesi Asilia (LNG) mkoani Lindi. Hakika kilio chao kilikuwa cha muda mrefu na sasa Serikali imetekeleza kiu ya wananchi hawa kwa wakati muafaka.** Mheshimiwa Spika, Ni Rai ya Kamati kuwa Wizara itaendelea kufanya kazi maoni na ushauri unaotolewa na Kamati.

2.2 Uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa (Fungu 58) Mwaka Wa Fedha 2020/2021

2.2.1 Mapitio ya Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati inaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Mpango Mkakati wake. Kulingana na Mpango Mkakati huo Wizara ina malengo makuu sita (6) ambayo ni:

- i) Kuongeza uzalishaji na kuboresha mifumo ya usafirishaji na usambazaji wa umeme;
- ii) Kuongeza mchango wa nishati jadidifu katika matumizi mbalimbali ya nishati;
- iii) Kuimarisha shughuli za utafiti na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia;
- iv) Kuboresha rasilimali za Wizara ili kutoa huduma bora za nishati;
- v) Kutekeleza kwa ufanisi Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Kuzuia Rushwa; na
- vi) Kupunguza maambukizi ya VVU na UKIMWI sehemu za kazi na kuboresha utoaji wa huduma kwa waathirika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na malengo hayo Wizara inapaswa kuendelea kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara na Taasisi zake katika kusimamia Sekta ya Nishati ikiwemo kuendelea kuelimisha umma na kuboresha mawasiliano kati ya Wizara na wadau mbalimbali kuhusu masuala ya nishati.

2.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato

2.3.1 Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2020/2021
Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2020/2021, Wizara ya Nishati (Fungu 58) inakadiria kutumia jumla ya **Shilingi 2,488,289,499,000** ikilinganishwa na **Shilingi 2,142,793,309,000** zilizotengwa kwa Mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia **16.1**.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyotengwa kwa Mwaka 2020/2021 ni **Shilingi 28,399,590,000** sawa na **asilimia 1.1** ya bajeti yote ya Wizara. Kati ya fedha hizo **Shilingi 15,025,821,000** zitatumika kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (O.C) na **Shilingi 13,373,769,000** ni kwa ajili ya mishahara (P.E) ya watumishi wa Wizara na Taasisi zilizopo chini yake.

2.3.2 Makadirio ya bajeti ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika mwaka 2020/2021 unakadiria kutumia jumla ya **Shilingi 2,459,889,909,000** ambazo ni sawa na **asilimia 98.9** ya bajeti yote ya Wizara. Bajeti ya fedha za ndani zilizotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi 1,967,689,292,000** sawa na **asilimia 80** ya Bajeti yote ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa Kiasi kikubwa cha fedha za ndani za maendeleo kimeelekezwa katika miradi ya kielelezo na kimkakati ambayo ni: Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere, MW 2,115; Mradi wa Kusambaza Umeme Vijiji Awamu ya Tatu; Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Kinyerezi I Extension MW 185; na Miradi ya Ruhudji, Rumakali, Singida - Arusha - Namanga, Iringa - Mbeya - Sumbawanga - Kigoma na LNG, EACOP. Aidha, Bajeti ya Fedha za Nje inayopendekezwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi 492,200,617,000** sawa na **asilimia 20** ya Bajeti yote ya Maendeleo.

Muhtasari wa Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2020/2021

A: FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA		
MAELEZO	BAJETI	ASILIMIA (%) YA BAJETI YOTE
Mishahara (P.E)	13,373,769,000.00	
Matumizi Mengineyo (O.C)	15,025,821,000.00	
Jumla Fedha za Matumizi ya Kawaida	28,399,590,000.00	1.1 %
B: FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO		
Fedha za Ndani	1,967,689,292,000.00	
Fedha za Nje	492,200,617,000.00	
Jumla Fedha Za Maendeleo	2,459,889,909,000.00	98.9 %
JUMLA KUU	2,488,289,499,000.00	100%

Chanzo; Maeleo ya Randama kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka 2019/2020

Aidha, kwa upande wa makisio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka 2020/2021, Wizara inakadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 160,622,137,324**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 160,601,745,679** zitakusanya kupitia shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia; na **Shilingi 20,391,645** zitakusanya kupitia shughuli za utawala. **Kamati inatoa angalizo kwa Serikali kuwa upo uwezekano mkubwa wa kuwepo kwa m dororo wa shughuli za uwekezaji ulimwenguni kutokana na uwepo wa janga la COVID-19; hali ambayo inaweza kuathiri makisio ya makusanyo yaliyowekwa.** Kwa muktadha huu, Kamati inaishauri Serikali kufuatilia kwa karibu hali ya uwekezaji inavyoendelea ulimwenguni ili kuweza kufanya mapitio ya haraka kwenye mipango iliyowekwa.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kutekeleza majukumu yake ya kikanuni ambayo ni ukaguzi wa miradi ya maendeleo na uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, Kamati ina maoni na ushauri ufuaao kwa Serikali: -

3.1 Utekelezaji wa Mradi wa Julius Nyerere - MW 2,115

Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maji katika Bonde la Mto Rufiji (Julius Nyerere - MW 2,115) una umuhimu wa kimkakati kwa uchumi wa taifa letu, **Na kwakuwa** katika mwaka 2019/20 utekelezaji wake ulijielekeza katika ujenzi wa miundombinu wezeshi; **Na kwamba** kwa mwaka 2020/2021 mradi unaingia katika hatua muhimu sana ya utekelezaji ikiwemo kuanza kwa ujenzi wa bwawa (main dam and spillways), ujenzi wa njia kuu za kupitisha maji (tunnels), ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme (Power House) na ujenzi wa kituo cha kusafirisha umeme (Switch yard). Kamati inatoa rai kwa Serikali kuhakikisha kuwa inaongeza usimamizi, na kuhakikisha Fedha za uendelezaji wa mradi zinapatikana kwa wakati kama zilivytengwa na kuidhinishwa na Bunge.

3.2 Utekelezaji wa Mradi wa Kinyerezi I Extension

Kamati ilibaini kuwa mkandarasi anayetekeliza mradi wa *Kinyerezi I Extension* 185MW ameshindwa kutekeleza majukumu yake ya kimkataba na kuuacha mradi bila kumalizika, kutokana na changamoto hiyo Kamati inatoa rai kwa Serikali kuhakikisha mkandarasi mwingine wa kumalizia mradi anapatikana kwa haraka. **Aidha** Serikali ifanye jitihada za makusudi kuhakikisha "sub-contractors" wote ambao walikuwa wanatoa huduma kwa mkandarasi wa awali wanalipwa fedha zao kwa wakati ili kuwaepusha na hatari ya kufilisika kutokana na kupanda kwa riba za mikopo waliyochukua kwenye mabenki.

3.3 Viwanda vya Kuzalisha Vifaa vya Umeme Nchini.

Uwezo wa uzalishaji wa viwanda vilivyopo unazidi mahitaji ya soko nchini na kwakuwa hata uzalishaji kwa ajili ya soko la ndani unafanyika bila ya wazalishaji kupata takwimu halisi za mahitaji kwa mwaka hivyo kushindwa kukadiria vyema mahitaji ya malighafi na kujipanga kwenye mizunguko ya uzalishaji, **Hivyo basi** Kamati inashauri Serikali kuvisaidia viwanda vyetu kutafuta masoko nje ya nchi kwa kuweka mkakati mahsuswi wa kuzishirikisha ofisi zetu za ubalozi kwenye ukanda wa Afrika mashariki na SADC; kufanya hivi sio tu kutawezesha bidhaa za viwanda hivi kupenya kwenye masoko ya nchi hizo bali pia itaongeza mapato ya kikodi kwa nchi yetu. **Vilevile**, Kamati inashauri REA na TANESCO kutangaza mapema mahitaji yao ya mwaka ya Mashine-umba ili kuwezesha viwanda hivi kujipanga na kuzalisha kwa ufanisi. **Sambamba na hili**, baadhi ya malighafi muhimu za kutengenezea Mashine-umba (Ambicant Catalyst, na GALVANISED Stranded steel wire) HS code zake uhitaji kulipiwa 'import duty' hivyo kuongeza gharama za uendeshaji na kuathiri bei ya bidhaa; **Na kwakuwa** mfumo wa ukaguzi bidhaa bandarini huchukua muda mrefu hivyo kusababisha malighafi kuchelewa, na viwanda kulazimika kusimamisha uzalishaji; **NA** kutopatikana kwa cheti cha mazingira kutoka NEMC kumesababisha kutopatikana kibali cha ubora wa

kimataifa ISO kwa kampuni ya Europe Inc Industries Ltd na hivyo kuathiri ushindani wa soko la nje ya nchi, **Kamati inaishauri** Serikali iangalie namna bora ya kushughulikia changamoto hizi kwa kushirikiana na mamlaka zingine za Serikali ili vibali na bidhaa ziweze kupatikana kwa wakati na bila vikwazo.

3.4 Bei ya Umeme Unaozalishwa na Wazalishaji Wadogo (SPPs/ Minigrids)

Serikali ilifanya uamuzi mahsusini wa kuwashirikisha wazalishaji wadogo wa umeme (Small Power Projects – SPP) kuwekeza nchini ili kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na umeme wa uhakika kutoka katika vyano mchanganyiko; **Na kwakuwa** wazalishaji wadogo waliitikia wito wa Serikali kuwekeza, Hivyo basi ili kulinda uwekezaji ambao tayari umefanywa na wazalishaji wadogo ambao wanahudumla zaidi ya wateja 100,000 hapa nchini; **Na vilevile** ili kuendelea kujenga imani kwa wawekezaji kuwa mazingira ya ufanyaji biashara hapa nchini yanatabirika, **Kamati inaona ipo haja** kwa Serikali kuharakisha mchakato wa kutafuta suluhu ya mkanganyiko uliopo sasa wa bei ya kuuzia umeme unaozalishwa na wazalishaji wadogo.

3.5 Kuvutia Uwekezaji Katika Sekta ya Nishati

Uandaaji wa miongozo ya kutangaza miradi inayotekeliza kwa kutumia vyano vya Makaa ya Mawe, Jua, na Upopo kwa njia ya ushindani ulikamilika tangu Oktoba 2018, na zabuni za miradi hiyo kutangazwa Novemba 2018 kwaajili ya kuzalisha MW 600 za makaa ya Mawe, MW 150 za Umeme wa Jua; na MW 200 za umeme wa Upopo, Kamati inasisitiza kuwa ni muhimu uchambuzi wa zabuni hizo ambao umechukua muda mrefu ukakamilika haraka ili ujenzi wa miradi hii uweze kuanza mwezi Oktoba 2020 na kukamilika mwezi Desemba 2021 kama iliyokusudiwa.

3.6 Matumizi ya Gesi Asilia Majumbani

Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya petroli (TPDC) imeanza kutekeleza miradi ya usambazaji wa gesi

asilia katika maeneo ambayo tayari kuna miundombinu wezeshi; **na kwakuwa** hadi kufikia mwezi **Februari 2020** tayari miundombinu yenye urefu wa **kilomita 10.8** imejengwa ikiwa na uwezo wa kuunganisha zaidi ya nyumba 10,000; **kwa mtazamo wa Kamati** kasi ya uunganishwaji gesi asilia majumbani hailingani na uhitaji uliopo, wala kasi ya uharibifu wa mazingira unaosababishwa na matumizi makubwa ya nishati ya mkaa nchini; **Hivyo basi** ili tuweze kunusuru nchi yetu na janga hili la uharibifu wa mazingira hatuna budi kuwekeza zaidi na kuruhusu sekta binafsi kushiriki katika miradi ya usambazaji na uunganishaji wa gesi majumbani.

3.7 Tahadhari ya Athari za COVID -19, Kuhusiana na Upatikanaji na Matumizi ya Mafuta Nchini;

Dunia inakabiliwa na changamoto kubwa ya ugonjwa wa Homa ya Mapafu (COVID -19); changamoto ambayo Taasisi mbalimbali za Utafiti za Kimataifa kama IMF, World Bank, UNECA, na Fitch Solutions zimetoa angalizo la uwezekano wa kutokea m dororo wa uchumi duniani, **Na kwakuwa** tayari dunia imeanza kushuhudi Sekta za Usafiri wa Anga na Utalii zikisimama, biashara na uzalishaji viwandani kushuka na hivyo kushuka kwa kiasi kikubwa kwa matumizi ya mafuta; na bei ya mafuta kwenye soko la kimataifa kuporomoka kwa kiwango kikubwa ambacho hakijawahi kushuhudiwa. Kufuatia mkanganyiko huu na mwenendo usiotabirika wa soko la mafuta ulimwenguni, ipo haja kwa nchi yetu kuweka mikakati thabiti ya kuhakikisha nchi inakuwa na akiba ya mafuta ya kutosha wakati wote; **Na halikadhalika** kutafakari namna bora ya kutekeleza miradi ya REA ambayo utekelezaji wake unategemea chanzo cha tozo kutoka kwenye mafuta yanayotumika nchini.

3.8 Kasi ya uunganishwaji wa wateja na huduma ya umeme; Serikali kufanya tathmini kuhusu kasi ya kuunganisha wateja waliolengwa kuunganishwa na huduma ya umeme kwakuwa makisio ya uunganishwaji wa wateja yanatakiwa kuwiana na hali ya uzalishaji wa umeme.

3.9 Utaratibu wa uagizaji wa Liquefied Petroleum Gas (LPG)

Matumizi ya Gesi ya LPG hapa nchini yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku. Hatahivyo gharama ya upatikanaji wake ni kubwa, hali inayosababisha bei kwa mtumiaji wa mwisho kuwa juu. Kamati inatambua kuwa kupitia agizo la Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dr. John Pombe Magufuli wakati akizindua hifadhi ya gesi ya kampuni ya Taifa Gas, Serikali kupitia PBPA ilianza mchakato wa kufanya majadiliano na EWURA, WMA, TPA, TRA na Wafanyabiashara wa LPG nchini ili kuweka utaratibu bora utakaokuwa na manufaa kwa pande zote. Kamati inashauri Serikali kuharakisha majadiliano hayo na kuja na mapendekezo yatakayowezesha gesi ya LPG kupatikana nchini kwa mfumo wenye tija kwa watumiaji na taifa kwajumla.

3.10 Usimamizi wa Wakandarasi wanaotekeleza miradi ya REA;

Bado zipo changamoto kadhaa katika miradi ya REA, Kamati inashauri Serikali kuendelea kuimarisha usimamizi wa wakandarasi wanaotekeleza miradi ya REA ili miradi hiyo ikamilike kwa wakati kama ilivyo katika matakwa ya mkataba; Aidha, ipo haja Serikali kuongeza wigo (scope) ya utekelezaji wa miradi hii kwani maeneo yanayoainishwa ni madogo ukilinganisha na uhitaji.

3.11 Udhibiti wa upotevu wa Mafuta katika miundombinu ya kupokelea mafuta;

Ili kuendelea kudhibiti upotevu wa Mafuta katika miundombinu ya upokeaji wa Mafuta, Kamati inashauri Kampuni zote za Mafuta zinazomiliki Hifadhi za Mafuta kufunga *flowmeters* kwa kila njia ya kupokelea Mafuta. Aidha, Serikali kupitia wakala zake wasimamie zoezi hili ili kuhakikisha linatekelezwa kikamilifu na kwa wakati.

3.12 Wigo wa kutoa huduma kwa wananchi wa mijini na vijiji;

Serikali iielekeze TANESCO kubuni njia bora zaidi ya kusogea huduma zake karibu na wananchi bila kutumia gharama kubwa kwani wateja wengi hususan wa sehemu za vijiji

wanakosa huduma kwakuwa maeneo yao hayajafikiwa na ofisi za TANESCO. 4.0

HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge, kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuliongoza Bunge hili Tukufu. Mungu awajalie afya njema, hekima na busara katika kutekeleza wajibu huu mkubwa tuliovakabidhi. Aidha, Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa Waziri wa Nishati Mhe. Dkt Medard Matogolo Kalemani, (Mb), Mhe. Subira Khamis Mgali, (Mb)- Naibu Waziri wa Nishati pamoja na Watendaji wote wa Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu Eng. Zena Ahmed Said kwa kusimamia vema shughuli za Wizara na kwa ushirikiano wao mkubwa kwa Kamati yetu wakati wote. Kwa namna ya pekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa weledi na umahiri waliouonesha wakati wote wa kutekeleza majukumu ya kamati. Kwa heshima kubwa naomba majina yao katika orodha ifuatayo yaingizwe kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge:-

1. Mhe. Dunstan Luka Kitandula, Mb - **MWENYEKITI**
2. Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri, Mb – **M/MWENYEKITI**
3. Mhe. Hamida Mohamed Abdallah, Mb
4. Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb
5. Mhe. Hamoud Abuu Jumaa, Mb
6. Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi, Mb
7. Mhe. Jesca David Kishoa, Mb
8. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb
9. Mhe. Ussi Salum Pondeza, Mb
10. Mhe. Mwantakaje Haji Juma, Mb
11. Mhe. Maryam Salum Msabaha, Mb
12. Mhe. Wilfred Muganyizi Lwakatare, Mb
13. Mhe. Kiza Hussein Mayeye, Mb
14. Mhe. Mohamed Juma Khatib, Mb
15. Mhe. Bahati Ali Abeid, Mb
16. Mhe. Msukuma Joseph Kasheku, Mb
17. Mhe. Yosepher Ferdinandi Komba, Mb

18. Mhe. James Kinyasi Millya, Mb
19. Mhe. Lameck Okambo Airo, Mb
20. Mhe. Suleiman Masoud Nchambi, Mb
21. Mhe. Zubeda Hassan Sakuru, Mb
22. Mhe Ally Mohamed Keissy, Mb
23. Mhe. John Wegesa Heche, Mb
24. Mhe. Frank George Mwakajoka, Mb
25. Mhe. Abdallah Ally Mtolea, Mb

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati Ndg. Ndg. Felister Mgonja na Ndg. Herman Berege na msaidizi wa Kamati Ndg. Grace Mwenye kwa uratibu mzuri wa shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya **Fungu 58** Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kama yalivyowasilishwa na mtoe hoja ambayo ni **Shilingi 2,488,289,499,000**.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Dunstan Luka Kitandula, (Mb)
MWENYEKITIKAMATI YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI
8 Mei, 2020

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

HOJA YA DHARURA

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya dharura.

NAIBU SPIKA: Hoja ya dharura kutokea Msekwa, Mheshimiwa Ally Saleh.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Tumesikia kwenye mitandao na mimi mwenyewe nimethibitisha kwa kuzungumza na watu kwamba linaandalifi zoezi la kwanza la aina yake kuwa-*evacuate* au *repatriate* Watanzania ambao wako nje na *specifically* kwa kesi hii ni wale ambao wako India.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ina ncha mbili ili kukushawishi ukubali ijadiliwe.

Kwanza, ni *aspect* ya kwamba ndege inayopelekwa huko imekodiwa na imekodiwa na mtu binafsi sijui ilikuwaje na imekodiwa kwa njia gani lakini imepelekea nauli kuwa kubwa kiasi ambacho inatishia kutokuwa *affordable* kwa watu ambao tayari wako India kwa miezi mitatu au minne kwa ajili ya matibabu na sasa wanataka kurudi nyumbani. Nauli imetoka dola 400 mpaka imefika dola 850. Hilo kwa kwanza, *affordability* inaweza ikawatanza Watanzania wengine wasiweze kuja kwa sababu ya bei. Hiyo ni kwa sababu kuna mtu amekodishwa ndege hiyo ya Tanzania ya Serikali ili kwenda kuwachukua Watanzania wale.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ni ya *humanitarian aspect*, unachukua watu 300 au 400 kwenye ndege ambao ni wagonjwa, wengine ndiyo kwanza wanaanza kupona lakini pia ambao wana *contagious disease possibly* ili uwalete nyumbani lakini hawajaambiwa wanakwenda moja kwa moja kwenye kambi au wanakwenda nyumbani kwa maana pia kuna tazito la *public health*. Hawajaambiwa wapime, hawajaambiwa lolote, wanaambiwa tarehe 11 ndege inafika, tarehe 12 ndege inarudi, hawakuambiwa wafanye lolote lile. Kama tunawaleta, tutawaweka wapi na kama wanakwenda nyumbani...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ally Saleh, ili tuweze kuokoa muda wa Bunge umeshaeleza maelezo ya kutosha, hoja yako ni nini kwa dakika moja.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ni kwamba nauli iliyotolewa ni kubwa sana watu hawa kuweza kurudi nyumbani, hiyo ni hoja ya kwanza. Hoja ya pili ni kwamba hawakuarifiwa kwamba wapime au wasipime wanaweza wakaja hapa na bado wakawa na *possibility* ya maradhi hali hiyo inakuwaje wakija hapa nyumbani *for public health reason?*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Ally Saleh ameeleza kwa mujibu wa Kanuni ya 47 inayompa fursa Mbunge ye yote kueleza kama analo jambo mahsus la dharura ili Bunge liweze kuacha kufanya shughuli ambayo inaendelea lakini lipate fursa ya kujadili jambo mahsus atakalokuwa amelileta Mheshimiwa Mbunge. Jambo hilo liwe mahsus na la dharura na muhimu kwa umma, ndiyo Kanuni ya 47 inavyoeleza.

Waheshimiwa Wabunge, lakini Kanuni ya 47 huwa inabidi isomwe na Kanuni ya 48 kwa sababu Kanuni ya 48 ndiyo inatoa masharti ya matumizi ya Kanuni ya 47. Sikusudii kuyarejea maelezo aliyotoa Mheshimiwa Ally Saleh kwa sababu sote tumeyasikia lakini anasema hoja yake anayoiita ya dharura amesoma kwenye mitandao kuhusu ndege iliyokodiwa kwenda kuchukua Watanzania walioko India lakini pia anaeleza kwamba ana wasiwasi sasa kwa sababu watu ambao wanatarajiwa kupanda kwenye hiyo ndege watakuwa wengi sana na hawajaambiwa wapimwe na hawajaambiwa wakija hapa watawekwa sehemu gani ama wataelekea huko waliko na wengine pengine wana magonjwa ya kuambukiza. Kwa hiyo, ameeleza maelezo marefu ambao sina haja ya kuyarejea.

Kwa masharti yaliyopo kwenye Kanuni ya 48 hasa ukisoma fasili ya (2) na (4) utagundua kwamba jambo hili hatutaweza kulijadili hapa. Ukisoma fasili ya (2) inakueleza kwamba liwe ni jambo mahsus iakini fasili ndogo ya (2)(c) inasema halikutolewa kwa kutegemea habari zisizo za uhakika au habari halisi juu ya jambo hilo hazipatikani au halihusu mambo ya kinadharia. Sitaki kuita ni la kinadharia,

ukisoma hii (c) peke yake inatosha kwa sababu mimi binafsi sijazisoma hizo taarifa.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, kwamba tutaanza kujadili jambo hili kwa kusikiliza tu habari ya mtu mmoja na ye ye amesoma kwenye mitandao hatuna hizo taarifa za kututosha kulipekelea Bunge kulijadili jambo kama hili. Hata hivyo, kama hilo jambo lipo na ni halisi niseme wazi sasa hilo halina uhusiano na jambo kuwa la dharura au siyo la dharura. Hoja ya mtu kusafiri kule alikokwenda inategemea alienda kufuata nini na hoja ya bei hata watu wote tunafahamu bei ya ndege hutegemea, huyu amepanda ndege hii analipa bei ile, ndege hazina bei moja. Kwa hiyo, hayo mambo lazima tuyatazame kwa namna hiyo. Watu wanafanya maamuzi binafsi ya kupanda hiyo ndege, sidhani kama kuna mahali wamelazimishwa. Kama nilivyosema sina hizo taarifa mahsus ikuhusu jambo hili na sizifahamu, kwa hiyo, itaniwia vigumu sana kusimamia hilo jambo kwenye mjadala hapa. Kwa hivyo, hilo jambo siyo la dharura kwa mujibu wa hiyo Kanuni ya 47 kwa hivyo sitaitoa hili Bunge litoe maamuzi. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, sitamuita Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa sababu taarifa yake haikuwa imewekwa mezani. Kwa namna hiyo, tumemaliza kusikiliza mawasilisho tutaendelea na uchangiaji na ninayo majina hapa ya Wabunge mbalimbali ambao wangepend a kuchangia kwenye hoja hili ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati. Tutaanza na Mheshimiwa Daniel Nicodemus Nsanzugwako atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mheshimiwa David Ernest Silinde ajiandae. Kila Mbunge atachangia kwa dakika 5 kwa sababu majina yako mengi hapa mezani.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWAKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nami nitoe pole nydingi kwa misiba yote iliyotufika hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini kwa namna ya kipekee, naomba kwa ruhusa yako dakika moja tu, nitoe shukrani zangu za dhati kabisa kwa Wabunge wote wa Bunge

hili ambao walipa moyo na faraja nilivyopata msiba mkubwa wa wadogo zangu wawili waliofariki kwa ajali ya gari. Waheshimiwa Wabunge nimepokea faraja zenu kwa mikono miwili, nasema ahsanteni sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee pia, naomba nimshukuru Spika na Katibu wa Bunge na wewe mwenyewe Naibu Spika kwa faraja zenu na msaada milionipa kuweza mimi kufika Kasulu kwa wakati na haraka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, kwa namna ya pekee sana kabisa naomba kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli kwa upendo wake mwingu, alinipa faraja na kwa kweli alinipa msaada mkubwa ulioniwezesha kufika Kasulu na kuhudumia msiba ule kwa muda na kwa haraka. Kupitia kwako na Waziri Mkuu uko hapa nipelekeeni salamu za upendo kwa Mheshimiwa Rais kwamba watu wa Kasulu tunampenda sana na ahsante sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu yeye binafsi kwa faraja zake kwangu wakati wa msiba huu. Salamu zako nilizipata nikiwa kule Kasulu, Waziri Mkuu nasema ahsante sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa ujumla niseme mmenipa faraja sana kwa kipindi hiki ambacho kilikuwa kigumu sana kwangu wakati wa msiba wa ndugu zangu hawa. Nawashukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niseme mambo machache tu. Nianze kwako Mheshimiwa Kalemani na Naibu wako Mheshimiwa Mgusu na watendaji wako, hongereni sana kwa kazi. Mmefanya kazi kubwa na nzuri sana na sisi watu wa Mkoa wa Kigoma tunaendelea kuwashukuru. Wewe Mheshimiwa Waziri binafsi pamoja na Naibu wako mmefanya ziara katika Mkoa wetu wa Kigoma zaidi ya mara mbili na uliweza hata kutufungulia kiwanda cha nguzo kubwa kilichopo katika Jimbo langu pale Kasulu Heru Juu. Hongera sana kwa kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema kweli Wizara hii mmeiteenda haki, mmeefanya kazi kubwa na mmeonyesha uwezo mkubwa. Ni matumaini yangu kwamba wananchi wa Chato na wananchi wa kule Pwani, kule Kisarawe, bila shaka watawarejesha mfanye kazi kubwa iliyobaki mpaka mwaka 2025 kama ambavyo na mimi Mbunge wa Kasulu Mjini najiandaa kukamilisha kazi mpaka 2025. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, nieleze mambo mawili tu ya harakaharaka. Ukurasa wa 22 wa hotuba ya Waziri nimefarijika sana sana umezungumza habari ya umeme wa Mto Malagarasi. Umeme wa Mto Malagarasi tumeusubiri kwa muda mrefu sasa takribani miaka 10 mpaka 15. Nimefarijika sana kuona mradi huu kwa 2020/2021 umetengewa shilingi bilioni 322. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri na ombi langu ni kwamba *m-fast track*, mfanye uharakaharaka hivi ili mradi huu sasa uanze kutekelezeka. Ni mradi wa siku nydingi sana na nina hakika hizi megawati 45 zikiingizwa kwenye gridi ya taifa zitakuwa zinajaziliza wingi wa umeme kwenye mfumo wetu wa gridi ya taifa. Bila shaka sambamba na mradi mkubwa huu wa Mwalimu Nyerere kule Rufiji, utakuwa *un-compliment* kuingiza umeme wa gridi katika nafasi hiyo. Mradi huo ni muhimu sana kwetu sisi watu wa Kigoma na taifa kwa ujumla.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa kengele imeshagonga.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWAKO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba dakika moja tu kwa sababu nilianza na salamu za misiba, naomba dakika moja kwa ruhusa yako.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nimewatangazia majina yako mengi sana hapa, haya dakika moja malizia.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWAKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie habari ya wakandarasi wa *REA*, *they are three, round one and round two*. Sisi Mkoa wa Kigoma wakandarasi wetu wa Kakonko na Kibondo na wa Kasulu, Kibondo, Buhigwa na Uvinza wamekwenda taratibu sana. Tunaomba kupitia kwako Waziri, muongeze *speed* ili wakandarasi hawa wakamilishe kazi hizi kwa muda ili tuingie kwenye uchaguzi ikiwa maeneo mengi yana umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. (*Makof!*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka atafuatiwa na Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah ajiandae.

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nami nianze kwa kutoa pole sana kwa wenzenetu ambao wametutoka katika kipindi hiki. Pia kwa sababu muda ni mchache sana, naomba nzungumze harakaharaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze pia kwa kupongeza Serikali kwa jinsi ambavyo kupitia Wizara ya Nishati wameweza kufanya kazi kwa kweli nzuri sana. Mheshimiwa Waziri wa Nishati pamoja na Naibu wako kwa kweli mmefanya kazi nzuri sana. Mheshimiwa Kalemani kule kwako niliona kuna wazee fulani waliandamana ili upite bila kupingwa wale wazee hawakufanya makosa. Tunakuombea uweze kupita ili kuja kukamilisha ungwe hii lakini wakati huo huo wewe umesoma Tabora naomba uniombee na mimi niweze kupita na kuvunja rekodi ya pale mjini maana pia nimefanya kazi nzuri sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nisiwasahau wananchi wangu wa Jimbo la Tabora Mjini kwa kuendelea kuniamini. Wamenipa ushirikiano mkubwa sana katika kipindi changu cha Ubunge. Niishukuru pia familia yangu akiwepo mke wangu pamoja na watoto wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu umeme ni tegemezi kubwa kwa viwanda vyetu, sasa hivi tunasema tuna uchumi wa kuendeleza viwanda, sasa hivi umeme kwa unit 1 ni karibu shilingi zisizopungua 250, kama wale wazalishaji wakubwa wa umeme watalipa lakini pia kuna wale wakwepaji wa umeme na mara nyingi ni wale watumiaji wenye matumizi makubwa, kama watabanwa na wakalipa hizi bili za umeme kwa wakati nadhani mapato yataongezeka na pengine mbele ya safari tukawa na *unit price* ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe shukrani moja kwa sababu sikuweza kupata nafasi ya kuchangia mradi wa maji, Tabora Mjini ni moja ya sehemu ambazo kwa kiwango kikubwa sasa haina shida ya maji. Naomba niipongeze sana Serikali na naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kutimiza ahadi yake ya Kumtua Mwanamke ndoo ya maji kwani ameweza kufanikiwa kwa kiwango kikubwa kwa Mkoa wa Tabora. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais, sisi Tabora sasa hatuna shida ya maji imebaki tu usambazaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la nguzo za umeme. Mheshimiwa Waziri bado kuna matatizo kidogo ya nguzo sehemu mbalimbali na hasa Jimbo la Tabora Mjini. Kuna maeneo hata ya Tabora palepale Mjini, kwa mfano, kuna maeneo ya Mpera, Uredi ni mjini hapohapo lakini nguzo ndiyo shida ya upatikanaji wa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa upande wa *REA*, Awamu ya Tatu sisi tuna vijiji 41 Tabora Manispaa ambavyo sehemu kubwa umeme wa *REA* haujafika. Naomba tafadhali uweze kutukumbuka na sisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme naunga mkono hoja kwa asilimia 100. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa David Ernest Silinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate ajiandae.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa dakika ni chache na mimi nitajikita kwenye hoja moja kwa moja. Nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii kuchangia hotuba ya Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Jimbo la Mombasa ambao walinichagua kuwa mwakilishi wao kwa miaka mitano na ambao nimewatumikia sasa kwa jumla ya miaka kumi, kuanzia mwaka 2010, leo wamenituma kushukuru kwa sababu maandiko yanasesma anayeshukuru anaongozewa zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati naingia mwaka 2010, Jimbo la Mombasa, hususani Mombasa ya sasa katika kata zote 14 tulikuwa hatuna umeme hata kata moja. Hivi tunavyozungumza leo umeme umefika kwenye kata kumi bado kata nne. Kwa hiyo, wananchi wa Kata za Kamsamba, Mpapa, Ivuna, Msangano, Mkangamo, Ndalambo, Ikana, Chitete, Kapele na sehemu ya Mkomba wanashukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejapata umeme na sasa hivi kule Mombasa walau mwanga upo, kwa hiyo, tunashukuru. Kwa hiyo, tunachohitaji sasa hivi Mheshimiwa Dkt. Kalemani, ujaribu kutufikishia umeme kama nilivyoleta maswali yangu na yale maeneo ambayo hamjafikisha na ahadi ya Serikali iweze kutekelezeka; Serikali ilisema umeme utafika kijiji kwa kijiji na kitongoji kwa kitongoji. Kwa hiyo, kwanza tumeanza kwa kushukuru lakini cha pili tunaomba sasa mjaribu kumalizia yale maeneo yote ambayo yamebakia ili wananchi wa Mombasa wafaidike na umeme wa REA. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la pili kwa kifupi sana, Mheshimiwa Waziri amezungumzia hali ya upatikanaji wa mafuta nchini. Ni jambo jema lakini napenda Serikali kwa wakati wa sasa itumie fursa ya kushuka kwa bei ya mafuta duniani ili kuongeza *reserve* ya mafuta nchini ili wakati mafuta yale yanapopanda juu ama wakati wa changamoto hizi za *Corona* zinapotokea basi sisi kama taifa tuwe tuna uwezo wa kujitegemea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ambalo napenda nilizungumzie kwa haraka ni mradi wa umeme wa Mwalimu Nyerere ambao unaendelea hivi sasa. Tunachokihitaji sasa ni kwamba Serikali haiwezi kujikita kuimaliza wote kwa wakati mmoja lakini tunahitaji sasa kuwepo na *phases*. Kuwe na *phase one* ambayo inaweza kuisha mapema kwa sababu ukiangalia kwa mfano sasa hivi kwenye Mradi wa *SGR* inakwenda spidi na inakaribia kuisha. *SGR* ni treni ambayo itakuwa inatumia umeme sasa lazima tuwe na umeme wa uhakika ambao unaweza kusaidia nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia takwimu ambazo nimepitia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, utaona katika miaka mitano malengo yetu ya kuzalisha umeme yalikuwa ni makubwa tofauti na hali halisi iliyopo. Bado Serikali haijajiwekeza zaldi kwenye miradi ya umeme ya *IPP* (*Independent Power Producers*).

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia mpaka sasa hivi *Independent Power Producers* nchini wanazalisha megawati 13.5 tu lakini maombi ya hao watu kuja nchini kuzalisha umeme, kwa mfano, umeme wa *solar* yaani kwa maana ya umeme juu, umeme wa upepo, ni watu wengi wanahitaji kuja kuwekeza nchini na hiyo ndiyo njia pekee ambayo inaweza kusaidia Serikali kuongeza umeme katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sasa hivi mimi ninachotaka ama ombi langu kwa Serikali ni kwamba wajaribu kupunguza ule ukiritimba ambao upo kwa sababu malalamiko makubwa ya hao watu wanaotaka kuja kuwekeza nchini kumekuwa na *bureaucracy* kubwa kiasi kwamba wanashindwa kuingia kwa wakati. Sasa tuwaruhusu waingie ndani halafu baada ya hapo sisi kama Serikali ndiyo iweze ku-control hao wawekezaji kwenye jambo hilo. Kwa hiyo, naamini kabisa wakiwekeza kwenye upande huo umeme utapatikana wa kutosha na Serikali haitajikita zaidi yenewe kuwa kama mzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, atafuatiwa na Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma ajiandae.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Naibu wake na Katibu Mkuu kuititia Wizara ya Nishati na timu nzima ya wataalam kuititia Wizara hii kwa kazi kubwa ambayo wameifanya ya kuendelea kuimarisha sekta hii ya nishati. Nipongeze sana Serikali kwa hatua mbalimbali ambazo wameendelea nazo kuhakikisha kwamba sekta ya nishati inaendelea kuimarika na kuleta mapinduzi makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuipongeza Serikali kwa kufanikisha uzalishaji wa umeme nchini lakini kuendelea kufanya tafiti mbalimbali na kusimamia majukumu mbalimbali ya uzalishaji wa umeme kuhakikisha kwamba Watanzania tunaendelea kupata huduma ya umeme. Pia uagizaji wa mafuta na kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata huduma hii ya mafuta bila kuwa na changamoto yoyote.

Meshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali kwa kufungua fursa ya uwekezaji wa viwanda. Leo tuna viwanda ambavyo vinatengeneza nyaya za umeme, transfoma na vifaa mbalimbali vyta umeme na kufanya wasambazaji wa umeme kupata vifaa kwa haraka na kwa bei nafuu. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya ya kuhakikisha kwamba uwekezaji nchini unaendelea kuimarika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie suala zima la REA. Katika kipindi hiki cha miaka mitano vijiji ambavyo vilikuwa ndani ya mpango wa REA ni 12,268. Vijiji ambavyo vimefikiwa na umeme mpaka dakika hii ni 8,726. Vijiji ambavyo vinaendelea kuweka miundombinu mbalimbali ya upatikanaji wa umeme ni vijiji 1,721. Ifikapo Juni, tutakuwa na vijiji 10,446. Haya ni mapinduzi makubwa katika sekta hii

ya nishati kuhakikisha kwamba kila eneo litakuwa limefikiwa na umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi katika Mkoa wa Lindi tumefaidika sana na mradi huu wa *REA*. Tulikuwa na vijiji 133 lakini vijiji 107 tayari vimefikiwa na umeme wa *REA* na vijiji 26 vilivyobakia viro katika mpango wa *REA* *III*. Kwa hiyo, tunaamini kwamba vijiji hivi ifikapo mwisho wa mwaka huu basi vyote vitakuwa vimekamilika kupatiwa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini si hivyo tu, leo ama kesho tenda inafunguliwa pale Masasi ya kununua kifaa cha *AVR* kitakachosababisha sasa Wanaliwale kupata umeme wa gridi unaotoka Songea lakini Wananchingwea watafaidika na umeme huu lakini hata kule Ruangwa watafaidika na umeme huu.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hamida, kengele imeshagonga.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru Shirika la *TPDC* kwa kutuletea fedha shilingi milioni 5.2 kwa ajili ya wafidiwa wa mradi wa *LNG*.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa, muda umekwisha.

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, atafuatiwa na Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma, Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi ajiandae.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi jioni hii ya leo kuchangia katika bajeti hii ya Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya

Bunge hili Tukufu kutoa maoni yangu mawili, matatu juu ya Wizara hii ya Nishati. Vilevile naishukuru Serikali ya Awamu ya Tano kwa niaba ya Wabunge wa Mkoa wa Ruvuma kwa kutuletea Gridi ya Taifa katika Mkoa wetu wa Ruvuma ambayo imeleta maendeleo makubwa katika mkoa wetu. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na pongezi hizo, kuna changamoto iliyotokana na hiyo Gridi ya Taifa kwa upande wa Tunduru ambapo tunapata umeme mdogo na kusababisha matatizo kwa wananchi wetu, wanaunguza vitu hovyo, hasa wakati wa usiku umeme unakuwa ni mdogo sana. Nashukuru nimeongea na Meneja wa *TANESCO* Mkoa, amenidhihirishia kwamba mchakato wa kuweka *AVR* pale Nandembo umeanza kufanyika. Naomba uendelee kwa kasi ili kupunguza adha hii ya watu wa Tunduru kuunguliwa na vitu vyao kila siku inapofika wakati wa usiku.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa upande wa *REA* jinsi Serikali ilivyofanya kuhakikisha kwamba vijiji vingi vinakuwepo katika mpango huu. Pamoja na vijiji hivyo lakini kuna changamoto ambazo zimejitokeza katika maeneo mengi katika Jimbo langu la Tunduru Kusini *scope* iliyokuwepo katika kugawa umeme kwenye vitongoji mbalimbali katika vijiji imekuwa ni changamoto kubwa sana. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa namna ambavyo amenipa ushirikiano na kunihakikishia kwamba vijiji vyangu vya Nalasi na Mchoteka kuanzia wiki ijayo programu ya kupeleka nguzo na kuanza kuzisimika utaanza. Nakushukuru sana kwa jitihada zako kwa sababu nimekusumbua kwa muda mrefu kwa sababu miji hii miwili ni mikubwa sana katika Jimbo langu la Tunduru Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, naomba hii Awamu ya *Tatu*, *Part Two*, naomba Waziri ueleze ni lini hasa itaanza. Kwa sababu orodha ya vijiji tunavyo lakini uhakika ni lini itaanza awamu hii bado haujawewe kupatikana. Naomba Serikali kama inawezekana basi hii *Phase III* basi wapewe wale ambao wapo *site* sasa hivi kupunguza gharama ya mchakato kuanza upya ili shughuli isiweze

kusimama na lengo letu litimie la mwaka 2021 Julai vijiji vyote kuwa na umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kwenye *REA*, vile vijiji ambavyo vina umeme kumekuwa na changamoto ya *scope* kiasi kwamba mitaa mingi haina umeme. Kwa hiyo, suala la ujaziliaji wa umeme katika mitaa iliyokosa ni muhimu sana ili kuhakikisha kwamba kila kitongoji kinafaidika na miradi hii ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo naomba kulizungumzia ni madhara ya *Corona* katika sekta ya mafuta. Sekta ya mafuta haikuachwa katika janga hili la *Corona*. Sasa hivi biashara ya mafuta imeshuka sana, kwa asilimia kubwa mauzo kwenye vituo yameshuka kutokana na matumizi ya mafuta kwa watu binafsi yamepungua na mafuta yale yaliyokuwa yanaenda nje magari mengi yamezuiliwa. Naomba Serikali iangalie namna ya kuwasaidia hawa wauzaji wa mafuta ya jumla na rejareja ili kuwawezesha kukabiliana na hali hii ambayo imejitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia 2015 mpaka leo *EWURA* wanapanga *margin* ya *retail price* ni Sh.105 kwa lita. Kutokana na m dororo huu uliotokana na *Corona* ambapo mauzo yameshuka maana yake wauzaji wengi watalazimika kuwapunguza wafanyakazi ili kukidhi mahitaji ambayo yatakwenda sambamba na mapato wanayopata kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Maftaha Abdallah Nachuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia ajiandae.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nami nikushukuru kwa kunipa nafasi, nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu-Wataala* kwa

kuendelea kutujalia afya njema, tunaendelea kupambana na *Corona*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaongea mambo matatu kwa harakaharaka kwa sababu ya dakika zangu kuwa ni chache. Kwanza, nimshukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii, kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana na hawa watu ni wasikivu sana na ukiwaendea wanakushauri na mnashauriana vizuri. Mheshimiwa Subira na Mheshimiwa Waziri, Dkt. Kalemani pongezi kwenu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza pamoja na pongezi hizo, nimezungumza ndani ya Bunge lako hili Tukufu kwa muda mrefu sana kwamba Mtwara Mjini kuna mitaa ya pembezoni ambayo nimekuwa nikiitaja kila mwaka, mpaka mingine unaifahamu kwa majina kwa sababu nimekuwa narudia ndani ya Bunge hili lakini mpaka leo ni mtaa mmoja tu ndiyo umepelekewa umeme ambao ni wa Mbawala Chini, bado maeneo ya Mkunjanguo, Mkangara, Dimbuzi na Namayanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nazungumza na Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa muda mrefu sana. Bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri anaifahamu mitaa hii, kuna wakati alitumwa na Mheshimiwa Waziri akaja pale Mtwara Mjini kwenye Mtaa wa Mkangala na akawaambia wale wananchi kwamba hii mitaa ya pembezoni tuna mradi wa umeme unaitwa ujazilizo. Mpaka leo ile mitaa mpaka pale alipofika Naibu Waziri bado hawajapeleka umeme. Juzi nilikuwa nazungumza na Mheshimiwa Waziri hapo nje akaniahidi kwamba nawaagiza. Sasa Waziri amekuwa akimuagiza Meneja wa *TANESCO* wa Mtwara lakini mainjinia pia wamekuwa wakiagizwa, yale ambayo wanamwambia Waziri wanamuongopea kila siku. Kwa sababu mara nydingi kawaagiza lakini maeneo haya hawapeleki umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi leo naomba nishauri Bunge lako Tukufu, Mheshimiwa Dkt. Kalemani amuondoe *Engineer* pale Mtwara kwa sababu amekuwa akitoa kauli za uongo kila siku. Tunaomba atubadilishie atuletee *Engineer*

mwingine. Akimuagiza peleka umeme na anatoa taarifa za uongo kwamba tayari tumeshapeleka kumbe walichofanya ni kudonoa tu sehemu moja wakapeleka Mbawara Chini wakaacha Naulongo Mkunjanguo, Namayanga, Mwenge na Dimbuzi. Mpaka leo nimekuwa nalia ndani ya Bunge hili, maeneo haya ni maeneo yaliyopo Manispaa ya Mtwara Mikindani. Mheshimiwa Waziri atakavyohitimisha atueleze lini hasa atapeleka umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo naomba kuzungumza kwa harakaharaka, tunashukuru sana Mheshimiwa Waziri amesema kwamba tumepeleka umeme wa Gridi ya Taifa Mikoa ya Kusini; Mtwara, Lindi na Ruvuma. Ni kweli na Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja kuzindua pale Mahumbika, Lindi. Mheshimiwa Waziri Mkuu alielezwa kwamba umemesana Mtwara, Lindi na Ruvuma hautakuwa unakatikakatika lakini ni jambo ambalo ilimekuwa tofauti kabisa na imekuwa ni kinyume.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ukikaa Mtwara na nimuombe Mheshimiwa Waziri afanye ziara ya siri, kimyakimya tu aje pale Mtwara tumtafutie hoteli akae kimyakimya aingie usiku amuone Mbunge wa Mtwara Mjini halafu mimi nimwambie lala hapa halafu aone umeme unavyokatika Mtwara, kila siku umeme unakatika usiku na mchana, kwa siku unakatika mara kumi, mara ishirini mpaka mara thelathini. Sasa sisi tunashangaa tulikuwa tumeshukuru sana kwamba Mtwara na Lindi sasa tatizo hili la kukatikakatika umeme litakuwa halipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri pia mimi pale Lindi ni nyumbani, ukitoka Mtwara ukienda Lindi pale Mitwero umeme unakatika kila siku zaidi ya mara kumi, mara ishirini. Sasa lile suala ambalo Mheshimiwa Waziri alitueleza kwamba Gridi ya Taifa imekuja kuwa ni mkombozi wa Mikoa ya Kusini, bado mpaka leo kuna tatizo la kukatikakatika kwa umeme. Naomba kujua tatizo hasa ni kitu gani; ni mitambo au ni nguzo zilizoletwa kule Kusini kwamba ni ndogo kama zile za kujengeta nyumba au tatizo ni nini? Kwa sababu wakati mwingine ukiwaliza wale wataalam wanatuambia kwamba mvua

zikinyesha nguzo zinadondoka basi tuwekewe nguzo kubwa na za chuma kwa sababu Gridi ya Taifa inabeba umeme mkubwa.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Tunaomba sana hayo Mheshimiwa Waziri ayashughulikia katika Mikoa ya Mtwara na Lindi. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia, Mheshimiwa Wilfred Muganyizi Lwakatare ajiandae.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa fursa hii. Nitumie fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunipa zawadi hii ya uhai na kuendelea kuwasemea wananchi wa Ukerewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati, Naibu wake, Katibu Mkuu na watendaji wengine kwenye Wizara kwa kazi kubwa sana wanayoifanya kuhakikisha kwamba taifa hili kweli tunafikia ile azma ya kutengeneza nchi ya viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii vilevile kumpongeza sana Meneja wa *TANESCO* wa Dodoma hapa, amekuwa anafanya kazi kubwa sana. Kuna baadhi ya maeneo tulikuwa na shida ya umeme lakini kwa muda mfupi angalau ameweza kuyafanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii imefanya kazi kubwa sana na wanastahili pongezi. Tukiangalia taarifa yao katika vijiji zaidi ya 12,000 viliviotakiwa kupata umeme kwa kutumia mradi wa *REA* mpaka sasa zaidi ya vijiji 9,000

vimepata umeme, ni kazi kubwa sana ambayo inahitaji kupongezwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo letu la Ukerewe katika vijiji 76 ni vijiji tisa tu ndiyo havijapata umeme, ni hatua kubwa sana. Kwa fursa hii nimshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa maono na uamuzi wake wa kuhakikisha kwamba vifaa vinavyotumika kwenye miradi hii vinatengenezwa hapa nchini. Jukumu tulilonalo sasa ni kuwezesha viwanda hivi viweze kuzalisha malighafi za kutosha kuweza kustahimili mahitaji ya soko ambalo ni sisi wahitaji wa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kutoa changamoto mbili ambazo ningeomba Wizara itusaidie. Kwenye eneo la Ukerewe kuna tatizo kubwa sana la kukatika kwa umeme na tatizo hili kwa miezi takribani mitatu limesababisha matatizo makubwa sana na hasara kubwa kwa wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla wake kwenye eneo la visiwa vya Ukerewe, lakini chanzo chake hasa ni kwasababu, ile *cable* inayotoka Lugezi kwenda Kisolya imechoka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru Wizara, Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Waziri na watendaji wengine mmekuwa mnanipa sana ushirikiano. Na nipongeze kazi inayofanyika sasa pale kuweza kurekebisha ile hali. Lakini suluhisho la kudumu kwenye eeo hili niombe Mheshimiwa Waziri, kama ulivyoniahidi, inunuliwe sasa *submarine cable* ili iweze kuwekwa pale tatizo lilloloko pale liweze kuondoka, lakini kama tusipopata *submarine cable* kuweza kuweka pale lile tatizo litaendelea kwasababu, hivi sasa kwa takribani miezi mitatu umeme unakatika karibu mara mbili mara tatu kwa siku, wakati mwagine siku tatu siku nne Visiwa vya Ukerewe vinakuwa havina umeme, jambo linalosababisha hasara kubwa na usumbufu kwa Wananchi wa Visiwa vya Ukerewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niiombe Wizara katika bajeti hii, Mheshimiwa Waziri kama ulivyoniahidi,

tuhakikishe kwamba, ile *cable* inapatikana tuweze kuondoa tatizo lilitopo. Hatua zilizochukuliwa hivi karibuni kuleta nguzo za chuma kuweza kuvusha lile eneo ni hatua nzuri, nipongeze na ninaamini kwa utaratibu wa muda angalau hii inaweza kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo nilitaka nilizungumzie ni juu ya maeneo ambayo yako *off grid*, hasa maeneo ya visiwa ambapo kuna wakandarasi walipewa jukumu la kusambaza umee kupitia mifumo ya jua na mingineyo. Kuna baadhi ya maeneo sawa yamepata umeme, lakini maeneo mengine wale wakandarasi walipewa jukumu la kusambaza umeme wamesimika nguzo, lakini bado hawajamalizia kazi ile kwa hiyo, sijui tatizo ni nini, lakini nikuombe uweze kuwasukuma wamalizie kazi ile ili wananchi waweze kupata umeme kama ambavyo tulikuwa tunatarajia. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye yale maeneo ambayo tayari yana umeme kama Visiwa vya Ukara, Ilugwa, na kadhalika, zile gharama za umeme ule zilikua ni juu sana ukilinganisha na umeme wa kawaida wa gridi ya Taifa. Nikupongeze Mheshimiwa Waziri na watendaji wengine kwa juhudzi mlizozifanya kuhakikisha kwamba, gharama hizi angalao zinaweza kushuka, basi dhamira ile iweze kufikiwa ili wananchi wa visiwa hivi, hasa vya Ukara, Ilugwa na kwingineko ambako wanapata umeme kupitia makampuni kama Jumeme, na kadhalika, waweze kuupata katika mazingira ambayo angalao ni bei ambayo ni *affordable* kuliko ile ambayo walikuwa wanailipa hapo mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache kwa dakika hizi chache nashukuru sana kwa fursa hii. Mwenyezi Mungu akujalie sana, nashukuru. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Juma Seleman Nkamia, atafuatiwa na Mheshimiwa Wilfred Muganyizi Lwakatare, Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi ajiandae.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitoe shukrani zangu za dhati kabisa kwa Serikali hii ya Awamu ya Tano kwa juhudi kubwa zinazofanyika za kupeleka umeme katika maeneo ya Tanzania nzima. Ni kazi kubwa na inafanyika vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kalemani, Naibu wake dada yangu Mheshimiwa Subira na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri inayofanyika. Leo katika Wilaya ile ya Chemba mimi najivuna kuona kwamba, katika vijiji 114 vya Wilaya ya Chemba vyote vipo kwenye orodha ya kupata umeme. Nikushukuru sana Mheshimiwa Waziri tumeshakwenda mara mbili, kazi iliyobaki sasahivi pale Mombose na Bubutole kuvusha zile nguzo ili ziende pale Poro Banguma na kuwashaa umeme pale kwa Mtoro inaendelea. Yale maji pale Mto wa Bubutole pale yameshapungua ningeomba kazi hiyo ifanyike kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili niruhusu niwapongeze sana meneja wa mkoa, *zonal manager* na mhandisi wa umeme pale Chemba, *Engineer Mwalyambi* kwa kweli, kijana yule anafanya kazi nzuri sana. Jana nilikwenda pale tumezungumza kwa kirefu sana kwa kweli, Mheshimiwa Waziri nikuombe yule kijana muacheni kwanza atumalizie ile kazi pale msije mkamtoa na mkimtoa sana sana mpandisheni cheo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe rai tu kwa Serikali katika baadhi ya maeneo; yapo maeneo ambayo kuna umeme kwenye kijiji, lakini baadhi ya vitongoji ndani ya kijiji kile hayana umeme. Kwa mfano, ukifika pale Waida unakuta kitongoji cha Shali chenye watu wengi zaidi hakina umeme, umeme umefika pale *centre* tu. Nilikuwa nadhani hayo ni maeneo ambayo mngeweza kuyaangalia. Lakini pia nilikuwa nataka nitoe rai kwenu kwenye Kata zile za kule Wilaya ya Chemba, Lahoda, Ovada, Sanzawa, Mpendo, Babayu na

Makorongo, kwenye Kata ya Makorongo Babayu kazi imeanza, nikuombe Mheshimiwa Waziri uongeze juhudui dogo ili waweze kumalizia zoezi hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu mwingine, yapo baadhi ya maeneo nguzo zinakaa kwa muda mrefu sana. Kwa mfano ukienda kule Chemba pale Ombiri kuja mpaka Mwailanje mpaka Wisuzaje nguzo zimechimbiwa muda mrefu sana, lakini bado kazi ya kuwashaa umeme inachukua muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kwa kweli, niipongeze sana Wizara hii, msema ukweli ni mpenzi wa Mungu. Kama kuna kazi ambayo Mheshimiwa Kalemani hata kesho ukitangulia mbele ya haki watu wa Tanzania watakukumbuka ni hii kwenye *issue* ya umeme, umefanya kazi kubwa sana na nakuombea kwa Mwenyezi Mungu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na niwashukuru Wananchi wa Chemba, ni mzima kama mnavyoniona, niko hai kabisa, haya maneno mengine yapuuzeni;

NAIBU SPIKA: Ahsante!

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umeisha. Asante sana, Mheshimiwa Wilfred Muganyizi Lwakatare, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati ajindae.

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Mheshimiwa Naibu Spika, napata changamoto ya dakika tano, lakini nitajitahidi kwa sababu, nieleze kabisa usiku wa kuanzia jana mpaka leo sijalala kwasababu, nilijiruhusu mwenyewe kwamba, simu iwe wazi nimpokee kila mmoja atakayenipgia na nimjibu kila mmoja atakayenihoji. Kwa hiyo, nimepata simu toka Tanzania nzima na hususan mkoani kwangu wakiwa wana tataruki ya

kusema Mheshimiwa Lwakatare amefanya mapinduzi ya kupata u-KUB.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme mpaka dakika hii nashangaa huyo aliye-*spin* madhumuni yake ni yapi, lakini ukweli wenyewe hakuna mapinduzi yoyote. Suala lililofanyika tu na wenzangu ambao wako humu ni kwamba tulitaka tusikae humu ndani kama kuku wa kienyeji ambaye amechukuliwa Rungwe akaletwa sokoni Mbeya, akachomoka kutoka kwenye tengä akaanza kutaharuki mazingira ya sokoni, hajui ameletwa na nani, hajui maetokea wapi, njia ya kurudi kule ni wapi, hajui hatima yake ya kuwa pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi na wenzangu tukatimiza ule wajibu ambao tuliupata midhalii kwamba, ili tunapoingia ndani ya Bunge hili tukaleta vikaratasi kuomba kuchangia tuna hatari ya kuwaletea corona hapo Mezani. Kwa hiyo, tukashauriwa mionganoni mwetu wawepo watu wa kupokea majina kutoka upande wetu na tunawasilisha Mezani, ili Kiti na Meza iweze kupanga sawasawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na ndio maana sisi viongozi wetu tunawaheshimu kwelikweli na tunawapenda, lakini katika masuala mengine ambayo yanasmamiwa na *three line whip* ambapo unaangalia masuala ya Kitaifa, unaangalia masuala ya chama chako, unaangalia na *self consciousness* yako na hiyo shule nilipigwa mwaka 2000 wakati wa Bunge la Mheshimiwa Msekwa kwa hiyo, nilliiva na ninatambua hivyo. Na mara nyangi na Waheshimiwa wananjua, hata waliokuwa *CUF*, mimi huwa nasimamia nafsi yangu na huwa sitaki kuwa mtumwa wa nafsi kwa hiyo, na nitaendelea kuwa hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na ndio maana pamoja na kwamba, kumebaki muda mchache, wiki chache, mimi nilishaaga. Sikutaka nitoke ndani ya Bunge hili nikiwa mnafiki kwa kuamini nisichokiamini, ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja kwenye hoja iliyoko humu ndani. Mimi ni Mjumbe wa Kamati, kazi ya Waheshimiwa Kalemani na watendaji wenzake na Naibu Waziri naiheshimu ni watu ambao wanafanya kazi si wabishi. Ni watu wanaosikiliza maoni kiasi kwamba, kero zote tulizokuwa tunazungumzia, sehemu kubwa Waheshimiwa hawa wamekuwa wepesi wa kuzipokea na kuzifanyia kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo moja ambalo nataka nilizungumzie ni suala la madeni ya wakandarasi. Imekuwa sehemu sugu ya kuzorotesha kazi, kuwakatisha tamaa wakandarasi, tena kwa mara ya kwanza Wizara hii ndio imeonekana inajali wakandarasi wa humuhumu nchini na kuwaheshimi, lakini suala la kuwalipa limekuwa kizungumkuti.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hata pale kamati ilipomuagiza Waziri, tuletee wakandarasi tuzungumze nao kwa nini kazi zinazembea, Waziri mpaka sasa tunamaliza kazi yetu ya kamati hakuweza kufanya hilo. Yeye anajua alikokwama ni wapi, lakini tunasema wakandarasi wana malalamiko makubwa, hawalipwi, matokeo yake hawaaminiwi na mabenki, matokeo yake hawaaminiwi na *suppliers*, wakati hawaaminiwi hata na wananchi huko wanakofanyia kazi kwasababu wanakopa vyakula, hawaaminiwi na wafanyakazi wao ndani ya makampuni kwasababu, hawalipi mishahara, matokeo yake kazi zote zinazembea. Kwa hiyo, Waziri hilo ujaribu kuliingilia umeshindwa kupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa la mwisho mfano mzuri ni kampuni ya *urban Rural Engineering Limited*. Hii kampuni ilikuwa chini ya Mkurugenzi marehemu Awadh Zuberi Athumanli aliyeefariki wiki kama tatu zilizopita. Familia yake kwasababu, naongea naye, wanasema sehemu ya kifo chake kimetokana na kudaiwa. Anadai zaidi ya bilioni 4.5 na pia Dola za Kimarekani laki tatu na nusu; sasa wanasema wao kifo cha marehemu kimesababishwa na madeni kwa sababu, kwa miaka miwili mfululizo amekuwa anapiga safari,

anakuja Dodoma, mara waseme anayehusika yuko Dar-es-Salaam. Jamani, mlipeni marehemu madeni, sasa hivi ni mtafaruku mkubwa kwenye familia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nataka kuwaambia wenzangu waliopo huku...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa kengele imeshagonga.

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Mheshimiwa Naibu Spika, dakika moja kama nilivyoomba. Namalizia kwa kusema, nitoe ushauri kwa wenzangu CHADEMA kwamba, tuna kazi kubwa hatupaswi kugawana mbao bado tuko katikati ya ziwa. Lakini nina uzoefu kwenye vyama vyaa ulinzi nimekuwa Mkurugenzi wa Ulinzi ndani ya CHADEMA na wakati ule *CUF*. Ku-retreat kamwe sio kushindwa vita, viti vyaa KUB na uongozi wetu vyote bado viko wazi wala hata hatujavichukua, lakini ku-retreatsio kuogopa vita bali ni kurudi kujipanga upya unaweza ukapambana na vita zaidi. Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Haya, asante sana. Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige ajiandae.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia kwa niaba ya wananchi ninaowawakilisha. Kwanza nianze kwa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii kwa kazi kubwa ambayo wamefanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini napongeza, kwasababu wakati naanza ubunge 2010 Jimbo langu zima la Bukene kulikuwa hakuna hata kata moja, hata kijiji kimoja, hata kitongoji kimoja chenye umeme, lakini leo hii ninasimama hapa kifua mbele kwasababu, katika kata 17 za Jimbo langu la Bukene umeme umeshafika kwenye kata 13. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumebakiza kata nne, Kata ya Igusule, Kamalanga, Karitu na Isagehe, lakini hii Kata ya Igusule ninafahamu kwamba, inakwenda kupata umeme kuititia huu mradi wa bomba la mafuta kutoka Uganda kwenda Tanga kwasababu, hapo Igusule ndipo itajengwa kambi kubwa ya kuyaandaa mabomba kabla hayajafukiwa kwa hiyo, pale nina uhakika umeme unakuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe tu Wizara sasa ifanye utaratibu wa kuhimiza, ili kata zilizobaki hizi Kamalanga, Karitu na Isagehe. Ninajua ziko kwenye mpango na tulikuwa na changamoto ya *speed* ya mkandarasi, lakini ninamuamini Mheshimiwa Waziri kwa uwezo wa kufuatilia. Nakumbuka hata wakati tunawasha pale Kijiji kikubwa cha Mwamala Mheshimiwa Waziri Kalemani alikuja jimboni na alikaa siku mbili *physical* kumsimamia mkandarasi mpaka umeme ukawaka pale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Waziri naomba nikukumbushe unisaide kusukuma ule umeme wa Mwamala unatokea Itobo, pale katikati ya Itobo na Mwamala kuna kijiji kikubwa cha Lububu ambacho kuna taasisi muhimu pale, kuna Parokia ya Kikatoliki kubwa pale, kuna misikiti, kuna shule, kuna zahanati. Na ulipofika pale ulipokuja kuwasha Mwamala ulitoa maelekezo kwa REA na mkandarasi kwamba, *transformer*ishushwe pale kwasababu, umeme umepita pale, shida ni kushushwa *transformer*ili taasisi na wananchi wa kijiji kile waweze kupata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nakuomba maelekezo yako uyaklumbushie kwa REA kwamba, Kijiji cha Lububu ambacho kiko katikati ya Itobo na Mwamala kishushiwe *transformer* kwasababu pale ni kushushwa tu *transformer* lakini umeme umepita pale na ulitoa maelekezo hayo ulipokuja kuwasha umeme pale Mwamala.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna kijiji cha Sigili, sera yetu ni kwamba, umeme unapofika kwenye kata au kijiji, taasisi muhimu kama zahanati, shule, zipewe kipaumbele,

lakini pale Sigili, Kata ya Sigili umeme umefika, lakini haujafika kwenye hizi taasisi. Tuna zahanati pale umeme haujapelekwa zahanati, tuna shule na taasisi nyingine, makanisa na misikiti umeme haujafika kwenye hizi taasisi. Kwa hiyo, naomba maelekezo yako kwasababu, tumekuwa tukifua tililia, lakini *response* sio kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri sisi katika Jimbo letu la Bukene sasa wakati tukisubiri mpango wa kujaziliza, kama ambavyo wenzangu wamesema pamoja na kwamba, umeme umefika kwenye kata, lakini kuna baadhi ya vijiji, baadhi ya vitongoji ambavyo umeme haujafika. Na ninafahamu kwamba, kuna mpango mahususi wa kujaziliza kuhakikisha kwamba, vitongoji vyote na vijiji vyote vinapata kwa hiyo, hili tunaomba lihimizwe, lakini tunajipanga sasa kuhakikisha kwamba, umeme huu sasa unaongeza thamani ya mazao ya wakulima. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Bukene tumeamua sasa hatutaki kuuza mpunga, tunataka kuuza mchele. Tutaukoboa wenyewe kwasababu, miaka yote mchele mwangi unaolimwa tumekuwa tukiusafirisha kupeleka Kahama kukoboa na faida walikuwa wanapata watu wa Kahama, lakini kwa ujio wa umeme sasa mpunga wa Bukene tutaukoboa wenyewe tutaongeza thamani wenyewe, hatutauza mpunga tena tutauza mchele. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja asilimia 100, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige. Atafuatiwa na, aah, Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati atafuatiwa na Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige. Mheshimiwa Joyce Bitta Sokombi atachangia kwa dakika tatu, ajiandae.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kunipa nafasi, nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa mambo yote ambayo amenitendea kwa kipindi chote nilichokuwa hapa bungeni, nasema ahsante sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikupongeze sana kwa kazi nzuri ya hapa ndani ya Bunge na nje ya Bunge kule Mbeya, hongera sana. Naomba nitoe pole kwa Wabunge wenzetu wote waliotangulia mbele za haki, nasema wao mbele sisi nyuma, Mwenyezi Mungu aendelee kuwabariki huko waliko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuongea naomba niungane na wote waliompongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa hotuba yake ya tarehe tatu mwezi wa tano ambayo, iliyotuondolea uwoga, hofu na kuamsha ari mpya ya mapambano dhidi ya gonjwa hili la corona. Mheshimiwa Rais wetu kwa sasa amekuwa gumzo katika vyombo vya habari vya Kitaifa na vya kimataifa na ni kiongozi anayeheshimika duniani kote kuwa na msimamo usiroyumba na anayesimamia lile analoliaminia. Watanzania tuna kila haki ya kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu na kujivunia ushupavu wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Waziri Mkuu wetu ambaye kwa kweli, amekuwa ni mlezi mzuri. Wananchi wa Iringa, hasa wazee wanasema kwamba, Mheshimiwa wataendelea kukuombea wanakumbuka ulivyokuja kufanya kazi nzuri sana pale Iringa na Mwenyezi Mungu akubariki sana kwa kazi ya wazee. Lakini pia Mheshimiwa Janeth Magufuli amefanya kazi kubwa sana ya wazee, na ye ye kwa kweli, huko aliko mpeni salamu tunampongeza na tunakumbuka yote anayoyafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye hoja, nianze na mchango wangu kwa kumpongeza Waziri Dkt. Kalemani, kwa kazi nzuri mno. Naibu Waziri wake Mheshimiwa Subira Mgusu ametu wakilisha vizuri sisi wanawake wenzie, hongera sana. Wakati wote wako tayari, wamemu wakilisha vizuri sana Mheshimiwa Rais kwa kweli, hakufanya kosa kuwaweka pale mlipo na tunawa ombeeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza Shirika la *TANESCO*, kwa kipindi kifupi limeji endesha kwa faida.

Tumeona upatikanaji wa umeme wa uhakika majumbani mwetu na kwenye maofisi, hongereni sana. Tumeona kuitia miradi hii ya *REA* Serikali imeweza kufikisha umeme kwenye vijiji 9,112 sawa na asilimia 85, hongera sana. Niwapongeze Mkao wa Iringa *TANESCO*; Mkao wangu zaidi ya vijiji 45 wameweza kupata umeme wa uhakika katika vijiji hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya muda mfupi sana umeme umeleta mapinduzi makubwa sana nchini kwa sababu umeme ni maendeleo. Umeme ni maisha bora na umeme ni ajira. Tumeona Serikali imeweka vipaumbele katika Taasisi, kwa mfano Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati. Sasa Vituo vya Afya vimeweza hata kufanya upasuaji. Tumeona vifo vya akina mama na watoto vimepungua kwa sababu ya kuweka huo upasuaji na Mheshimiwa Waziri amesema. wananchi wa Iringa wamenituma, kama wewe ulivyo kwenye Jimbo la Mbeya...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. RITTA E. KABATI: Nichangie dakika moja tu.
(Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vijiji vilikuwa vipatiwe umeme wa miradi ya *REA*, lakini wakati wa upanuzi wa miji, vikaingia kwenye Halmashauri. Kwa mfano, Jimbo la Iringa, Mchungaji Msigwa kaondoka hapa, hajatenda haki. Sasa naomba tu nitaje baadhi tu baadhi ya vijiji ambavyo vinatakiwa vipatiwe...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nawe unajua uchungu wa Jimbo la Iringa. Kwa Jimbo la Iringa Mjini, Kata ya Nduli, kuna Mtaa wa Msisina, Mtaa wa Msalagala, Mtaa wa Kisowe na Mtaa wa Kipulupulu. Kata ya Kitwili kuna Mtaa wa Kitwili A, Mtaa wa Uyole, Mtaa wa *Block J*, Mtaa wa Uyole; Kata ya Mkwawa, kuna Mtaa wa Lukosi, Mtaa wa Mtamba, Mtaa wa Mgela,

Mtaa wa Hoho. Wananchi wa Iringa wasionje tena sumu kwa sababu leo hii haya mambo angeyafanya Mbunge wao wa Jimbo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na ninaunga mkono na nitachangia kwa maandishi. Ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, atafuatiwa na Mheshimiwa Joyce Bita Sokombi na Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza ajiandae.

Mheshimiwa Maige, huko Msekwa. Mheshimiwa Joyce Bita Sokombi, dakika tatu, atafuatiwa na Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza na Mheshimiwa Justin Joseph Monko, ajiandae.

MHE. JOYCE B. SOKOMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kupata nami wasaa huu niweze kuchangia Wizara hii ya Nishati. Kwanza kabisa kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama katika kipindi hiki, niweze kutoa pole kwa ajili ya wenzetu waliotangulia mbele ya haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa sisi wenyewe tulipo tuweze kujilinda kwa kufuata maelekezo ya wataalam wetu na kikubwa pia waendelee kutoa elimu juu ya ugonjwa huu wa *Covid - 19* kwa sababu mpaka leo wengine hawajaelewa ugonjwa unatokana na nini. Maana ukitembea maeneo ya masoko wengine watakwambia kwamba ugonjwa huu unatokana na sehemu ambazo zina *G5*, wengine wanassema kwamba ni kutockana na kufanya ngono kwa sana ndiyo maana unapata ugonjwa huu. Kwa hiyo, tunaona kabisa elimu haijafika sehemu nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu kusema kwamba Mheshimiwa Waziri kweli anafanya kazi kubwa sana, lakini nimwambie tu ukweli, Wakandarasi wanamwangusha. Hii yote ni kwa sababu hawalipwi kwa wakati. Wangkuwa wanalipwa kwa wakati, tunaamini kwamba kazi zingekuwa zinaisha kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi wamekuwa wakilalamika sana kuhusu kulipia nguzo kwa sababu unakuta usipotoa hela kidogo kulipia nguzo, inakuwa ni shida, wakati Serikali inasema kuwekewa huu umeme wa *REA* ni bure. Sasa kama ndiyo hivyo, kuna pesa ambazo zinatakiwa zitolewe, basi Serikali itoe bei elekezi ili wananchi wawe wanaelewa kwamba ni bei ya kiasi kadhaa ili mtu awe anatoa kwa kujua kwamba ni hela ambayo inatakiwa itolewe kiuhalali, kwa sababu wananchi wengi wanashangaa mtu anapokwenda anaambiwa angalau atoe hela kidogo, wanabaki kushangaa, kwa sababu wanasielia kwamba ni umeme wa kuwekewa bure, inawatatiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia sasa hivi ni kipindi cha mvua na nguzo nyingi ziko chini. Sasa...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. JOYCE B. SOKOMBI: Uuh!

Mheshimiwa Naibu Spika, niongezee dakika moja. (*Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Haiwezekani Mheshimiwa, muda umekwisha. (*Kicheko*)

MHE. JOYCE B. SOKOMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, atafuatiwa na Mheshimiwa Justin Joseph Monko na Mheshimiwa Omari Kigua, ajiandae.

MHE. USSI SALUM PONDEZA AMJADI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema kuweza kusimama nami kuwa mionganoni mwa wale ambao wanaochangia katika Wizara hii ya Nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, vile vile napenda kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii. Kwanza, naomba nitoe pole kwetu sote Wabunge kwa kuondokewa na Wabunge wenzetu watatu amba Mwenyezi Mungu amewachukua, amewapenda zaidi ya sisi na niseme, Mwenyezi Mungu *inshaallah* awaweke mahali ambapo wanastahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi ya pili napenda niitoe kwa Mheshimiwa Waziri wa Nishati - Mheshimiwa Kalemani na Naibu Waziri wake - Mheshimiwa Subira Mgallu na Katibu wake *Eng. Zena*. Vile vile kama haitoshi na kwa umuhimu zaidi, napenda kumpongeza Mwenyekiti wetu wa Kamati kwa jinsi ambavyo tunashirikiana naye katika kuiendeleza na kuisimamia hii Wizara ya Nishati iweze kutekeleza majukumu yake. Kwa kiwango kikubwa kwa kweli tunasema *Alhamdulillah* na imefanya kazi kubwa sana, kila mmoja anaona na ndiyo sababu hata kila anayesimama lazima aipongeze Wizara hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda niwapongeze ni Mheshimiwa Spika, Naibu wake na Wenyeviti wote wa Bunge amba wanatuongoza vyema na wanalisimamia vyema Bunge letu hili Tukufu tangu tumeingia mpaka sasa hivi kuweza kutuweka katika mwongozo amba unatakiwa na kutusaidia katika kuhakikisha tunaisimamia vizuri Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze zaidi katika sehemu ya *REA I*, *REA II*, *REA III*. Utekelezaji wake umefanywa vizuri sana na Serikali ya Awamu ya Tano japokuwa upungufu haukosi katika utekelezaji wake na upatikanaji wa vifaa kama wengine walivyoendelea kusema, lakini umekuwa imara zaidi baada ya kuwa na mkakati wa Serikali hii kuweza kuhakikisha vifaa vyote vinapatikana ndani ya nchi yetu hii ya Tanzania. Ubora wa viwanda vyetu ambavyo vinazalisha, kwa hiyo, vyote vimeweza kuleta urahisi wa *material* na upatikanaji haraka wa huduma kwenda kwa wananchi wetu kama

mipango ilivyo ya Serikali yetu hii ya Awamu ya Tano. Japokuwa...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. USSI SALUM PONDEZA AMJADI: Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa niliseme...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, Kengele imeshagonga.

MHE. USSI SALUM PONDEZA AMJADI: Mheshimiwa Naibu Spika, dakika moja tu, nina jambo mahususi. Nakuomba dakika moja.

NAIBU SPIKA: Huwezi kuanza jambo jipya kwa sababu hutamaliza. Haya sekunde 30.

MHE. USSI SALUM PONDEZA AMJADI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nakushukuru wewe kwa kunikubalia hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo moja mahususi ambalo napenda kulisema ni jambo lile ambalo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuititia Mawaziri wake na Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na Baraza lake la Mawaziri, kuweza kuridhia na kutuondolea Zanzibar katika ununuzi wa umeme wa *bulk VAT*. Hivi sasa hatuwezi kulipa lakini tumesamehewa zaidi ya shilingi bilioni 22.8. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaipongeza sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Wanzanzibari wameniambia lazima nikipata nafasi niseme. Hili limetusaidia na tunaipongeza sana na tunasema Muungano udumu na hizi ndiyo faida za Muungano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nakushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nawashauri, ni vizuri kuanza na hoja zako, umalizie na pongezi, kwa sabbau pongezi Wizara hii kila mtu anaipongeza. Hata mimi mwenyewe nampongeza Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, pongezi kila mtu anazo kwa Wizara hii kwa kweli, wamefanya kazi nzuri. Kwa hiyo, twende kwenye ile Mitaa tunayotaka kuitaja. Ukianza na pongezi dakika zinakwisha halafu unajikuta hoja zako hujasema. Pongezi Mheshimiwa Waziri ameshazipokea kwa mikono miwili kutoka kwa Wabunge wote. (*Makof*)

Mheshimiwa Justine Joseph Monko, atafuatiwa na Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua na Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali ajiandae, atachangia kwa dakika tatu.

MHE. JUSTIN J. MONKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye Wizara yetu hii ya Nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maelekezo yako, lakini naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Makamu wa Rais kwa utekelezaji makini wa llani ya Chama cha Mapinduzi katika kupeleka umeme kwenye vijiji vyetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, viongozi hawa wamejidhihirisha kwamba kweli wao ni viongozi wa wanyonge. Pia napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mheshimiwa Waziri, Medard Kalemani na Naibu wake kwa ziara walizofanya katika Jimbo la Singida Kaskazini ambazo zimetao maelekezo na kutatua changamoto nydingi katika kuwapatia wananchi huduma hii ya umeme. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka miwili na nusu iliyopita Jimbo la Singida Kaskazini lilikuwa na vijiji sita pekee ambayo ilikuwa ni sawa na asilimia 7.1 ya vijiji vyote vilivyouwa na Nishati ya Umeme. Hadi tunavyozungumza sasa, vijiji

ambavyo vimepata umeme na ambavyo vinamalizia mradi ni vijiji 53 sawa sawa na asilimia 63.1. Kazi kubwa imefanyika, tunastahili kutoa pongezi na wananchi wanawapongeza sana Mheshimiwa Rais pamoja na timu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, bado tunazo changamoto kwenye maeneo mawili makubwa. Moja, ni mradi wa umeme wa *REA* awamu ya pili ambayo tarehe 30 Januari, 2018 ndiyo nilianza nao hapa Bungeni. Mradi huo haujakamilika, kwa hiyo, Kijiji cha Mgori, Iddi Simba, Mjuhuda pamoja na Mangida, maeneo haya bado hayajaweza kupata umeme kama ilivyokuwa imepangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri alituahidi kwamba mradi huo ungeweza kukamilika mwishoni mwa mwezi huu, namwombe sana Mheshimiwa Waziri aweze kusukuma ili mradi huu uweze kutengemaa mapema na wananchi waweze kupata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tutakuwa na vijiji 31 katika Jimbo la Singida Kaskazini ambavyo havina umeme kabisa. Tuna vijiji vyote nya Kata ya Makuro, vijiji vyote nya Kata ya Muhunga, vijiji vyote nya Kata ya Ngimu, vijiji vyote nya Kata ya Mghori kwa sasa na tuna vijiji vyote nya Kata ya Ohande havijapata umeme hata kijiji kimoja. Vimepangwa katika mradi wa *KTIP*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mradi wa *REA* ///mzunguko wa pili, naomba sana Mheshimiwa Waziri afanye haraka, michakato hii ianze ili vijiji vyetu hivi viweze kupata umeme pamoja na umeme wa ujazilizi kwenye vijiji ambavyo vimepata kwa ajili ya Vitongoji ambavyo bado.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la ufuaji wa umeme hasa mradi wa umeme wa upopo ambapo Mkoa wa Singida una rasilimali kubwa sana ya upopo na mradi huu umekwama kwa muda mrefu. Mheshimiwa Waziri nimefika kwake, tumezungumza, naomba sana wakati anahitimisha...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa. Kengele imeshagonga.

MHE. JUSTIN J. MONKO: ...atueleze mradi huu umekwama wapi. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, shukrani. Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali na Mheshimiwa Allan Joseph Kiula, ajiandae.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nami nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hotuba ya Wizara ya Nishati ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, umesema tusianze kushukuru, lakini moyo wangu unasema lazima nianze kwa kushukuru. Wanasema mnyonge mnyongeni, lakini haki yake mpeni. Mheshimiwa Naibu Waziri Subira Mgusu na Mheshimiwa Naibu Waziri ni watu ambao wamefanya kazi kubwa kwenye Taifa hili. Binafsi niseme ukweli, wamefika Jimboni kwangu siyo chini ya mara tatu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Wana-Kilindi wamesema nichukue muda mchache kuweza kuwapongeza na kuwatakitia mema katika maisha yenu. Namwomba Mheshimiwa Rais, nina uhakika ninyi nyote mtarudi Bungeni hapa, Mheshimiwa Rais akurudishe kwenye nafasi yako Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pia urudi muweze kukamilisha kazi iliyobaki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme ni uchumi wa nchi na kwa mwananchi mmoja mmoja. Sisi tunaotoka kwenye majimbo ya vijiji, mahali ambapo palikuwa hamna umeme, ukiwaka unaona faraja za wananchi. Wanafarrijika na maisha yanabadilika. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa uamuzi

mgumu ambao umewaletea faraja wananchi wa Tanzania.
(Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa nizungumzie juu ya REA. Namshukuru Mheshimiwa Waziri, wakati naingia Bungeni hapa tulikuwa na vijiji 17 tu vyenye umeme, leo hii ni takriban vijiji 62 Wilaya ya Kilindi vina umeme. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, nakuomba sasa, muda huu ninaozungumza Wakandarasi wako katika maeneo mbalimbali. Wako Kikunde, naomba vijiji ambavyo viko karibu na Kikunde vipate umeme. Navyo ni Vijihi vya Ludewa na Mafulila katika Kata ya Kikunde lakini pia Kata ya Tunguli kuna vijiji vinne ambavyo vina *population* ya takribani watu 17,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, Kijiji cha Mafulila kina mradi mkubwa sana wa mambo ya madini. Nina uhakika umeme ukifika katika maeneo haya, basi utakuwa umewasaidia Wana-Kilindi. Ppia nakuomba Mheshimiwa Waziri, vijiji vingine vichache 32 au 37 ambavyo havijapata umeme, basi naomba awamu inayokuja wananchi wa Wilaya ya Kilindi wanahitaji umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kuna jambo kubwa Mheshimiwa Wziri amelifanya nalo ni suala la kutuletea mradi wa umeme kutoka Kiteto hadi Kilindi wa KV 132. Ni mradi utakaosaidia kuondoa kukatikakatika kwa umeme. Nakupongeza katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno hayo, naomba kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofii)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali, dakika tatu, atafuatiwa na Mheshimiwa Allan Joseph Kiulana Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele ajiandae.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Itoshe kusema hongera kwa watumishi wa

Wizara. Mwaka 2019 nilisimama nikashika shilingi ya Mheshimiwa Waziri kwa ajili ya mradi wa *LNG* na nafikiri Mheshimiwa Waziri anakumbuka. Nashukuru kwamba wameanza kulipa na ni jambo la heri kabisa. Nitoe tu wito kwamba sasa baada ya kulipwa, basi mradi usichelewe tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewasikia wenzangu wakisifia *REA*, nami nazungumza kwa huzuni kubwa. Katika kipindi chote cha miaka mitano sasa, Jimbo la Mchinga halijanufaika hata kijiji kimoja. Hatujapata umeme wa *REA* katika hivyo vijiji 8,000 ambavyo tayari Serikali imeshapeleka, Jimbo la Mchinga hatujapelekewa hata kijiji kimoja katika Serikali hii ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, hili *li-take note* kwa sababu ni historia kwamba kila Mbunge anayesimama hapa anasema amepata vijiji, mimi sina cha kukumbuka zaidi tu ya hii miradi ya *LNG* ya gesi na kulipa fidia pale wananchi Kilangala na kutuletea mradi wa maji. Kwenye umeme Mheshimiwa Kalemani, hebu angalia. Tunavyo vijiji ambavyo vimeingia kwenye mpango; Namkongo, Dimba, Ruvu, Mihangara na vijiji vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka yote tumekuwa tukiambiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri alikuja hivi karibuni tena alinipa matumaini makubwa nampongeza, tulifanya mkutano vizuri kabisa na wananchi, hakuleta habari ya siasa, tulifanya mkutano kwa ajili ya kuleta maendeleo, ni historia kabisa. Mheshimiwa Waziri pia amekuwa akipita na kutoa maelezo, kwa hiyo, naomba katika kipindi kilichobakia hiki, basi angalau Ruvu na Dimba ambavyo vimeingia kwenye awamu hii ya tatu, tuwapelekeeni ili nao waone matunda ya Serikali ya Awamu ya Tano kwenye Sekta ya Umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisimama kusema hayo kwamba mmeefanya vizuri kwenye Sekta ya Gesi, naunga mkono mllichokifanya *LNG*, naunga mkono pale Kilangala mmetupatia kisima cha maji chenye zaidi ya shilingi milioni 53 kama fidia kwa wananchi ambao mashamba yao yaliunguzwa moto wakati ule wa ujenzi wa Mkuza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, atuangalie sasa kwenye umeme. Ana Mtendaji mzuri wa TANESCO pale, nampongeza sana yule *Engineer* wa Mkao na ma-*Engineer* wote, wanafanya kazi vizuri, tunashirikiana nao, panapotokea *short* wanaenda kurekebisha kwa haraka lakini kwenye suala la REA Mheshimiwa Waziri tuangalie nasi tuweze kuandika historia kwenye Awamu hii ya Tano katika kipindi hiki cha miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Allan Joseph Kiula, atafuatiwa na Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele na Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay ajiandae.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nitoe shukrani kwa kunipa nafasi ya kuzungumza leo na Waziri mhusika nafikiri atashangaa kwa nini nazungumza na wakati juzi tulikuwa naye kwenye Jimbo. Nimewiwa kuzungumza kwa sababu amefanya kazi kubwa; yeye na Naibu Waziri wamefika kwa nyakati tofauti. Mkalama ya mwaka 2015 siyo Mkalama ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maagizo aliyotoa juzi yameanza kutekelezwa. Naomba tu wahimizwe Meneja wa Mkao ili ule mradi wa kupeleka umeme katika Kata ya Mwanga uweze kuendelea. Pia vijiji ambavyo vimepata umeme katika baadhi ya Kata nyingine kama Kata ya Mpambala, Kikonda na Mwongeza, tunaomba na yenyewe vijiji hivyo viweze kupata umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa kama tulivyomwambia wakati ule, kuna maeneo ambapo nguzo zinakwenda chache, kwa hiyo, zinaacha malalamiko. Kwa hiyo, tunaomba suala la nguzo liweze kuangaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kubwa zaidi ni umeme kufika katika taasisi husika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo maneno, nitumie fursa hii kuwashukuru wananchi wa Mkalama kwa kuniyamilia kwa miaka mitano na kwa kunipa ushirikiano. Pia nitoe pongezi na shukrani kwa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kusimamia vizuri Serikali na suala la umeme Mkalama sasa linaonekana. Namshukuru Makamu wa Rais, lakini namshukuru Waziri Mkuu ambaye alifika Mkalama na alizungumza na wananchi wa Mkalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Spika na wewe pia. Nilishatoa shukrani kwa Spika na sasa nikushukuru wewe kwa kazi kubwa na pia kwa kunichaguachagua niwe nasemasema. Kwa hiyo, nami nawakilisha wananchi wangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Mawaziri 15 na Manaibu ambaao wamefika Mkalama, ndiyo wameibadilisha Mkalama, pia ni kwa kupata kibali kutoka kwa *Chief Whip* wetu mama yetu Mheshimiwa Jenista Mhagama. Wamefika na wamefanya kazi kubwa na wananchi wanaona umuhimu wa kuchagua CCM kuingia madarakani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa umuhimu kabisa namshukuru tena Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu, maana yake wote wamekanyaga Mkalama na wameiona Mkalama jinsi ilivyo na tumepata mabadiliko makubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Mheshimiwa Waziri wakati tunamalizia muhula wetu aweze kuhakikisha vijiji vyote vilivyobaki vimepata umeme. Tulipoingia tulikuwa na vijiji 15 vyenye umeme, sasa tuna vijiji 55 vyenye umeme. Juzi aliwaambia wananchi wa Mkalama ndani ya miezi minne hesabu hiyo itaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Niseme Viva Dkt. John Pombe Magufuli, viva Mheshimiwa Kassim

Majaliwa Kassim, viva Makamu wa Rais na sisi Wabunge wote viva. (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa, kengele imeshagonga.

Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, atafuatiwa na Mheshimiwa Zacharia Paul Issay na Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, ajiandae.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika Wizara hii ambayo ni muhimu sana katika Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda kuishukuru Serikali ya Tanzania ikiongozwa na Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwanza kwa kuliona tatizo lilokuwepo katika Wizara hii ambayo ilikuwa ni Wizara kubwa sana, ilikuwa inaitwa Wizara ya Nishati na Madini. Wizara hii ilikuwa ikija humu Bungeni ni mshikemshike, lakini sasa hivi mambo yamenyooka, Wizara ya Madini ipo safi na Wizara ya Nishati ipo sawasawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza sana Watumishi wa Wizara hii wakiongozwa na Mheshimiwa Kalemani, Naibu wake Mheshimiwa Subira Mgalu, Katibu Mkuu, Meneja wa *TANESCO* wa kwetu Mkoa wa Geita na Meneja wangu wa Wilaya la Mbogwe kwa kazi kubwa ambayo wamekuwa wakiifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu yangu Mheshimiwa Kalemani amefika Mbogwe mara kwa mara, Wana-Mbogwe huwa wanamwita Kakalemanii kwa maana ya kamtu kazuri ambako kametusaidia. Umefanya mambo makubwa. Mbogwe sasa hivi iko vizuri, kiwanda chetu cha kuchambua pamba *TANESCO* wanapeleka umeme sasa. Kiwanda hiki

kilikuwa kimesimama muda mrefu, Tanzania ya viwanda na kwetu Mbogwe inakwenda kuonekana kuitia Wizara hii ya Nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Nishati mmepeleka umeme katika maeneo ya wachimbaji wadogo Nyakafuru. Mheshimiwa Waziri mwenyewe amefika amewasha umeme, wachimbaji wadogo wanashangilia wanasema sasa kazi imebaki ndogo tu uwaongezee tena *transformerya KV315* ambayo uliahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina imani na Mheshimiwa Waziri amefika Mbogwe na ahadi zake siku zote ni za mtu mzima. Ahadi zake ni za kiungwana, akisema amesema. Nami nakuahidi Mheshimiwa Waziri, wewe ni jirani yangu nitawaambia watu wa Chato kwa kweli wakurudishe tena hapa ndani na Mungu akubariki sana. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Zacharia Paulo Issay atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota na Mheshimiwa Willy Qambalo ajiandae, atachangia kwa dakika tatu.

MHE. ZACHARIA P. ISSAY: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa majaliwa yake kwetu sote. Nitume nafasi hii pia kuwaombea viongozi wa Taifa letu kwa jinsi walivyotuongoza kwa miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme tu kwamba nikzungumza kama mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Mbulu Mji, katika Serikali ya Awamu ya Tano, kumefanyika kazi kubwa sana. Hongera sana Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Mawaziri na Waandamizi wote Serikalini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, langu ni shukrani. Mheshimiwa Kalemani amekuja Jimbo la Mbulu Mji mara tatu kwa nyakati tofauti. Naingia kwenye Bunge hili, nilikuwa nina Kata saba au nane nadhani katika Kata 17 za Jimbo la Mbulu

Mji. Hadi leo zimebaki Kata nne na maeneo ya kujaziliza kwenye vijiji. Hatua hii ni kubwa sana kwa sababu kazi kubwa imefanyika na Jimbo la Mbulu Mji, Kata saba ndiyo zipo mjini, kumi ziko vijijini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa namna ya pekee sana, kazi hii iliyofanyika ni kubwa, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wa kujenga Bwawa la Rufiji (*Hydro Power*), Bwawa la Mwalimu Nyerere. Bwawa hili lisingekuwepo ndoto ya Watanzania kupata umeme kila nyumba isingekuwa rahisi. Kwa hiyo, tumpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa maamuzi haya makubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, kuna maagizo aliyatoa katika ziara zake; yapo maeneo yameteklezwa na maeneo mengine hayajatekelezwa. Kwa hiyo, kwa namna ya pekee sana niseme yale maagizo yatekelezwe. Mheshimiwa Kalemani na Naibu wako mmekuja mara nyingi, mmeefanya kazi kubwa katika Jimbo la Mbulu Mji na Jimbo hilo lilikuwa na eneo kubwa la vijijini halikuwa na umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani nyingi hizi ziwafikie, tunawaombea mpate kurudi tena kwenye Bunge hili, nami naamini nitakuja. Kwa hiyo, tutakutana humu, tutamalizia kiporo kilicho mbele yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba katika mazingira yetu ya kijijini kuna maeneo ya makazi, umeme wa *line* au nguzo hautafika haraka. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri awaagize watu wake; Mameneja wa Wilaya na Mikoa waweze kufanya tathmini ya maeneo ambayo umeme wa nguzo au umeme wa *line* kubwa hautafika ili tutafute tathmini kamili ya chombo cha *UMETA* tuweze kuwapelekea wale wananchi amba moja kwa moja hawataweza kupata umeme katika maeneo haya.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. ZACHARIA P. ISSAY: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nayasema haya...

NAIBU SPIKA: Kengele imeshagonga Mheshimiwa.

MHE. ZACHARIA P. ISSAY: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Ni kwamba kuna makazi katika vijiji viro juu ya mlima, nguzo zinazotakiwa kwenda huko ni 20 na kwa hivyo *UMETA* tukipeleka ni kama yale makampuni yanayopeleka kwa namna ya pekee *solar* za kukodisha ili walipe kwa njia ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, atafuatiwa na Mheshimiwa Willy Qambalo, atakayechangia kwa dakika tatu na Mheshimiwa Joram Ismail Hongoli ajiandae.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii ambayo ipo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuwapongeza viongozi wa Wizara hii hata kama mmesema kwamba tusipongze, lakini ni vigumu kwa viongozi wa Wizara hii kutowapongeza. Nampongeza Mheshimiwa Dkt. Kalemani lakini vilevile Naibu wake Mheshimiwa Subira Mgusu. Viongozi hawa walikuwa watu wa kwenda *filed* muda wote na Mkoa wa Mtwara tulikuwa na changamoto kubwa ya umeme, kwa uongozi na uchapakazi wao wametatua changamoto kubwa ambazo ziliikuwa zinakabili Mkoa wetu wa Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza *Eng. Fadhili*, Meneja wa *TANESCO* Mkoa wa Mtwara. Kuna Mjumbe amesema huyu Mtumishi ahamishwe, lakini huyu ni mchapakazi, mvumilivu na kijana mpenda maendeleo. Amesimamia vijiji 181 vya Mkoa wa Mtwara kupata umeme chini ya uongozi wake. Mheshimiwa Dkt. Kalemani anamfahamu, amekuja mara nyingi, zaidi ya mara

tano na amekuwa akimpa maagizo na amekuwa akiyafanya kazi... (*Makofi*)

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya umeme Mkoa wa Mtwara...

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: ...imechangiwa na matatizo mbalimbali ambapo Wizara yake imechukua hatua, ikiwemo kununua mitambo mipyä miwili ya gesi ambayo imeshafungwa Mtwara na mitambo miwili ambayo ina uwezo wa kufua megawati 4.3 kila moja, ipo katika hatua ya manunuzi na tumearifiwa katika vikao mbalimbali vya kimkoa kwamba ikiingia, basi itafua megawati 8.6 na kuboresha upatikanaji wa umeme Mkoani Mtwara. Kwa hiyo, tatizo la umeme Mtwara siyo la *Engineer*, ni la miundombinu ambayo Wizara yako nakushukuru kwamba inalifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie kuhusu usambazaji wa gesi majumbani. Naipongeza Wizara na *TPDC* kwa kazi kubwa ambayo anaifanya lakini nashauri kwamba kasi ya kusambaza umeme majumbani bado ni ya kulegalega kwa sababu mpaka sasa hivi wamesambaza kwenye kaya 425. Kaya hizi zipo Shangani na eneo la Chuo cha Ufundı na Chuo cha Ualimu kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri sasa mradi huu sasa uhamie Mitaa ya kawaida, Mangowela, Chuno na Magomeni kule ambako kuna wananchi wa kawaida ili wanufaike na mradi huu wa gesi ya majumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, nachukua nafasi hii kuipongeza Wizara na *TPDC* kwa tendo la kuanza kutoa fidia kwa mradi wa *LNG* Lindi. Wenzetu wa upande mwiningine walishaanza kutoa maneno kwamba Serikali ya Awamu ya

Tano imetelekeza miradi ya gesi. Hili suala la kulipa fidia shilingi bilioni 5.2 kwa wananchi wa Lindi inadhihirisha wazi kwamba Serikali ya Awamu ya Tano vilevile inathamini miradi ya gesi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa *LND* unahitaji fedha nyingi. Kwa hiyo, Serikali imekuwa ikienda hatua kwa hatua. Kwa hiyo, naipongeza Serikali yangu kwa kuanza kulipa fidia na wananchi wa Mtwara na Lindi tunawapongeza kwa hatua hii. Kinachotakiwa niishauri Serikali yangu, ni kutoa taarifa juu ya utekelezaji wa mradi huu ili Wana-Mtwara na Lindi wanufaika na *LNG*.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Willy Qambalo, dakika tatu atafuatiwa na Mheshimiwa Joram Ismail Hongoli na Mheshimiwa Anna Richard Lupembe ajiandae.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii ndogo nami niweze kuchangia kwenye Wizara hii ambayo ni muhimu sana kwa ajili ya maendeleo ya watu wetu na nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza shukrani. Mheshimiwa Waziri wengine wamekushukuru nami naomba niungane nao kwa kazi kubwa ambayo umefanya, wewe ni msikivu lakini wewe unatenda. Umekuja Karatu mara moja lakini matunda ya ziara yako yanaonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri; alifika Kijiji cha Kusmai tulimwombwa pampu ya maji iunganishwe na Kijiji cha Endala pampu ya

maji iunganishwe na umeme. Pampu ya Endala imeshasimama kwa sababu wameshindwa kulipia għarama za mashine za Dizeli. Alitoa maelekezo karibu miezi minne imepita lakini hakuna kilchhofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili nashukuru pia kwa kuunganisha vile visima vingine ambavyo sasa wananchi wanavitumia kwa ajili ya huduma yao ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, nimeona kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri kwamba baada ya 2021 Tanzania nzima vijiji na vitongoji vyote vitakuwa vimewaka umeme. Ushauri wangu, wale ma-*surveyor* wanapokwenda kwenye ile kazi ya awali ya kutambua maeneo ya kupeleka umeme, naomba waripoti kwenye ofisi za vijiji waungane na Watendaji na Viongozi ili waongozwe na viongozi kwenye maeneo hayo kuliko wao wenyewe kwenda wanafanya kazi nusu nusu. Upungufu uliotokea kwenye awamu zilizopita ni kwa sababu wale walipofika walikwenda kufanya kazi peke yao bila kuongozwa na wale ambao wamewafikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahi sana kuona vijiji ambavyo vimepata umeme maeneo machache, sasa vinakwenda kupata umeme katika ule mradi wa ujazilishaji. Ni jambo jema, vipo Vijiji vya Endabash, Kurus, Endamarariek, Basodiwish, Rhotia na Rhotia Kainam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alitoa maelekezo Rhotia Kainam, nguzo zimewekwa miaka miwilji iliyopita lakini mpaka sasa umeme ule haujawaka. Naomba tena afanye mawasiliano na wanaohusika ili wananchi wale ambao wameshalipa waunganishwe na umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona pia kuna mradi kwa ajili ya vijiji vyote ambavyo vimebak. Tuna vijiji 12 kati ja 58 ambavyo naamini vipo kwenye orodha ya vijiji hivyo ambavyo vitapelekewa umeme. Kijiji cha Mikocheni, Endamakar, Mataha, Enbeshi, Dumbechan, Endagemu, Chemichemi, Mahoromba, Kinyehe, Korong'aida, Masabeda

na Marera. Vijiji hivyo vikipata umeme tutakuwa tumepeata umeme katika maeneo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kazi ambayo imefanyika na naamini katika kazi hii ambayo itaendewa basi itasimamiwa vizuri na maeneo yote ambayo yanastahili yatapata umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Joram Ismail Hongoli, atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Richard Lupembe na Mheshimiwa Phillip Augustino Mulugo, ajiandae.

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi. Kwanza nianze kuipongeza Serikali kwa ujumla wake kwa miradi mingi ambayo imeendela kutekeleza katika maeneo yetu.

Nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Kalemani - Waziri wa Nishati na Naibu Waziri wake kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya usiku na mchana. Kwa kweli wanahitaji pongezi kubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, kwenye Jimbo langu la Lupembe tumepeata miradi miwili ya umeme; mmoja ni mradi ule wa Makambako – Songea kuna baadhi ya vijiji vimenufaika na mradi huo; pili, tumepeata huu mradi wa REA na umeme unaoendelea kusambazwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana, kuna vijiji ambavyo ni muhimu kupata umeme; Kijiji cha Madeke. Kijiji hiki ni maarufu kwa uzalishaji wa nanasi na kuna kiwanda kilishanunuliwa muda mrefu kwa ajili ya kuchakata nanasi na kilizinduliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Pinda, lakini sasa hakifanyi kazi kwa sababu hakuna umeme. Wakati ule waliweka *solar*, sasa *solar* haina nguvu. Kwa hiyo haifanyi kazi tena. Kwa hiyo, naomba kiweze kupata umeme. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na vijiji hivyo, pia kuna Vijiji vingine kama vya Mfiriga, Ikang'asi, Itambo, Lwafi, Idamba, Dyalalo na Kitole navyo tunaomba sana viweze kupata umeme ili wananchi waweze kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa kuja na uamuvi huu wa kuja na kuanzisha mradi wa umeme wa Ruhuji ambao utazalisha megawati 358, kwa kweli naipongeza sana Serikali. Mradi huu utatusaidia sana hasa wananchi wa Njombe na maeneo mengine kwa maana ya Tanzania nzima kwa sababu utaunganishwa kwenye gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Njombe ni eneo ambalo ni la baridi lakini pia *evaporation* haipo kubwa sana, kwa hiyo, mradi huu utafanya tuwe na umeme wa kutosha sana. Kwa hiyo, naomba basi uweze kuanza haraka ili wananchi wa Njombe na Watanzania wote waweze kupata umeme kuitia mradi huu wa Mto Ruhuji ambao utaanzishwa pale Njombe na utazalisha Megawati hizi 358. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kwamba tuna kampuni ambayo pia ni *NGO* inasambaza umeme katika Jimbo langu la Lupembe imesambaza vijiji saba, Kampuni ya Sefa.

Naomba sana Serikali m jitahidi kuisaidia hii kampuni kwa sababu imeweza kusambaza kwenye vijiji hivi lakini haina uwezo wa kuweza kusambaza kwenye Vijiji au Mitaa yote kwa sababu hawana fedha za kutosha. Kwa hiyo, mkiwawezesha watafanya kazi za kusambaza eneo kubwa sana. Sasa hivi umeme unaotumika ni asilimia 30 tu, asilimia 70 hautumiki. Basi naomba Serikali isaidie kwa hilo.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele imeshagonga Mheshimiwa.

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Anna Richard Lupembe atafuatiwa na Mheshimiwa Phillip Augustino Mulugo na Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba, ajiandae.

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia. Naomba nimshukuru Mungu kwa siku hii ya leo. Naomba nimpongeze sana Waziri Mheshimiwa Kalemani kwa kazi kubwa anayoifanya. Kwetu sisi Mkoa wa Katavi ameshakuja mara nyingi, tunaomba tumshukuru sana pamoja na Nailbu Waziri kwa kazi kubwa wanayoifanya kwa ajili ya Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wana-Katavi wanashukuru sana kwa ujenzi wa gridi ya Taifa. Wanasema ahsante sana kwa sababu ujenzi huu utaleta maendeleo makubwa sana ndani ya Mkoa wetu wa Katavi, tutapata viwanda na vijana wetu wa Mkoa wa Katavi watapata ajira. Naomba niwashukuru sana Wizara kwa kazi hii ambayo wanaifanya kwa ajili ya Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna miradi ambayo inaendelea ndani ya Mkoa wetu wa Katavi lakin Wakandarasi kama vile Wabunge wenzangu walivyosema, wanacheleweshewa sana kulipwa pesa zao. Miradi hii inaenda pole pole na Wakandarasi wanalalamika sana kutokana na pesa zao kucheleweshwa. Pia wanalalamikia sana *TANESCO* ambaye anaenda kukagua kwamba hafiki katika maeneo ya site kuwakagua haraka ili aweze kuwaandikia malipo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona jitihada kubwa sana ya Waziri anapambana sana na wakandarasi na ni

mfuatiliaji mkubwa kuhakikisha vijiji vyote vinapata umeme wa REA. Sisi unaotuunganisha kuititia Mradi wa Gridi wa Taifa tunaona jitihada zako. Tunaomba basi Wizara kuititia Waziri endelea baba kufuatilia kwa sababu wakandarasi hawa wanapata shida, miradi inasuasua sana. Malengo yako wewe na Naibu Waziri ni mazuri lakini kuititia mdhamana yule wa TANESCO ndiyo anachelewesha kuwaandikia wakandarasi malipo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaipongeza sana Serikali kwa kazi kubwa wanayoifanya. Sasa hivi Mkoa wa Katavi vijiji vingi vimeshawaka umeme. Mheshimiwa Kalemani kaza buti baba tunashukuru, hata Rais alikuja kwetu kuzindua Mradi huu wa Gridi ya Taifa, tunaomba basi ufuatilie wakandarasi waweze kulipwa ili miradi yote iweze kuisha.

Mheshimiwa Nailbu Spika, nakushukuru sana, naomba kuunga mkono hoja 100%. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Phillipo Augustino Mulugo atafuatiwa na Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba, Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk atachangia kwa dakika tatu ajiandae.

MHE. PHILLIPO A. MULUGO: Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwa siyo mara nyingi kuchangia na toka bajeti hii imeanza sijachangia lakini kwa kweli kwa Wizara hii nimeona sina budi nisimame kwa wembe ule ule kwanza wa kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa ujumla, chini ya jemedari wetu Mheshimiwa John Pombe Magufuli, wanafunga magoli pamoja na Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hongereni sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri na Naibu pamoja na Wizara yote kwa ujumla ya Nishati, niwashauri jambo moja katika Jimbo langu. Mheshimiwa Waziri ulikuja mwaka juzi na mwaka jana nikakupeleka sehemu moja inaitwa Maleza pale Mbangala ukajionea mradi fulani hivi umesimama pamoja na kampuni ya Heritage Tanzania

walikuwa wakifanya utafiti wa utafutaji wa mafuta. Naomba jambo hili ulifuatiilie uone limeishia wapi kwa sababu mpaka sasa kampuni ilishaondoka, walishazira sjui walikosana nini na watu wa *TPDC*, sijajua kinachoendelea. Mheshimiwa Waziri ulipokuja Jimboni kwangu ulileta ung'aavu mkubwa sana kwenye Jimbo langu. Nitoe ushuhuda kwamba inawezekana kabisa wana Songwe wakanirudisha Bungeni hapa kwa kishindo kikubwa kwa sababu ya miradi hii ya umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ulipokuja kule kwetu sasa hivi wanakuita Mheshimiwa Medard Kelemani Udinde. Wewe ni Udinde kwa sababu ulipokuja kwenye kile kijiji toka wakati wa Mheshimiwa Nyerere, Mheshimiwa Mwinyi, Mheshimiwa Mkapa na Mheshimiwa Jakaya Kikwete hakuna umeme. Wakati wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kukutumia wewe umefika kijiji cha Udinde na Navua wananchi wale wakaweza kupata umeme ambako ndiko nimezaliwa mimi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini Mheshimiwa Waziri naomba kwa bajeti hii unisaidie sana kumalizia vijiji 12 ili kuweza kutimiza vijiji 43 kupata umeme kwenye Wilaya ya Songwe. Vijiji hivyo ni Itizilo, Ngwala, Some, Itindi, Ileya, Iyovo, Mpona, Muheza, Manda, Namkukwe, Isanzu, Namambo na Namaleza. Nakuomba kwenye bajeti ya mwaka huu Mheshimiwa Waziri vijiji hivyo viweze kupata umeme. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kunifanyia kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi mchango wangu ulikuwa ni huo mfupi tu kuipongeza Serikali pamoja na Mheshimiwa Waziri kwa kazi hii nzuri. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mulugo. Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk atakayechangia kwa dakika tatu tutamalizia na Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia atakayechangia pia kwa dakika tatu.

MHE. LOLESTIA J. BUKWIMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nianze kutoa pole kwa Mkuu wa Mkoa wetu wa Geita kwa msiba wa Mkuu wa Wilaya ya Nyang'hwale. Pia nitoe pole kwa Mheshimiwa Mbunge wa Nyang'hwale pamoja na wananchi kwa msiba mkubwa huo wa Mkuu wetu wa Wilaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pole hizo, nitoe pongezi kubwa sana kwa Mheshimiwa Waziri wa Nishati pamoja na Naibu wake, kwa kweli wanafanyakazi kubwa sana katika Wizara hiyo, wameitendea haki. Mimi binafsi nina imani kwamba Wabunge wote hapa kila mmoja amesimama kwa ajili ya kuwapongeza kwa kazi kubwa wanazozifanya. Niombe tu Mwenyezi Mungu kwa kipindi kijacho basi aweze kufanya muujiza muendelee kuongoza katika Wizara hii ili wananchi waendelee kunufaika zaidi katika sekta hii ya nishati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, nianze sasa kipekee kabisa kuleta salamu za shukrani kutoka kwa wananchi wa maeneo ambapo wamepata umeme hasa katika Kata za Bujura ambako Mheshimiwa Waziri ulikuja kuzindua umeme. Wananchi wale wanashukuru sana na wanatoa pongezi nyngi kwa jinsi ambavyo Serikali imeweza kupeleka umeme katika vijiji vyote katika Kata ya Bujura. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia katika Kata ya Kamena, vilevile wanatoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Waziri pamoja na Serikali kwa ujumla kwa kuweza kupatiwa umeme. Pia Kata za Nyarwanzaja na Nyakamwaga katika maeneo ya pale Buyagu ambapo ulikuja kuzindua wiki mbili zilizopita, kwa kweli wananchi wamefurahi na wanashukuru sana kwa ajili ya umeme ambao hakika hawakutegemea lakini kwa sababu ya jitihada ya Awamu ya Tano, kwa kweli wanashukuru sana kwa umeme huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa niaba ya Mkoa wetu wa Geita, napenda kushukuru sana kwa miradi miwili; mradi wa umeme wa kutokea Bulyanhulu kwenda Geita Mpomvu na kutoka Geita kwenda Nyakanazi, kwa kweli tunashukuru sana kwa mradi huo kwani utaleta ufumbuzi mkubwa kwa changamoto mbalimbali za umeme katika mkoa wetu. Kwa niaba ya wananchi wa Geita, nitoe shukrani sana za dhati na Mwenyezi Mungu aendelee kuwabariki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maombi machache kwa Mheshimiwa Waziri. Katika Jimbo la Busanda nina kata 22 lakini katika kata hizo....

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. LOESIA J. BUKWIMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba Waziri awafikishie umeme wananchi wote, ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mheshimiwa Subira Hamis Mgusu ajiandae.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujalia afya njema tukaweza kukutana kuendelea na shughuli zetu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ulivyosema pongezi ziwe mwisho, nianze kuzungumzia suala zima la umeme kwenye Luku. Luku ni umeme ambao kwa kweli umesaidia kwamba sasa hivi hakuna ule utaratibu wa *TANESCO* kuja wakakukatia juu ya nguzo na ukapata usumbufu. Hata hivyo, kuna kero lazima tuzizungumze na Mheshimiwa Waziri na Naibu wako mpo naomba mnisikilize kwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza unapowekewa mita ya Luku, changamoto ya kwanza

unalazimishwa kukopeshwa *unit* 50 na unakopeshwa hata kama una uwezo wa kulipia lakini unaambiwa ni utaratibu lazima ukopeshwe. Kwa bahati mbaya sasa ukikopeshwa basi zitakapomalizika lazima umeme wako wa kwanza ukapitie *TANESCO*. Sasa itokee bahati mbaya umeme ukatike usiku na *TANESCO* wamefunga ofisi basi ujue utalala na giza. Naomba jambo hili lirekebishwe kama mtu ana uwezo wa kulipia aliye lakini unaambiwa hata kama una pesa mpaka umalize *unit* 50, naona huo siyo utaratibu mzuri. Kwa hiyo, naomba hilo lifanyiwe marekebishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru katika Jiji letu la Tanga maeneo ya Ngamiani ya mjini pale tumebadilishiwa tumewekewa mita za Luku, tunashukuru sana kwa hilo. Linakuja tatizo sasa tunaambiwa eti mita za zamani zilikuwa zina-charge umeme pungufu yaani zilikuwa zina-charge umeme kwa bei ndogo, sasa umewekewa mita ya Luku unazalishiwa deni; unaambiwa kuna deni linalotokana na mita za zamani nalo hilo unatakiwa ulipe. Ukinunua Luku ya Sh.10,000 unawekewa Sh.5,000 unaambiwa Sh.5,000 unalipa deni. Sasa hili deni siyo kosa langu mimi mtumiaji sitengenezi mita, mita ni ya *TANESCO* na kwa nini linapokuja suala la hasara taasisi zote za Serikali pamoja na *TANESCO* hawakubali hasara, wanasukumiza hasara ile kwa mwananchi. Kwa hiyo mimi, nitoe wito kwamba madeni yale ambayo yametokana na mita ya zamani basi *TANESCO* wayafanye ni *bad debts* kwamba ni madeni yasiyolipika wawasamehe wananchi ili waweze kutumia umeme kwa kadri wanavyonunua umeme wao, akinunua wa Sh.10,000 awekewe *unit* zake 28. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala zima la *REA*. *REA* kuna *Phase I*, *II* hizi zimefika baadhi ya maeneo kwenye Jiji letu la Tanga lakini *REA Phase III*/bado haijafika. Kwa mfano, kuna vitongoji au mitaa kwenye Kata ya Tongoni maeneo la Lumbwa, Kiwavi, Kivindani; kwenye Kata ya Mzizima kuna maeneo ya Kihongwe, Pangarawe, Mleni Kaskazini, Rubawa; kwenye kwenye Kata ya Mabokweni kuna maeneo ya Kiruku, Mchanga Mweupe na Mchanga Mwekundu, Kibafuta, Magunduro; Kata ya Pongwe kuna maeneo ya Kihongwe,

Kisimatui na Maranzara; na Tangasisi kuna maeneo ya Nema na Mbugani. Haya maeneo nashauri basi wenzetu wa *REA* wahakikishe nako umeme unapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia, kuna baadhi ya maeneo watu wamepata umeme, kama maeneo ya Machui, Mwarongo Tongoni lakini nguzo zilikuwa hazitoshi. Sasa hivi *TANESCO* wamesema kwamba hakuna tatizo la nguzo basi tunaomba wale wananchi ambao wamekosa umeme wa *REA* kwa sababu ya ukosefu wa nguzo, nguzo zimefika wapelekewe umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine la mwisho ambalo napenda kulisema ni kwenye suala zima la mafuta. Alizungumza mzungumzaji mmoja hapa kwamba katika kipindi hiki ambapo bei ya mafuta katika soko la dunia imepungua Serikali yetu nayo iruhusu mafuta yaingizwe kwa wingi ili tuwe na akiba pale bei itakapopanda angalau wananchi wetu wawe na nafuu. Tunaona nchi kubwa kama Marekani, Uingereza wana akiba ya mafuta ya miaka 20 basi sisi tukusanye au tununue mafuta hata kama ya miaka mitano ili bei itakapopanda sisi tuwe na nafuu kuwasaidia watumiaji wa mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nipongeze Wizara ya Nishati kwa kazi nzuri wanayoifanya. Mheshimiwa Dkt Kalemani salamu zako sana kwa wakazi wa Miyanjani kwa kuwapelekea umeme ambapo ilikuwa ni historia kwao, leo tatizo hilo limekwisha, nakushukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia atafuatiwa na Mheshimiwa Subira Khamis Mgatu na Mheshimiwa mtoa hoja ajiandae.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nami nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri; Mheshimiwa Naibu Waziri; Katibu Mkuu pamoja na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii inabeba kura za Chama chetu cha Mapinduzi kwa zaidi ya 80% kwenye Jimbo langu ikifuaatiwa na sekta ya afya.

Kwa hiyo, niliomba nafasi hii kwa ajili ya kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi waliyofanya katika Jimbo langu na pia kuwapa shukrani rasmi au maalum kwa ajili ya kuniongezea vijiji katika Kata ya Muungano na Kata ya Mbawala ambapo nimeambiwa wiki hii kazi itaanza. Hii itafanya Jimbo langu kati ya vijiji 110 nitakuwa nina umeme katika vijiji 89. Ndiyo maana nasema kura katika Jimbo langu kwa kiasi kikubwa zinabebwa na Wizara hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake wamekuja katika Mkoa wetu wa Mtwara zaidi ya mara tatu. Namshukuru pia Meneja wa Mkoa wa Mtwara na Mratibu wa REA Mkoa wa Mtwara kwa kweli wanafanyakazi kubwa sana. Mheshimiwa Mbunge aliyesema kwamba ahamishwe kwa kweli tunasema hapana, kazi wanayoifanya ni kubwa, yale yanayoshindikana wanatupa ufanuzi na changamoto ya umeme Mkoa wa Mtwara wametuambia tatizo ni nini na kwamba njia za utatuzi zipo na zinafanyiwa kazi.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hawa Ghasia, subiri kidogo. Ni Kanuni gani inayovunjwa?

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, mzungumzaji anayezungumza...

NAIBU SPIKA: Naomba unitajie kwanza Kanuni inayovunjwa.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Kanuni y 64.

NAIBU SPIKA: Kanuni ya 64 ngapi ili niwe nasoma hapa wakati unazungumza.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 64(1).

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Maftah, Kanuni ya 64(1) ni ndefu ni Kanuni ipi aliyovunja Mheshimiwa Hawa Ghasia?

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kwa Kanuni ya 64 kwamba mzungumzaji anayezungumza anajaribu kupotosha Bunge, anatoa taarifa za uongo.

Mimi nilipozungumza nimesema kwamba *Engineer* ambaye ndiye anasimamia kutoa taarifa kumpa Meneja wa *TANESCO* wa Mkoa ndiye ambaye nilikuwa nimemuomba Waziri nikiwa nachangia ahamishwe Mtwara kwa sababu anatoa taarifa za uongo. Mheshimiwa Hawa Ghasia anapozungumza anasema Mheshimiwa Mbunge alizungumza juu ya Meneja sijasema juu ya Meneja hapa, kwa hiyo, analipotosha Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe mzungumzaji taarifa hiyo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, ndiyo maana wakati wote nilikuwa nakuzuia kwa sababu hapa umechanganya mambo mpaka hueleweki unataka nini. Anasema uongo kwa maana ya kwamba huyo wewe uliyesema ahamishwe asihamishwe tena abaki hapo hapo.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, niliyesema ahamishwe ni *Engineer* siyo Meneja kama anavyosema Mheshimiwa Hawa Ghasia.

NAIBU SPIKA: Sasa wao wanawasifia wote, hoja yako wewe ulimaliza na wao hawakusimama kwa sababu hiyo hiyo kwa sababu kila mtu anakuwa na mtazamo juu ya mtu. Wao wamesema Meneja wa *TANESCO*, *Engineer* wa *TANESCO* wanafanya kazi vizuri, Meneja hawezi kufanya kazi peke yake bila *Engineer*. Sasa wao wanasema wote *TANESCO* Mtwara wanafanya vizuri, wewe umetaja mmojawapo aondoke....

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Naibu Spika...

NAIBU SPIKA: Ngoja sasa, Kanuni sasa iliyovunjwa kwenye hilo ni ipi?

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ni ya kusema uongo kwa sababu Mheshimiwa Hawa Ghasia anasema uongo kwamba mimi nimesema Meneja ahamishwe sikusema Meneja ahamishwe, nimesema ambaye anapaswa kuhamishwa ni Engineer wa *TANESCO*, Mkao wa Mtwara, ambaye ndiye kakaa muda mrefu Mtwara. Yeye anasema Mbunge aliyezungumza...

NAIBU SPIKA: Haya umeshasikika.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hawa Ghasia umesema *Engineer* ndiyo asihame au Meneja ndiyo asihame au wote *TANESCO* wasihame.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Naibu Spika, huyo Meneja wa *TANESCO* Mkao wa Mtwara ni *Engineer* na kuna ma-*engineer* wengi sasa bila ku-specify kwa kutaja jina, tunazungumzia maisha ya watu, unaweza ukaenda kumchukulia mtu hatua kwa sababu hakuna jina lillotajwa sasa hata huyo Mheshimiwa Kalemani atataja lipi? Mimi nachosema ni kwamba tunawapongeza. Changamoto hatukatai zipo lakini changamoto zilizopo ni nje ya uwezo wao na Serikali pia inazifanyia kazi. Kwa hiyo, huyo kutaja tu *engineer* ni yupi? Ameshindwa kumtaja ma-*engineer* pale *TANESCO* wako wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu, kwa kweli nishati hasa umeme *TANESCO*, *REA* vijijini kazi imefanyika na kura kwa zaidi ya 80% zitatoka huku. Naunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa jinsi anavyoendelea kuliangalia jimbo na wakazi wake katika sekta mbalimbali za maendeleo ya watu wa eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika utekelezaji wa ilani, mchango huu unalenga kumkumbusha Mheshimiwa Waziri juu ya ahadi ya Serikali na Mheshimiwa Rais kuwa mradi huu wa Awamu ya Tatu ya Umeme Vijijini hautaruka kijiji, kitongoji na nyumba ya Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata zote za Halmashauri ya Chalinze zimepitiwa na umeme isipokuwa vipo baadhi ya vitongoji ambavyo vimeendelea kuona umeme ukipita hewani pasi wao kutopata nishati hii. Mfano katika Kata ya Mkange, Kitongoji cha Kwamakuru na Zimbili wanaona umeme unaelekea Mkange pasi wao kuwamo katika mpango wa umeme huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia watu wa kijiji cha Matipwili, Saadan wanaendeeaa kusubiri Mheshimiwa Waziri japo natambua kuwa mvua zimekwamisha sana utekelezaji wa mradi lakini nataka kukuhakikishia Mheshimiwa Waziri wananchi wa Kata za Chalinze wanaomba kuongezewa kasi katika kipindi hiki ambacho mvua imeanza kupungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize kwa kuiomba Serikali itoe neno juu ya malipo ya fidia ya wananchi waliopisha mradi wa umeme unaotoka Kinyerezi - Chalinze. Kilio hiki ni cha muda mrefu sasa. Tunaomba kifanyiwe kazi kilio hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Waziri na viongozi wote wa Wizara ya Nishati kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge hasa katika kipindi hiki tunapopambana na janga la Covid-19.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka minne, Serikali kupitia Wizara ya Nishati, imetekeleza kwa ufanisi mkubwa miradi ya umeme ikiwemo miradi ya kusambaza umeme vijiji (REA) na ujenzi mkubwa wa Bwawa la Julius Nyerere (*JNHP*) litakalozalisha umeme wa megawati 2,115. Miradi hii ya kusambaza umeme vijiji umeiweka Tanzania katika nafasi ya juu Afrika na umeweza kuchochaea kasi ya ukuaji wa viwanda na uchumi. Katika Jimbo la Mbeya Vijiji, REA imetekeleza umeme kwa zaidi ya vijiji 120 ambayo ni 80% ya vijiji vyote na kwa kiasi kikubwa imechochea ukuaji wa viwanda hasa vya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na vyanzo vya sasa, napendekeza Serikali itekeleze miradi ya vyanzo vingine kama vile vyanzo vya Joto Ardhi, Umeme wa Jua, Upepo na Makaa ya Mawe ili nchi yetu iendane na mahitaji makubwa ya umeme kwa hapa Tanzania na hata nchi zingine za Afrika. Ni muda mrefu sasa, TANESCO kupitia kampuni tanzu ya uendelezaji wa jotoardhi nchini - TGDC inaendelea na tafiti katika maeneo mbalimbali nchini kama vile eneo la Ziwa Ngozi lililoko Mkoani Mbeya ambapo ndipo yalipo makutano ya Bonde la Ufa la upande wa Mashariki na lile la Magharibi. Napendekeza Serikali iharakishe utekelezaji wa mradi huu wa Joto Ardhi na ule wa Makaa ya Mawe wa Mchuchuma na

Kiwira ili kuweza kuzalisha umeme zaidi kwa mahitaji ya ndani na nchi za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ikamilishe vijiji viliviyobaki na kipaumbele kiwe kata ambazo vijiji vyake vyote havina umeme. Napendekeza vijiji vya Kata ya Itawa, Shizuvi na Maendeleo ikiwa ni pamoja na vijiji viliviyosalia kupata umeme vipewe kipaumbele. Kutokana na idadi kubwa ya mahitaji ya nishati, napendekeza kuongeza *speed* ya kupeleka umeme kwenye vitongoji na hii itasaidia hata kuongeza mapato kwa Shirika la *TANESCO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na vitongoji, bado kuna vituo vya afya na shule ambazo hazijaunganishwa kwenye umeme wa *REA*, napendekeza taasisi zote zikiwemo shule, zahanati vituo vya afya vipewe kipaumbele pia. Pamoja na kuwepo laini ya umeme mkubwa, Vituo vya Afya vya Ikukwa na Santilya, Shule ya Sekondari Mshewe na Shule ya Sekondari ya Ilunga, Chuo cha Biblia, katika Halmashauri ya Mbeya hakuna umeme wa *REA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba *TANESCO* iunganishe umeme kwa taasisi hizo na pia kushughulikia maombi ya wateja wengi wanaosubiria umeme na hii ni fursa pia kwa *TANESCO* kuongeza mapato ya shirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwapongeza watendaji wote wa Wizara ya Nishati , Mheshiiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote. Pia kipekee niwashukuru watendaji wote wa *REA* wakiongozwa na Mkurugenzi Mkuu wa *REA* Taifa na watendaji wake wote na watendaji wote wa *TANESCO* Mkoa na Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuharakisha kuweka umeme katika Jimbo la Bunda Vijiji kwa maeneo yafuatayo; Nyamatatu - Hunyari; Mmagunga - Hunyari; Saba - Osanza; Nyansirori; Nyamuswa A - Mekomariro; Saloka-Guta-

Mekomariro; Sanzate - Mugeta; Manyangale - Mugeta; Nyabuzume na Tiring'ati.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nimpongeze Mkandarasi wa Mradi wa REA Mkao wa Mara anafanya kazi nzuri. Waendelee kumalizia viforo vya kazi kwa maeneo haya; Mihingo, Mahanga, Manchimwero, Tingirima, Rakana, Nyangare na Masaba.

MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu, kwa utekelezaji mzuri wa llani ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mmeefanya kazi kubwa sana na hasa ya kusambaza umeme vijiji. Umeme ni maendeleo. Nawashukuru kwa uamuzi wenu kuwa wananchi wasilipishwe nguzo za umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkao wa Kagera bado kuna vijiji vingine havijapata umeme. Mradi wa REA I, REA II hazikutekeleza vizuri mkoani Kagera. Mradi wa ujazilizaji bado haujaanza Kagera. Naomba Serikali ilione hili, awamu hizo za REA zikamilishwe, watu na taasisi waweze kupatiwa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Manispaa ya Bukoba kuna vijiji na maeneo hayo huitwa *green belt*. Mara kadhaa nimekuwa nikiomba vijiji kwenye kata hizi hawajapatiwa umeme wa REA, lakini *basically* hivi ni vijiji viko mjini. Waziri ulieleza kuwa kuna mradi wa *peri-urban* utakaota umeme kwenye maeneo kama hayo. Je, mradi wa *peri-urban* utaanza lini Kagera, ili vijiji vilivyo katika Manispaa ya Bukoba, Kata za Ijuganyondo, Kibeta, Kitendaguro, Kagondo, Nyanga, Buhembe, Nshambya na Kahororo wapatiwe umeme wa REA?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru kwa uamuzi wa Serikali wa kuunganisha Mkao wa Kagera kwenye Gridi ya Taifa. Mkao una Halmashauri nane. Je, ni Halmashauri zipi au ni zote zitakazounganishwa kwenye Gridi ya Taifa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja

MHE. PROSPER J. MBENA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuliongoza Taifa letu vizuri kwa upendo na amani na kuliletea maendeleo makubwa yenye maslahi kwa wananchi wote. Nampongeza pia Waziri wa Nishati kwa hotuba yake ya bajeti aliyoiwasilisha hapa Bungeni leo tarehe 8 Mei, 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Morogoro Kusini bado tunahitaji umeme si kwa matumizi ya nyumbani tu bali kwa ajili pia ya kufungua maeneo ya viwanda hususan vile vitakavyotumia malighafi za kilimo na mifugo. Tuna vijiji zaidi ya 87 kati ya hivyo vijiji karibu 35 bado havina umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, imemuandikia Mheshimiwa Waziri na kuorodhesha vijiji na maeneo yote yasiyo na umeme katika Jimbo la Morogoro Kusini. Mara ya kwanza nilikuandikia mwezi Desemba, 2017 na kuhakikisha umeipata. Baada ya hapo nimefuatilia na wewe binafsi na Ofisi za *TANESCO* Morogoro. Nakushukuru Mheshimiwa Waziri nilipofuatilia na wewe mwezi Februari, 2020 uliahidi kufuatilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo uhusiano mkubwa kati ya kuwepo kwa barabara na upelekaji wa umeme vijiji. Jimbo la Morogoro Kusini sehemu kubwa ipo mlimali na sehemu nyingine bado hazijafunguliwa kwa kuwepo barabara. Naiomba Serikali ione umuhimu wa kufungua vijiji na maeneo hayo yenye wakazi wengi na kuwesha vifaa vya umeme kama vile nguzo za umeme na transforma ziweze kusafirishwa. Mfano, *TANESCO* wameleta nguzo kwa ajili ya Kijiji cha Konde, lakini wakaona barabara mbovu na daraja lililoharibika gari lao halikuweza kupita wakazishusha nguzo zile Kijiji jirani cha Kisera kwa zaidi ya miezi mitatu sasa. Wananchi wanalamika, *TARURA* haina msaada na *TANESCO* wapo kimya licha ya ufuatiliaji wangu binafsi ili nguzo zile zisambazwe haraka kwa kuwa daraja lilishatengenezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji vijiji vyote via Jimbo la Morogoro Kusini vipatiwe umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupongeza kazi nzuri mnayofanya, hakika bila umeme ni ndoto kufikia uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mafinga tumepata vijiji vyote 11, hata hivyo bado vitongoji vingi havijafikiwa, ninaomba Wizara itazame suala hili na hasa kwa kuwa Mafinga ni kitovu cha uzalishaji wa shughuli za mazao ya misitu, itasaidia sana kuchochea uwekezaji wa viwanda via mazao ya misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo kituo au Wilaya ya *TANESCO* ya Mafinga, sote tunafahamu Wilaya ya Mufindi ina viwanda vingi hivyo uhitaji na huduma nzima ya umeme ni kubwa, ndio maana kwa mwaka wa nne sasa ninashauri Wizara kuona umuhimu hata wa kuwa na Wilaya ndogo ya kiumeme/*TANESCO* Mafinga ili ihudumie wateja na viwanda vilivyoko Halmashauri ya Mji wa Mafinga na Wilaya ya Mufindi iwe na Wilaya yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naweza kusema mimi ni *layman* katika nyanja hii ya umeme lakini naamini hoja yangu imeeleweka na nina taarifa ambazo sio rasmi kwamba kitajengwa kituo Liganga au Kinyanambo, kwa niaba ya wananchi wa Mafinga, nitashukuru likifanikiwa kwa sababu kama nilivyodokeza litachangia sana kuchochea uwekezaji wa viwanda lakini juu ya yote itaongeza makusanyo kwa *TANESCO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI: Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi nyingi kwa Serikali Awamu ya Tano, ikiongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akisaidiwa kwa karibu

na Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu, kwa utekelezaji wa mfano wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Hongera mahsus kwa Wizara ikiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Kalemani, Waziri na Katibu Mkuu pamoja na kikosi kizima cha wataalam na watumishi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yangu, kwanza, kasi iongezwe kumalizia utekelezaji wa Ilani ya CCM na mipango ya Serikali kufikisha umeme kwa wananchi katika miezi iliyobakia mwaka 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, mpango wa ujaziliaji uende sambamba na ongezeko la vijiji na hatimaye kufikisha umeme katika vijiji vyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, shukrani kwa Serikali kutufikishia Gridi ya Taifa Tunduru na kutukwamua kutoka matumizi ya mitambo ya dizeli kwa gharama kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, shukrani kwa Serikali ya CCM kutufikishia umeme katika vijiji 61 kati ya 92 vya Jimbo la Tunduru Kaskazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, tunaomba kasi ya usambazaji umeme katika vijiji vilivyobaki 31 iongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JUMA OTHMAN HIJA: Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kukushukuru wewe kwa namna unavyoliongoza Bunge letu tukufu kwa weledi wa hali ya juu. Namuomba Mungu aendelee kukuongoza na kukupa hekima na afya uweze kutekeleza kazi zako. Aidha, nachukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia katika hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa namna walivyoitayarisha hotuba yao kwa utaalam

mkubwa na hatimaye kuiwakilisha vyema katika Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, matumizi ya nishati nchini, nchi yetu bado inakabiliwa na uharibifu mkubwa wa ukataji wa miti kwa matumizi ya mapishi na mengineyo. Hii inatokana na kwamba Watanzania wengi hasa wa vijijini hawana uwezo wa kujitafutia mbadala wake. Tanzania tunayo gesi ya kutosha katika nchi yetu, lakini bado haiajwafaidisha wananchi walio wengi katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Serikali yetu ni kuchukua juhudli za makusudi kuifanya gesi hili kuwa ni rafiki kwa matumizi ya wananchi ili kuepuka ukataji wa miti nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwani wamekuwa ni wadau namba moja kuhakikisha nchi ya Tanzania kupitia vijiji vyote zaidi 11,000 vinapata umeme na kubaki vijiji 1,800 tu ambavyo hivyo pia kwa maelezo ya Waziri vitapata umeme, sina budi niendelee kumpongeza Waziri na timu nzima ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie hali ilivyo ndani ya Jimbo langu na niishukuru Wizara na Mkurugenzi wa REA Ndugu Maganga jana wananchi wa Nguruka wameona umeme kwa mara ya kwanza, wamenitura nikushukuru sana tena sana ila bado wana ombi nguzo zilizowekwa ni chache sana hivyo wanaiomba TANESCO kupeleka nguzo kwani mitaa mingi haina nguzo hivyo kupelekea wananchi wengi kukosa umeme na kubaki kuwa

watazamaji. Kwa kuwa natambua wewe ni mtu mwema na msikivu nguzo zitapelekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la transfoma ziko chache na wakati vijiji na vitongoji ni vingi na wewe mwenyewe ulitoa hilo agizo kuwa transfoma ziongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ni kumuomba Mheshimiwa Waziri, mkandarasi aongeze *speed* upande wa vijiji vilivyopo upande wa Ziwa Tanganyika Vijiji vya Katete, Sambala, Kajeje, Karago, Mlinga, Sunuka, Kirando, Songambele, Kinywangiri, Msiezi na Lyabusende.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji viko kwenye mpango na vilitakiwa viwashiwe umeme Juni, 2020 lakini hadi leo hata nguzo hazijaenda na kuwafanya wananchi wajione wao ndio wamebekwa nyuma, nikuombe Mheshimiwa Waziri hebu mwambie mkandarasi afanye jitihada za makusudi kuharakisha kupeleka nguzo na vifaa vingine na kazi iongezeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kuna wale wadau wa *REA* umeme ambao wamekubaliana kupeleka umeme vijiji kwangu wameweza kupeleka nguzo, nyaya na *solar panels*, cha kusikitisha hadi leo kati ya vijiji 20 walivyochukua hakuna kijiji hata kimoja ambacho wamewashasha umeme wakati vifaa vyote tayari. Niombe Wizara iingilie kati suala hili ili *solar energy* uweze kuwashwa na wananchi wanufaike.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nipongeze Wizara kwa kutenga pesa kwa ajili ya mradi wa kufua umeme Mto Maragarasi kwa niaba ya wananchi wa Kigoma, tunasema ahsante sana maana mradi huu utapunguza shida ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hoja hii muhimu sana na

kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watumishi wote kwa kazi nzuri ambazo wanafanya kwa kusimamia vizuri miradi mikubwa ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, pamoja na kazi nzuri hiyo inayofanyika, lakini ningependa kutoa masikitiko yangu makubwa kwa mkandarasi huyu wa Mradi wa REA aliyepangiwa Muheza. Mkandarasi huyu wa Kampuni ya RADI uwezo wake ni mdogo sana. Vijiji 19 alivyopewa hadi wakati huu hajavimaliza na hata hivi vya *variation* 13 hajavianza pamoja na kukulalamikia. Ningekuomba sana Mheshimiwa Waziri kama kesho utakwenda Tanga basi uwaamuru TANESCO waingie kazini kuwasaidia hawa jamaa. Kuna Mkurugenzi wake mmoja anaitwa Abdallah ni jeuri na hajawahi hata kuja kukagua miradi yake inaendeleaje. Wazawa wanapewa kazi lakini ndiyo hivyo wanashindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba kutoa msukumo kwa mradi mkubwa wa bomba la mafuta kutoka Hoima, Uganda ili mradi huo kuanza maana mradi huu tunautegemea kwa kiwango kikubwa kukuza uchumi wa Tanga na nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, sasa hivi kuna tatizo kubwa sana la kukatikatika kwa umeme katika Mji wa Muheza, sijui tatizo ni nini na wananchi wanalalamika sana na wengine vyombo vyao vinaharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, napongeza kwa mradi mkubwa wa Mwalimu Nyerere ambao kumalizika utainua sana uchumi wa nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

MHE. ZAINAB M. AMIRI: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mungu kunipa afya njema ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi mbalimbali ya

maendeleo zitolewe kwa wakati ili kuweza kutekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali itumie nguzo za zege ili kupunguza ukataji hovyo wa miti kwa ajili ya nguzo za umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iwalipe fedha zao za fidia wale wananchi waliopisha uwekezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwa wakati ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima kati ya wananchi na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali isambaze gesi ya bei nafuu kwa wakazi wa Mkoa wa Dar es Salaam, kama ilivyofanya katika maeneo ya Mikocheni ili kupunguza matumizi ya mkaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ianzishe kozi za mafuta na gesi katika vyuo vyetu vikuu ili kuweza kuwadahili wanafunzi na kuweza kupata wataalamu wa kutosha katika sekta ya mafuta na gesi kuliko kutegemea wataalamu kutoka nje ya nchi.

MHE. DKT. HADJI H. MPONDA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri wa Nishati, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara na taasisi zake zikiwemo *TANESCO* kwa utekelezaji wa majukumu yao katika kuangaza Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakazi ya Wilaya ya Malinyi katika Mradi wa Umeme Vijijini Awamu ya Kwanza (*REA I*), walipisha makazi yao, waliacha mashamba yao na baadhi waliharibu mashamba na mazao yao ili kupisha ujenzi wa miundombinu ya umeme kwa mradi huo. Katika kufanya hayo ili kuruhusu mradi kutekelezeka, Serikali kuititia *TANESCO* walikubali kufidia ubomoaji wa majengo na mashamba yao. Mchakato mzima wa malipo ya fidia hiyo umeshakamilika muda mrefu na tayari tathmini ya fidia ilishafanyika na fedha

zilishatengwa ili wananchi hao waathirika wa mradi huo walipwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena nimuombe Mheshimiwa Waziri kwa heshima zote sasa umefika mahali kuwalipa fedha zao za fidia kwa waathirika wa mradi huo wa *REA* / katika Wilaya ya Malinyi. Waziri tunamwomba atekeleze ahadi yake ya kukamilisha malipo hayo ahadi ambayo aliwaeleza wawakilishi wa waathirika hao alipokuja ofisini kwake Machi mwanzoni mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja.

MHE. DKT. STEPHEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja iliyoko mezani kwa kumwomba Waziri ufanuzi au majibu kwa masuala matatu toka kwa wananchi wa Longido kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni lini wananchi wa Kata za Longido, Kimokouwa na Namanga ambao walilipia kuunganishiwa umeme tangu mwaka jana mwezi wa pili watapata umeme?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, katika Tarafa ya Enduimet (*West Kilimanjaro*) kuna wananchi wengi ambao wamerukwa na umeme uliopita toka Siha hadi Rombo bila kushushiwa umeme. Ni lini wananchi hao watapata umeme? Vijiji husika ni pamoja na Elerai, Olmolog, Lerangwa, Kitenden, Irkaswaa na Kamwanga?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kwa kuwa wakati wa survey ya njia ya kupitisha umeme wa msongo mkubwa wa KV410 toka Singida hadi Namanga Wilayani Longido; umeme huo umepita katika baadhi ya maeneo ya wazi ya malisho ya mifugo kwenye vijiji vilivyopitiwa na umeme huo; na fidia ya maeneo hayo ilipendekezwa itolewe kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya vijiji husika. Je, ni lini Serikali italipa fedha hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji husika na fidia hiyo ya maeneo ya malisho Wilayani Longido ni Engikaret, Ranchi, Orbomba, Kimokouwa na Eorendeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nitumie fursa hii kumpongeza Waziri wa Nishati na Wizara kwa ujumla kwa kazi nzuri na zaidi sana kwa mradi mkubwa unaoendelea wa kupeleka umeme katika Tarafa ya Ketumbeine ambayo ni Tarafa ya pekee Wilayani Longido ambayo hadi sasa umeme haujafikia hata kijiji kimoja kati ya vijiji vyake vyote 19.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache, nashukuru kwa kupokea mchango wangu na ninaunga mkono hoja.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na *oil* za mitambo; kodi iongezwe kwenye *oil* inayotoka nje na kuwapa unaifuu wazalishaji wa *oil* wa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na gonjwa la Corona wauzaji wa mafuta jumla kwenye *depots* wasaidiwe kuwaongezea muda zaidi wa kulipa kodi mpaka siku 45 kutokana na biashara ya nje kudorora.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida ya wauzaji mafuta iangaliwe kuwapunguzia mzigo wauzaji wa mafuta ili kulipa mishahara kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa kujenga matenki ya kupokelea na kuhifadhiya mafuta ya jumla upoje?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ipunguze tozo mbalimbali, Serikali iangalie upya uuzaaji wa mafuta kutumia magari *mobile*.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Waheshimiwa viongozi wote wa Taifa letu

kuanzia kwa Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Rais wetu mpPENDWA, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Spika wetu na Watanzania wote, kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kutujalia baraka, amani, mafanikio na ustawi wa Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuendelee kumwomba sana Mungu atuondolee janga hili la Corona katika nchi yetu na dunia nzima kwa ujumla sisi sote tunaamini kwake yeze inawezekana. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawapa pole ndugu zetu wote wa makundi mbalimbali waliofiwa na wapendwa wao toka tuenze Bunge hili, Mwenyezi Mungu awajaalie mioyo ya faraja, amani na utulivu, kwa pamoja tuwaombee ndugu zetu marehemu wote kwa Mungu wapumzike kwa amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa moyo wangu wa dhati naipongeza sana Serikali yetu ya Awamu ya Tano kwa jinsi ilivyotekeleza llani ya CCM ya 2015 -2020 kwa kweli Chama cha Mapinduzi tuko kidedea. Mojawapo ya pongezi zangu ni ujenzi wa Bwawa la *Mwalimu Nyerere Rufiji Hydropower*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nitoe mchango wangu ushauri kwa Wizara hii; kwanza, Serikali iwasimamie kikamilifu wakandarasi wababaishaji ambao wameonekana katika utekelezaji wa REA Awamu ya Tatu ambao mpaka sasa wako nyuma ya wakati hadi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa kuwa lengo la Serikali yetu tukufu ni kufanikisha umeme kila nyumba na kwa kuwa nyumba nyingi ziko mbalimbali na uwezo wa kupeleka nguzo na waya kwa kila kaya Wizara iwaagize Mameneja wa Mikoa na Wilaya wafanye ni nyumba ngapi ambazo zitapelekewa kile chombo cha Umeme Tayari (UMETA) ambayo Serikali itachukua tozo kwa gharama ndogo kila mwezi ili Serikali ijue mahitaji halisi ya chombo hiki kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kuna watumishi wa *TANESCO* ambao siyo waaminifu wanaosema kauli ya viongozi wa Wizara ni siasa hao hawajui kuwa nchi hii itaongozwa na viongozi wa kisasa nao wanashirikiana na vishoka kupokea rushwa hao wadhibitiwe kwa kuwa watachagua heshima ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, kupitia *REA Awamu* ya Tatu tuwe na mpango wa kufanikisha umeme kila makao makuu ya kata kwa kijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia moa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru Waziri Dkt. Kalemani kwa kutusaidia kufikisha umeme kwenye visima virefu vya maji tisa ambavyo vilikuwa vinatumia mashine za dizeli kikiwemo kisima cha kijiji cha Kainam. Umeme huo ulitokea Kijiji cha Rhotia umbali wa kilometra nne. *REA* /// walitoa kandarasi ya kupeleka umeme Kainam kabla ya mradi huo mdogo wa visima ambao ulikuja na fedha zake. Ina maana mkandarasi wa *REA* /// amelipwa fedha za kilometra nne ambazo hajafanya kazi. Malipo hayo yafuatiliwe ili yatumike kwenye malengo mengine ya kijiji katika Wilaya yetu ya Karatu.

MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali naomba kuchukua fursa hii kumpungeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na kwa uhodari wake wa kuchapa kazi. Nawapongeza pia Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa juhudhi zao na utekelezaji mzuri wa llani ya CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nachukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa miradi mikubwa ya umeme ikiwemo mradi wa kufua umeme wa Mwalimu Nyerere Rufiji, Miradi ya *REA*, *densification, peri-urban* na kadhalika. Mradi wa umeme wa Mwalimu Nyerere (2,115 MW) ni mradi wa

ukombozi kwa maendeleo ya nchi yetu. Uzalishaji mkubwa wa umeme kwa mradi huo utaboresha sekta nyingi pamoja na elimu, afya, maji, viwanda, kilimo, *SGR* na kadhalika. Pia fursa za ajira zitaongezeka sana. Naipongeza Wizara kwa kusimamia vizuri kazi hii nzito.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, nashauri Wizara ihakikishe kuwa wakandarasi wanatekeleza wajibu wao kwa wakati. Mkandarasi wa Mradi wa *peri-urban* Bagamoyo - *SNOTEC* amechelewa sana kuanza kutekeleza mradi ambao alipewa Agosti, 2019. Lakini pia kasi yake ya utekelezaji wa mradi ni ndogo. Wananchi wametaharuki sana na wana wasiwasi kuwa pengine hawatopata umeme. Namuomba Mheshimiwa Waziri amfatilie mkandarasi huyu ili aweze kutekeleza majukumu yake kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, namuomba Mheshimiwa Waziri ahakikishe kuwa ahadi zinatekelezwa. Kijiji cha Kondo katika Jimbo la Bagamoyo kilipangwa katika *REA* //lakini mradi haukutekelezwa. Pia hawakuwekewa umeme kwenye *REA* ///. Sasa hivi Kondo imepangwa kwenye *peri-urban*. Namuomba sana Mheshimiwa Waziri ahakikishe kuwa safari hii wananchi wa Kondo wanapata umeme kwenye mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, kwa ufanisi wa miradi ya *REA*, nashauri *REA* izingatie mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge kwa maeneo ya kupatiwa umeme kwa utaratibu uliowekwa kuititia *TANESCO* Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wanafahamu kero za wananchi wao na wanafahamu maeneo ya kero kubwa. Wakati mwингine mapendekezo ya Wabunge hayakuzingatiwa na kwa hiyo, kusababisha shida kwa wananchi. Mfano maeneo yenye umeme kupangiwa miradi ya *REA* na kuacha maeneo yasiyokuwa na umeme. Wataalam wa *REA* wazingatie mawasilisho ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa ushauri kuwa Serikali kuititia na kurekebisha baadhi ya vipengele nya Sheria za Rasilimali vinavyowakwamisha/vilivyowakwamisha na kusababisha watafutaji wa mafuta na gesi kushindwa/kusimamisha shughuli za utafutaji na kuondoka nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na ahsante sana.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuendeleza mchango wangu pale nilipoishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere; pongezi nyingi sana mradi huu utakapokamilika, utaweza kuzalisha megawati 2,115. Sera ya Tanzania ya viwanda itakwenda sambamba na mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiwapo na umeme wa uhakika gharama za uzalishaji viwandani zitapungua, kwa sababu karibu asilimia 35 - 40 ya gharama katika viwanda ni umeme. Kama gharama za uzalishaji zitapungua viwanda vyetu vitajidesha kwa faida na bidhaa zetu zimekuwa na ubora na zinaweza kuwa na ushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo Serikali italeta kodi ya uhakika, ajira zitaongezeka, tutapata wawekezaji wa uhakika. Sasa hivi tuna mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa ya mwendo kasi kuwa wa uhakika. Wananchi wetu watanunua umeme kwa bei ya chini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa kubadilisha mfumo wa magari yanayotumia nishati ya mafuta kwenda gesi. Huu ni mradi ambaa umeanza muda mrefu sana toka mwaka 2008 ni mradi unaofanywa katika ya *TPDC* na Chuo cha *D/T* kwa ajili ya kubadilisha mfumo wa magari toka kutumia petroli na dizeli kwenda mfumo wa gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi hili limeanza na ni magari kati ya 300 na 400 tu yameweza kubadilishwa kuitia mfumo huu. Lakini mradi huu kama ungekamilika tungeweza kuokoa asilimia 60 - 70 ya gharama za mafuta. Mradi huu ni mzuri utasadia pia katika utunzaji wa mazingira kwa kupunguza hewa chafu na magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia nchi nyininge kama India na Bangladesh waliweza kufanikisha sababu wamepeleka teknolojia kufundisha katika nchi zao na sisi hapa Tanzania tunaweza kupeleka teknolojia hii katika vyuo vya VETA, TEMESA, Magereza na SUMA JKT, tungeweza kutekeleza mradi huu kwa haraka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujua kama kuna tatizo lilitosababisha ucheleweshaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. VICKY P. KAMATA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi. Ninayo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niipongeze sana Serikali kwa kutekeleza mradi mkubwa wa kielelezo wa Julius Nyerere wa MW 2115; mradi wa kwanza kwa kuwa na bwawa kubwa Afrika Mashariki. Mradi wa kwanza wa umeme kuendesha treni ya kisasa ya mwendo kasi hadi Morogoro katika Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niipongeze Serikali kwa kuwa ya kwanza kusambaza umeme vijiji kwa 75% kwa Afrika Mashariki na Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupunguza gharama ya kuunganisha umeme vijiji kutoka 177,000 hadi 27,000. Ni mengi ya kupongeza hivyo naomba kuunga hoja mkono ili fedha zitoke zikasaidie miradi zaidi kwa maendeleo ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono.

NAIBU SPIKA: Sasa nadhani Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri kwa sababu ndiyo zamu yenu inakuja, Mheshimiwa Maftaha nadhani anazungumzia *Engineer* wa Mkoa, mimi sijui kama huwa kuna cheo cha *Engineer* wa Mkoa lakini ndiyo maelezo yake hapa, anataka *Engineer* wa Mkoa ndiyo aondoke. Sasa sijui kama hizi sifa anapewa mtu ambaye ni tofauti na huyo *Engineer* wa Mkoa kwamba ndiye anayesimamia sifahamu lakini nadhani hoja yake iko hapo.

Mheshimiwa Subira Khamis Mgusu na Mheshimiwa mtoa hoja ajiandae. Mheshimiwa Subira una dakika saba.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu kuchangia hoja yetu ya Wizara ya Nishati na nianze kusema kwamba naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama kwa heshima na taadhima kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama ndani ya Bunge hili kwa mara ya tatu katika bajeti yetu ya Wizara ya Nishati. Napenda sana nimshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt John Pombe Magufuli kwa imani yake alivyoniteua kuwa Naibu Waziri na kuhudumu katika sekta hii ya Nishati kwa miaka mitatu. Namshukuru sana namtakia kila la kheri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini pia namshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais Mama Samia, Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Chief Whip wetu Mama Jenista Mhagama na Mawaziri wote na Manaibu.

Kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wangu, Dkt Medard Kalemani kwa kuniongoza vizuri, kwa kunipangia majukumu mbalimbali ambayo Waheshimiwa Wabunge leo mmeona kwamba na mimi nilivyotoa mchango. Pia nawashukuru sana watendaji wa Wizara yetu ya Nishati wakiongozwa na Injinia Zena Saidi pamoja na Naibu Katibu

Mkuu, Wakuu wote wa taasisi, Wenyeviti wa Bodii, watumishi wote, madereva wetu, masekretari na makatibu kwa kutusaidia kutekeleza majukumu yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kipekee pia niwashukuru wazazi wangu, mume wangu na watoto kwa kunivumilia wakati natekeleza majukumu yangu. Mwisho si kwa umuhimu niwashukuru sana wana UWT wa Mkoo wa Pwani pamoja na Chama cha Mapinduzi kwa kuniwezesha kuwa Mbunge kupitia Chama cha Mapinduzi kwa mwaka 2015-2020 ambayo imepelekea Mheshimiwa Rais kuona Mkoo wetu wa Pwani na kunteua na imepelekea kupata fursa hii ambayo mara ya mwisho alikuwa nayo marehemu Bibi Titi Mohamed mwaka 1965. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikupongeze wewe pamoja na Spika na Wenyeviti wote kwa kutuongoza vizuri kwenye Bunge letu hili la kisasa kabisa la Kumi la Kumi na Moja ambalo limetekeleza wajibu wake vema kabisa. Niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja yetu kwa yote waliyozungumza, kwa pongezi zao, ni wazi wametoa pongezi wakihitaji zaidi na ndiyo maana kila walipozungumza walielezea pia mapungufu yako wapi ili tuweze kuyafanya kazi zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mjadala wote nilipokuwa naufuatilia asilimia kubwa ya mjadala ni umeme vijijiini, na jambo ambalo Waheshimiwa Wabunge wengi wamepongeza, na niunge mkono kwamba kwa kweli Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli na Serikali yake ya Awamu ya Tano itakumbukwa, kwa kuifanya Tanzania kuwa ya kwanza. Kusambaza umeme vijijiini ukanda wa Afrika Mashariki na nchi za Kusini mwa Afrika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, inaonyesha pia kabisa dhamira ya kujenga uchumi wa viwanda ambayo injini kubwa, ni umeme na kuelekea uchumi wa katii mwaka, 2025 kwamba itatimia. Nalisema hivyo kwa sababu kwa kazi iliyofanyika hapa ambayo Waheshimiwa Wabunge

mmesema, kwa vijiji tulivyovikia 9,112 na tunaanza safari Julai, 2020 ya vijiji 1,822 vilivyosalia. lakini safari hiyo itaenda sambamba na kusambaza umeme kwenye ngazi ya vitongoji ambapo kwa kipindi cha Awamu ya Tano pia, pamoja kwamba ilani ilisema tupeleke umeme vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini iliona kuna haja kwa maeneo ambayo yamefikiwa na umeme kuendelea kusambaziwa kwenye ngazi ya vitongoji, na ndio maana tulianza ujazilizi awamu ya kwanza, ujazilizi awamu ya pili *two A na B Peri-urban* na miradi mbalimbali ambayo inamaanisha matumaini ya Wabunge ya maeneo ambayo mmeyataja wote Wabunge 26 mliochangia. Kwamba yapo maeneo yaliyosalia vipo vijiji vilivyorukwa, yapo maeneo ambayo pengine kwa namna moja au nyngine yana watu wengi, napenda kuwaahidi kwa kipindi kilichosalia hiki cha utekelezaji wa hizi kazi, tutaendelea kuyafanyia kazi maeneo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Waheshimiwa Wabunge mmeleza pia baadhi ya Taasisi za Umma ambazo hazijaunganishiwa umeme. Ni kweli zipo lakini nataka kama ambavyo bajeti yetu imesema Mapinduzi makubwa yaliyofanya kupitia Taasisi za Umma elfu kumi na tano kutoka elfu nne. Zaidi ya Taasisi za Umma mpya kumi na moja elfu, Zahanati, Miradi ya Maji, Vituo vya Afya vyote hivyo vimeunganishiwa umeme. Na kwa kuwa tunatambua katika wakati huu ambapo Mheshimiwa Rais wetu anaongoza vita ya kupambana na janga hili, sisi sekta ya nishati tunayo nafasi kubwa ya kuhakikisha umeme unapatikana kwenye shule zote na maeneo mbalimbali vijijini ili ile elimu inayotolewa kwa njia ya masafa ipatikane. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya wagonjwa wa ugonjwa huu, lakini katika mazingira mbalimbali. Kwa hiyo, niseme itoshe tu kusema yote yaliyozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge nimeyapokea, tutaendelea kuyafanyia kazi kwenye mapungufu kutatua, kwenye maeneo ya masuala ya miradi ya usambazaji gesi, na maeneo maalum ya Mkoa

wa Mtwara. Napenda kusema ni kweli Serikali imefanya kazi kubwa ya kuhakikisha umeme unatulia kwenye maeneo ambapo umepelekwa *grid* ya Taifa na kila jambo lazima litakuwa na changamoto kwenye hatua za awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nipende kuwaahidi Watanzania wa maeneo hayo, hatua tu ya kufikisha *grid* ya Taifa ilikuwa na lengo la kuiwezesha kwanza *TANESCO* kupunguza gharama za uendeshaji na hiyo tumefanikiwa. Lakini hatua ya pili ni lazima tuhakikishe umeme wa uhakika unapatikana katika maeneo hayo.

Kwa hiyo, ndio maana kuna hatua mbalimbali za ununuzi wa vifaa ambavyo vitawezesha umeme kutulia katika maeneo hayo ya Mkoa wa Ruvuma, ya Mkoa wa Mtwara, ya Mkoa wa Lindi, ya maeneo ya Biharamulo na maeneo mbalimbali ambapo tumepeleka gridi ya Taifa. Kwa hiyo, naomba waone kama hiyo ni fursa na kwamba sasa katika maeneo hayo ni wazi kwamba uchumi wa viwanda utapatikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia limezungumzwa hapa suala zima la kuhakikisha kuna maeneo yamejitokeza kukatikakatika kwa umeme. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Wazir, alishalitolea maelekezo kwamba ni marufuku kwa *TANESCO* kukata umeme kwa makusudi na haijawahi kutokea. Lakini wazi kwa nchi ambayo kwa sasa tuliyokuwa na nguzo 1,700,000 mpaka mwaka 2015 lakini sasa hivi tumeweza kujenga nguzo mpya zaidi ya takribani 3,700,000 na umeme umefika katika maeneo mbalimbali. Ni wazi sasa kazi inayofuatia ni kuimarisha miundombinu ya vituo vya kuzalishia umeme, vituo vya kupooza umeme lakini na njia za kusafirishia umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba naunga mkono hoja. Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana Watanzania, ahsante Mheshimiwa Rais kwa muongozo wako, Sekta ya Nishati itaendelea kuchangia uchumi, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, nimuite sasa Mheshimiwa Dkt. Medard Matogolo Kalemani, Waziri wa Nishati ahitimishe hoja yake.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru tena kwa mara ya pili kunipa nafasi ili niweze kuhitimisha hoja yangu kwa mwaka 2020/2021. Yamesemwa mengi na niwashukuru Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi wamefika takribani 24 na wengine wamechangia kwa maneno na wengine kwa kutumia mtandao wa kisasa. Kwa hiyo nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote mliochangia kwenye maada hii kwa sababu mmelenga kufanikisha. Niwaahidi Waheshimiwa Wabunge michango yenu na ushauri wenu mlioutoa kwetu ni maelekezo, tunakwenda kuufanya kazi kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuendelea kujibu hoja chache naomba nitoe shukrani kwako kwa kuendesha mjadala wa leo. Lakini pia mfikishie pongezi Mheshimiwa Spika na timu nzima ya Sekretarieti ya Bunge lako.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba niseme mambo matatu ya msingi, katika Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Magufuli yako mambo makubwa matatu ambayo kidunia Tanzania imepaa kwa daraja la kwanza, na ningependa niyaeleze Watanzania waweze kuyafahamu. Kabla sijampongeza Mheshimiwa Rais Magufuli na viongozi wetu waandamizi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Julius Nyerere kama ambavyo nimeutaja ni mradi ambao tutakumbukwa daima kwa Afrika na si kwa Afrika na dunia nzima. Nimeeleza kwenye hotuba yangu kwamba mradi huu unakwenda kututoa kwenye changamoto zote za kiumeme, na naishukuru Serikali na Waheshimiwa Wabunge mnavyopitisha bajeti kutekeleza mradi huu. Nasema kama msimamizi wa mradi huu hautacheleweshwa na wala hautakwamishwa utakamilika ndani ya muda ili Watanzania wapate umeme wa uhakika. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, umeme wa kuendesha treni; naomba niwaambie Watanzania kwa nchi za Afrika Mashariki nenda Uganda, nenda Kenya, nenda Rwanda hawajaanza kufikiri kuendesha treni kwa umeme sisi tumeanza. Na tumekuwa watu wa kwanza kwa Afrika Mashariki kutekeleza mradi huu na kwa sasa uko asilimia 89.2, mwezi Juni unakamilika. Kwa hiyo, si muda mrefu treni ya umeme itaanza kutembea tena kwa *speed* kali ya kisasa kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro kwa hatua ya kwanza. Serikali kwasababu tuna ziada ya umeme tumetenga *Mega Watts* 70 kwa ajili ya kuendesha treni ya mwendokasi kwa umeme. Hayo ni mafanikio makubwa sana ya pili. Kwa hiyo, Tanzania tunaingia kwenye ulingo wa Kiafrika kutembeza treni kwa mwendakasi kwa kutumia umeme, hilo la pili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu umeme vijijini, nilitoa takwimu hapa juzi. Nilisema mwaka 2007 umeme vijijini tulikuwa na asilimia 6, mwaka 2008 tukawa na asilimia 8.2, mwaka 2015 tukawa na asilimia 25, mwaka 2017 tukawa na silimia 58, mwaka jana tukawa na asilimia 80, leo tuna asilimia 85 na ndiyo tunaongoza kwa Afrika na nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe Watanzania haya mambo matatu Tanzania ilivyo sasa naomba mhesabu miaka miwili ijayo tutapaa sana kidunia. Na ndugu zangu huwezi kujenga uchumi wa aina yoyote kama huna umeme vijijini. Viwanda vyote na Watanzania wanaosikiliza vitajengwa vijijini, huwezi ukajenga kiwanda leo mjini, kwanza hakuna eneo malighafi iko kijijini. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais aliona mbali, naomba niwafundishe Watanzania tuwe na kumbukumbu za viongozi wa kimataifa na sifa zao tano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais Magufuli ana sifa tano, anazo sifa nyingi sana lakini tano ni kubwa. Sifa ya kwanza ni mjasiri wa kufanya maamuzi, bila kufanya maamuzi haya mambo matatu yasingewezekana leo. Sifa ya pili ni kuwa na maono ya kuona mbali, ni viongozi wako wengi wenye maono ni wachache. Sifa ya tatu ndugu zangu

Watanzania ni uzalendo, miradi niliyosema yote inahitaji uzalendo mkubwa na sifa ya nne ndugu zangu Watanzania nakumbusha tena nilishawahi kusema ni ubunifu. Mheshimiwa Rais ni mbunifu sana, anaweza akaanzisha jambo na usiweze kujua kama litatekelezeka kwa namna ile lakini ni mbunifu wa ajabu na jambo la tano anamtegemea na kumuweka Mungu mbele. (*Makof!*)

MBUNGE FULANI: Sawa kabisa!

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ndugu zangu Watanzania kwenye Wizara ya Nishati mambo haya yametusaidia sana ndiyo maana tumefika katika hatua ambayo tumefika hivi leo. Kwa hiyo, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli kwa uholanzi wake na maelekezo thabiti kwa kuifanya Tanzania kuelekea kweli kwenye uchumi wa viwanda tena bila kusuasua kwa sababu ya kuwa na umeme wa kutosha. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu wewe ni Mbunge, naomba niwaombe wana Ruangwa kusitokee mtu yejote kule Ruangwa wa kumpinga Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu amepeleka umeme karibu maeneo yote sijazungumza taasisi nyingine, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu tulienda pale Mchenganyumba. Mchenganyumba alikuwa hana umeme amepeleka Mheshimiwa Waziri Mkuu, Ipingo umepeleka umeme, Luchelegwa umepeleka umeme, Mng'au umepeleka umeme na maeneo mengine chungu nzima. Mtu atakayejaribu kujaza fomu Ruangwa Mheshimiwa Waziri Mkuu nitamshangaa sana, niwaombe wana Ruangwa waendelee kumpa ushirikiano. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Spika, ametusaidia sana kwenye miongozo ya majadiliano ya upelekaji umeme vijijini. Waheshimiwa wengi walikuwa wana hoja mahsus na sisi tumezizingatia sana,

mfikishie salama Mheshimiwa Spika vijiji vyake vitano vilivyokuwa vimebaki navyo vinapelekewa umeme. Mwambie kabisa kumbe kule Saigonitumeshaanza kupeleka umeme, Logiro tunapeleka umeme, Huguni tunapeleka umeme, Vurundiro tunapeleka umeme na Sirare wameshaanza na ndio vijiji vilivyobaki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwako ikikupendeza pale Mbeya, pale Nzoo tumeshaanza, pale Sagara tumeshaanza, na pale Iziwa tumeshaanza, Itiza tumeshaanza pamoja na Mwansekwa tumeanza, Msalagale Relini Nsalaga mpaka kwenye madampo tumeshapeleka, na wewe hongera sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ndugu zangu ninaweza nikasema mengi, naomba niwapongeze kila Mbunge, leo nchi yetu pembe zote nne zinang'ara umeme. Hata ukienda kule Buhigwe kabisa mpakani na Burundi, Burimanyi kuna umeme na ni mpakani kabisa mwa Burundi. Hata ukienda kule Uvinza kwa Mheshimiwa Hasna Mwilima kule Kazulamimba kuna umeme, tunakwenda Sunuka karibu na DRC kuna umeme. Hata ukienda kule Mwasi kwa Mheshimiwa Kalambo kuna umeme, nenda Masasi kule Mrunderunde nako kuna umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna mahali ambapo hatuajfika, hata kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama Rundusi tunapeleka umeme, vijiji vyako vyote tunapeleka umeme. Kwa hiyo, Watanzania naomba sana muiamini serikali maeneo yote yaliyobaki yatafikishiwa umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, imeona nitoe maelezo mengi kwenye hili, mwaka huu wa fedha umetupa fedha za kutosha, vijiji vilivyobaki kwa nchi nzima 1,822 vyote vitapelekewa umeme kufuka Juni mwakani na hatuna mashaka katika hilo niwaombe watanzani ushirikiano katika hilo ili vijiji vyote vifikiwe umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona kuna hoja vijazilizi vile vidogo vidogo maeneo ambayo yana madogo madogo

yenye maeneo yenye matatizo madogo madogo. Lakini niseme tu vitongoji na maeneo ya mitaani na maeneo ambayo hayaja fikiwa na umeme na hasa pembezoni mwa majiji kama Jiji la Mbeya, Jiji la Mwanza, Jiji la Dar es Salaam, Jiji la Tanga na maeneo mengine yote tuna mkakati na tumeshatenga fedha. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge si muda mrefu mtaidhinisha bilioni 103 zikawapelekee umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba maeneo yote ya Nyamagana. Maeneo yote ya jiji la Dar es Salaam, Chanika, Mbondole mpaka kwenda Nyeburu yanayolalamikiwa yatapata umeme.

Kwa hiyo, tumeweka mpanga mahususi wa maeneo ya mjini yenye sifa na tabia za kivijiji nayo yatapelekewa umeme kwa mtindo huo huo wa elfu ishirini na saba. Hii ni jambo kubwa sana Serikali imeenza kullifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja hapa imezungumza suala la mafuta, ni kweli ungonjwa huu wa corona umekuja na mambo mengi. Lakini sisi kama Serikali tulijipanga mapema, baada ya kuona ugonjwa huu unaweza ukaathiri upatikanaji wa mfuta na tunafahamu kuna nchi mbalimbali ambapo mafuta yatoka kama kule Qatar, Dubai, India nako wameshaaza kupata tatizo la ugoanjwa huu tulijipanga viziri. Kwa hiyo, tumeanza kugaiza mafuta yakutosha kwa miezi miwili ijayo, jambo ambayo halikkuweza kutokea namna hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunayozuada ya mafuta ya kutosha kutufikisha mpaka huko hata ikiendelea kwa namna hii. Pamoja na kuwa na ziada ya mafuta zaidi ya milioni 368 kwa miezi miwili ijayo lakini mafuta tunaendelea kupakua kila leo. Leo tumepakwa mfuta lita milioni 58 kwa Dar es Salaam na tunaendelea kupakuwa mafuta Mtwara pamoja na Tanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niwaondoe wasiwasi watanzania pamoja na uwepo wa ugonjwa huu wa corona lakini kazi inasonga mbele, na mafuta

yataendelea kapatikan bila kuwa na wasiwasi wowote.
(Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli pia bei imepungua na kutokana na punguzo la bei la soko la dunia hata mafuta hapa Dar es Salaam, Mtwara na Tanga kwa nchi nzima nayo yamepungua. Napenda niseme kwa upande wa *diesel* imepungua kwa shilingi 116, kwa upande wa *petrol* shilingi 165, mafuta ya ndege shilingi 55. Kwa hiyo, tunaendelea kuliingana na soko la dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maeneo yamezungumzwa kumatika kwa umeme labda nieleze kwa ujumla, kwanza kama nilivyosema tunayaziada yakutosha kwa leo tunaziada ya *Mega Watts* 312 kwa hiyo umeme unatosha. Na katika jiji la Dar es Salaam peke yake tuna *Mega Watts* 900 wakati matumizi ni *Mega Watts* 722.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jiji la Mwanza tuna *Mega Watts* 180 matumizi mega watts 58, katika jiji la Tanga tuna *Mega Watts* 90 matumizi ni *Mega Watts* 42 kwa hiyo hakuna sababu ya umeme kumatika popote pale. Naomba nitoe elekezo kwa mameneja wa *TANESCO* nchi nzima, kwamba kusitokee na katizo la umeme kunakotekewa na kudhaniwa kupungua kwa umeme labda iwe hitalifu na niya dharura, na ikitokea hivyo basi ukarabati ufanyike mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningezungumzia ni uingizaji wa vifaa, tunasambaza gesi pamoja na usambazaji wa umeme tumetoa maelekezo kwa watendaji wetu kwamba kuanzia tarehe 1Julai, vifaa vyta kuunganisha umeme kama nati na *bolt* nazo haziaanza kutolewa nje vitaanza kuagizwa hapa nchini ili kuharakisha utekelezaji wa kusambaza umeme na tumefanya hivyo hivyo kwenye usambazaji wa gesi majumbani na katika magari. Tulianza kutoa maelekezo kuanzia mwaka jana mabomba ya kusambaza gesi hayatoki tena nje ya nchi badala lake kuna viwanda vitatu vinatengeneza hapa nchi ambavyo vinatoa na ajira na kuharakisha mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa narudia kutoa tangazo tena kwa ajili ya mita za kusambaza gesi, nazo tutasitisha kuanzia tarehe 1, Julai, 2020 lli viwanda vyta kutengeneza gesi pamoja na kutengeneza mita gesi zianze kuzalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwasababu maelezo yapo mengi, na muda ni mdogo nitapenda nijielekeze kwa upande wa usambaji wa umeme kwa maeneo ya mjini kama Dodoma. Jiji la Dodoma tunataka kulifanyakuwa jiji la kwanza kwa Afrika Mashariki, kwa sasa Dodoma ina umeme wa *Mega Watts* 42 kama *total install capital*. Lakini tunajenga mtambo mkubwa sana pale Zuzu wa jumla ya *Mega Watts* 600 mpya. Kwa hiyo, tukiongeza na *Mega Watts* 42 kutakukwa na *Mega Watts* 642 hajjawahi kutokea kwenye Majiji ya Afrika kuwa na umeme mwingi namna hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumetenga fedha za kutosha kulifanya jiji la Dodoma kiumeme kuwa la kimatifa. Lakini mpango wa pili kwakwa Dodoma tunaweka *under ground cable* haya mawaya na mangozo nguzo mmnayoona leo hamtayaona baada ya miaka mitano ijayo. Tutakuwa na *under ground cable*, utakuwa unaona hakuna umeme hakuna mangozo na mawaya waya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona niliseme hili kama mipango mahususi ya Serikali ya Awamu ya Tano, umesema dakika kumi na tano lakini nina mambo mengi ya kusema. Labda nimalizie na jambo moja katika baadhi ya maeneo. Maeneo ya visiwa kama Ukerewe Mafia na maeneo mengine tumeenza mpango wa kupeleka *submarine cable*. Kwa hiyo, tutadumbukiza *cable* chini umeme utakwenda katika maeneo hayo ili napo kuwe na umeme wa uhakika. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge wa Ukerewe tunaomba hilo tufikishie salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kwa udogo sana, nafahamu kuna bei wasambaji wa umeme kwenye maeneo ya visiwa wanatoa tofauti na elekezo la Serikali. Naomba nitamke kutumia Bunge lako tukufu, bei kwa wateja kwa nchi

nzima lazima ziwe zinazofanana hakuna mtanzania atakayetozwa bei tofauti na mtanzania mwingine wa eneo tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba kutoa maelekezo kwa wasambaji wa umeme, hasa umeme jadilifu maeneo ya Ukerewe Mafia na maeneo mengine wanaotoza shilinigi elfu tatu kwa *unit* ikome mara moja, bei sahihi kwa *unit* moja ni shilingi mia moja kwa watumiaji wa kawaida, kwa hiyo, watanzania wote watalipa bei hiyo..

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kwa udogo ni kuhusu kulipia nguzo naomba kurudia nimeshatoa maelekezo na hapa narudia kwa niaba ya Serikali, bei ya vijiji ni 27,000 na hakuna bei nytingine ya kuunganishiwa umeme. Na hakuna mtanzania kutozwa bei ya nguzo Serikali imegharamia nguzo kwa asillimia 100. Haya maelekezo lazima Mameneja wote na wakandarasi wayazingatie kuanzia leo. Meneja yoyote atakeyesikika basi Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa na Kiongozi wa kata na Viji vachukue hatua dhidi yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *Engineerwa Mtwara* naomba niseme kidogo, ni kweli *Engineer* anaweza akawa meneja, na anaweza akawa meneja asiwe *Engineer* tu akawa na *professional* nytingine, *Engineer* wa Mtwara anayezungumzwa kwasababu ma-*engineer* ni wengi tutahitaji kukaa na Mheshimiwa Maftah kujua ni *engineer* gani. Lakini nieme ukweli ndugu zangu tuwatendee haki wafanyakazi wa *TANESCO*. Mameneja wetu kwa sasa wanafanyakazi usiku wan a mchana sana, nitakauwa mtu wa mwisho kabisa kabisa kwa kweli vijana wa *TANESCO* wanafanya kazi nzuri wapo wachache ambao tunahangaika nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini meneja wa Mtwara ambaye ni *engineer* anafanya kazi vinzuri sana. Nitakaa na Mheshimiwa Maftaha tuangalie, lakini naomba aniletee jina mahusi la huyo *engineer* anayemtaja. Kwa sababu si kweli ma-*engineer* wote ndiyo mameneja, lakini kuna meneja,

kuna *engineer*, kuna *Engineer Senior*, kuna *Engeneer Junior* kuna ma-*engineer* wengi. Naomba Mheshimiwa Maftaha basi tutakaa pamoja tuliweke sawa jambo hili, lakini nitoe rai basi kwa wakandarasi wote na mameneja mzingatie kutoa huduma kwa wateja bila kusuasua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshimiwa na busara kabisa naomba kwa hatua ya mwisho niseme neno moja. Niwaomba wananchi wangu wa Jimbo la Chato na ninafahamu wanansikiliza, na kwa heshima ya pekee niwashukuru sana wazazi wangu, wamenilea vizuri sana, wamenielekeza vizuri sana, bila wao nisengefanya kazi hizi. Ndugu zangu wazazi wangu wa Chato hongereni sana nipo pamoja na mara baada ya Bunge nitarejea huko tutaendelea kukaa pamoja kufanya utafakari wa namna yakuendeleza jimbo nzuri la Chato nawashukuru sana wazazi wangu wa Chato kwa kunilea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri wangu kwa kazi nzuri anazofanya, mnavyomuona bila yeye pengine ningekuwa nachoka choka sana. Lakini kama unavyomuona basi mambo yanakwenda vizuri, nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri unafanya kazi vizuri hongera sana. Naomba nimpongeza *Engineer Zena* anafanya kazi vizuri sana huyu ni Katibu Mkuu mpya, amefanya kazi zuri kwa ushirikiano mzuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bila kumsahau aliyekuwa Dkt. Mwinyimvua alitupa ushirikiano mzuri sana hata kabla ya kustaaifu. Nawapongeza Wenyevitii wa bodi zote Watendaji wa Mashirika yote chini ya wizara yetu kwa ushirikiano mnaotupa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho Waheshimiwa Wabunge sitawasahau Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili mmenipa ushirikiano wa kutosha kabisa kabisa nimeingia kwenye Ubunge nikiwa kijana naona kama naanza kuzeeka naomba basi mnichosechose niendelee kuwa kijana niendelee kuwahudumia. Lakini hii yote ni kwasababu ya nyie

manavyotupa ushirikiano. Mmakuwa mkinipa ushirikiano mmeleta hoja na yote mliyotupa pongezi nawaomba na ninyi yawarudie, Wabunge wote mmefanya kazi viziri hongereni sana na Mungu awabariki. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya sasa naomba kutoa hoja. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono ahsante sana nichukue fursa hii kwa niaba yenu wote nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri waliyoifanya. Kwa kweli tumewaona kila mahali na nadhini pongeze za Waheshimiwa Wabunge mmezisikia. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge baada ya kungwa mkono hoja hii kwa kawaida ilikuwa niwahoji, naangalia kura zilizopigwa hapa idadi ya wapiga kura ni kubwa na Waheshimiwa Wabunge wengi kati hao waliopiga kura wamepiga kura za ndiyo. (*Makof*)

Kwa hivyo nichukue fursa hii kutangaza kwamba Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/2021 yamepitishwa na Bunge. (*Makof*)

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 yalipitishwa na Bunge kama ifuatavyo:-

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu - 58 Wizara ya Nishati.....Sh.28,399,590,000/=

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu - 58 Wizara ya Nishati.....Sh.2,168,437,184,000/=

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Kwa hiyo, hongereni Wizara lakini watendaji wenu kwa kazi nzuri mliyoifanya lakini pia nawashukuru sana kamati ambao mmefanya kazi nzuri sana kwa niaba ya Bunge. Mmetoa mawazo yenu kwa upande wa Serikali na wameyafanya kazi ndiyo maana tunaona maendeleo makubwa sana na hata hizi takwimu zinazotajwa hapa za idadi vijiji mahali mbalimbali ambako wamefika tunawashukuru. Lakini pia tunawashukuru kwa usimamizi mzuri wa hii miradi mikubwa yote inayotajwa kamati imefanya kazi nzuri na pia imetuletea taarifa hapa ya kazi waliyoifanya pia wamefanya kazi nzuri. Pia, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wamekiri kwamba kamati imewasaidia sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, hizo ziliikuwa ni salamu kwa niaba yenu lakini pia Waheshimiwa Wabunge wote walifanikiwa kuchangia kwa maandishi wengine kwa kuzungumza nanyi michango yenu wengine ni ya kuboresha, mengine ni ya kukumbusha. Lakini kwa ahadi ya Mheshimiwa Waziri na kwa kuwa hii bajeti imeshapitishwa basi tunaamini yale yote yaliyozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge mtaenda kuyafanya kazi.

Lakini na mimi Waheshimiwa Wabunge niungane nanyi kwasababu kama anavyosema Mheshimiwa Spika sisi hatupati fursa ya kuchangia lakini kwa kweli wamefanya kazi nzuri sana hawa watu na mimi naungana na nyie. (*Makofii*)

Maeneo mengi sana yaliyotajwa hakuna Mheshimiwa Mbunge hapa aliyesimama akasema siyo kweli, kwenye eneo langu mimi hawajafika. Kila Mbunge ameелеza kwamba kwake wamefika lakini kuna maeneo kidogo ambayo bado hawajafika na anawakumbusha wafike. Jambo ambalo ni jambo zuri na kwenye hili niwapongeze sana kwasababu pande zote hata Waheshimiwa Wabunge wa Upinzani wameonesha kwamba Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wameshafika kwenye maeneo yao. (*Makofii*)

Pia, kwa ile habari ya bei za umeme kwenye maeneo ya vijijini lakini pia yale ya pembezoni mijini pia niwashukuru sana kwasababu bei ingekuwa kubwa hayo maeneo yako

kama vijiji tu. Kwa hiyo, tunawashukuru kwamba mnachukua hatua kila mnapopewa ushauri, kwa hiyo tunawapongeza sana ninyilakini tunaamini kwamba uongozi wa Mheshimiwa Rais umeturahisishia kazi huko nje kwasababu mmemsaidia vizuri.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge ninaahirisha Shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu Saa Nane Mchana.

*(Saa 11.05 Jioni Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatatu,
Tarehe 11 Mei, 2020 Saa Nane Kamili Mchana)*